

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

21 APRILI, 2012

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi – Tarehe 21 Aprili, 2012

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HOJA ZA KAMATI

**HOJA ZA KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI, KAMATI YA BUNGE
YA FEDHA NA UCHUMI, KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU NA
KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana kwamba tutaendelea leo mpaka saa 7.00. Sasa nitawaita Mheshimiwa Arfi, simwoni, Mheshimiwa Freeman Mbewe simwoni.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Mwongozo wa Spika kuhusu jambo gani. Tunaongozana kabla hatujaanza. Ehee!!! Nani mimi sijamwona asimame. Aha!!! Mheshimiwa John Mnyika Okay.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba mwongozo wako kuhusiana na Kanuni ya 45(3) na kanuni ya 61(1) kuhusu jambo ambalo limetokea hapa Bungeni, nitaomba nirejee Kanuni ya 45 (3) inayosema:

“Iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi au la nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha ataagiza lijiliwe kwa ufasaha zaidi katika kipindi kingine cha Bunge na Kanuni ya 61(1) inatamka:

21 APRIL, 2012

"Wakati wa Majadiliano Bungeni au kwenye Kamati yoyote ya Bunge, Mbunge ataruhusiwa kuzungumza jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi nalo ya kifedha isipokuwa baada ya kusema jinsi anavyohusika nalo na kutaja kiwango cha maslahi hayo.

Mheshimiwa Spika, juzi niliuliza swali la nyongeza.

SPIKA: Tuanze na Kanuni 45

MHE. JOHN J. MNYIKA: Nianze na Kanuni 45.

Mheshimiwa Spika, niliuliza swali la nyongeza kuhusiana na taasisi ya WAMA kutumika kisiasa kwenye Kampeni za Uchaguzi. Mheshimiwa Waziri wakati anajibu alisema si kweli jambo hilo, lakini kwa taarifa za nukuu ya vyombo vya habari za kipindi cha kampeni mke wa Rais Salma Mama Kikwete yeye mwenyewe alinukuliwa akitoa kauli na Mheshimiwa Spika, ukihitaji nakala ya kielelezo nitakiwasilisha mezani chenye kuonyesha kwamba aliitumia WAMA kisiasa wakati wa Kampeni.

Sasa ningeomba Mwongozo wako kuhusiana na kifungu hicho kwa sababu majibu yaliyotolewa hapa Bungeni hayajaridhisha, ningeomba utumie mamlaka yako hayo na niombe Mwongozo wako ili lile swali la nyongeza liweze kupatiwa jibu lenye kuridhisha.

Lakini kwa mujibu wa kifungu cha 61(1) kwenye suala hilo hilo ningeomba Mwongozo wako Kanuni hii inahusu majadiliano, lakini kifungu cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma cha 13 ambacho ndio msingi wa kuingizwa kwenye Kanuni yetu ya Bunge, Kifungu hiki cha 61(1) kinazungumza maslahi kwa upana wake na wakati wote.

Mheshimiwa Spika, imani yangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri alikuwa na taarifa sahihi kabisa kuhusu hili jambo, lakini aliamua kutoa taarifa zisizokuwa za ukweli ndani ya Bunge kwa sababu ana maslahi kwenye hili jambo na leo asubuhi nilikuwa napitia tovuti ya taasisi ya WAMA na nimekuta Mheshimiwa Waziri Sophia Simba ni mmoja wa Wajumbe wa Baraza la Wadhamini la WAMA na wakati wa Kampeni alizunguka pamoja na mke wa Rais. Kwa hiyo, yaliyotokea yote alikuwa anayafahamu, lakini aliamua kwa makusudi kutoa taarifa potofu mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kupata mwongozo wako pale ambapo Mawaziri wanapokuwa wana maslahi kwenye jambo ambalo wanaulizwa Bungeni na wanatoa majibu ambayo yanalinda yale maslahi

21 APRIL, 2012

ambayo wanayo. Mbunge anaweza akachukua hatua gani kwenye jambo kama hilo?

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Ahsante sana, tutatumia muda mwingine maana yake sio lazima tujiridhishe hayo yote sisi hatujui WAMA ni kitu gani. Kwa hiyo, tutatumia nafasi kuweza kujua baadaye. Nasema sijui WAMA ni kitu kama ni taasisi ya Serikali, ni taasisi ya watu binafsi na kadhalika, hiyo mimi sifahamu. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema na mimi ngoja nijiridhishe kadri itakavyofaa tutatoa maelezo wakati muafaka.

Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani shukuru, jambazi wako, jamaa wako amesema Kuhusu Mwongozo, mpaka umewahi. Basi nilikuwa nimekuita, lakini sasa nakuita tena. Nafikiri Mheshimiwa Arfi hayupo, Mheshimiwa Mbewe sasa zamu yako.

Nasema bahati yako mwongozo ndio umekuweka mpaka umefika, ulikuwa umesharukwa. Atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kwanza kuchangia asubuhi ya leo. Kwanza nikubaliane kuunga mkono hoja zote za Taarifa za Kamati na niseme tu kwamba nitachangia kwa kifupi jambo moja la msingi sana ambalo nafikiri Waheshimiwa Wabunge na wewe Mheshimiwa Spika na hata Serikali italitilia maanani. Mchango wa leo sitaukita katika kuelezea matatizo mbalimbali katika Kamati hizo, ila pengine nitajadili zaidi ufumbuzi wa tatizo hilo. Kwa sababu taarifa zimeeleza kwa kina matatizo mbalimbali ambayo yako katika sekta mbalimbali na kwa kweli matatizo haya yataendelea kwa muda mrefu kama hatutatatuwa tatizo la msingi ambalo ningelipenda kuliweka mbele yako kwa ajili ya tafakari ya Waheshimiwa Wabunge, Serikali na hata wananchi wanaotusikiliza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na matatizo makubwa sana ya kiutendaji katika Taifa. Ni lazima tutafakari kwa nini matatizo haya yamekuwa ni matatizo sugu. Ukitikia taarifa ya Miundombinu unaona kuna matatizo mengi sana ya msingi.

Ukisoma taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini unaona kuna tatizo kubwa zaidi la msingi. Ukisoma taarifa ya Mambo ya Nchi za Nje nayo unaona hali kadhalika matatizo kwa kweli ni mengi na ukisoma taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi unaona kama unakata tamaa. Ndiyo hali ambayo iko katika nchi, ndiyo hali ambayo inaonekana inakosa ufumbuzi wa uhakika kwa wananchi.

Sasa mimi katika kulijadili kama nilivyosema sitataka kujielekeza kwenye tukio moja baada ya jingine ila ni kama Taifa tunafikiria tunaweza vipi tukatoka katika hii, *dilemma* ambayo sisi tunayo nchi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni kubwa sana na kwa ukubwa wa nchi hii tuna tatizo moja la msingi ambalo tunalundika madaraka kwa Waziri kwa msingi kwamba tunaweka yote ya kusimamia uchumi na maisha ya Watanzania kwa kundi la Mawaziri ambao kwa kweli wanazidiwa.

Mheshimiwa Spika, utakavyofanya vyotevyote vile, utakavyobadilisha Mawaziri vyotevyote vile kama huku-address tatizo la msingi la mfumo wetu mzima wa utawala na uongozi bado utakuwa pale pale. Ambacho nawaomba Watanzania walitafakari kwa kina ni kwmaba tunakwenda kama Taifa katika kuanzisha ama kuandika upya Katiba ya Taifa letu ambayo pengine inaweza ikatupa mwanga mpya wa matumaini wa namna gani tuendeshe nchi yetu, namna gani tutajitawala, namna gani tutawale rasilimali ambazo Taifa hili limejaliwa kwa wingi sana.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali ni kwamba utawalaumu Mawaziri, utailaumu Serikali, utawalaumu Wakurugenzi, utalaumu kila mtu ambaye ana mamlaka ya kiutendaji, lakini kama tunabakiza mfumo huu huu wa utawala ambapo madai yote tunayalundika kwenye kapu moja Dar es Salaam kwamba una Waziri mmoja ambaye anasimamia madini yote Tanzania, una Waziri mmoja ambaye anasimamia madini yote kwa maana ya mafuta, gesi, umeme ni dhahiri huyu mtu anahitaji kuwa na *super natural powers* kuweza ku-perform kazi zake kwa ufanisi.

Kwa hiyo, kuna umuhimu sana katika kutengeneza ile *structure* ya utawala wa Taifa na namma ya usimamizi wa rasilimali za Taifa tuangalie madaraka yetu haya tunayagawa vipi.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tumezungumza mara nyingi kwamba tunahitaji kuji-decentralised nchi, hatuwezi kuendelea kuweka mamlaka yote kwenye Serikali ambayo iko Dar es Salaam kwamba Waziri mmoja anasimamia kilimo nchi nzima.

Kwa hiyo Waziri mmoja akifanya uzembe basi tatizo la pembejeo linakuwa Tanzania nzima kuna tatizo la pembejeo kwa sababu ya *central planning*. Sasa ni lazima tugawe haya mamlaka.

Katika Katiba tuangalie tuna-decentralise VIPI mamlaka na sio tu ku-decentralise utendaji lakini wakati huo huo Serikali Kuu ikawa inahodhi ya mapato yote ya kitaifa kiasi kwamba Halmashauri zetu za Wilaya zinategemea Serikali Kuu kwa asilimia kati ya 93 mpaka 97 au 98.

Sasa kama Serikali Kuu inaweza ika-control mapato kwa asilimia 98 hakika wale watu kule chini kote kwenye Wilaya zote, Mikoa yote kila mmoja anangojea Serikali Kuu iweze kutenda. Uzembe wa Waziri mmoja wa Nishati na Madini, ama makosa yaliyofanywa katika *central level* kwa maana ya Waziri ama Serikali katika ngazi ya juu basi nchi nzima inaingia gizani. Ni lazima tuweze kufikiria sasa tuanzishe utaratibu wa kwamba Serikali za Majimbo ambazo zinaweza tukagawana mamlaka haya ya kusimamia rasilimali za Taifa hili.

Kwa bahati mbaya sana kwamba watu wanafikiri Serikali za Majimbo ambazo CHADEMA huwa tunazungumzia mara nyingi labda ni Serikali za Kibaguzi ama Serikali za Kikabila, ukweli sio ukabila.

Sisi tunapendekeza kwamba Serikali za Majimbo tunazozizungumzia za kutawala na kuongoza nchi hii ziwe pengine kama saba ama nane na hakuna mkoaa mmoja ambaa utakuwa ni jimbo kama tutakubaliana kwenye Katiba Mpya tuwe na Majimbo mapya basi mikoa kama minne au mitano ndio inaunda Jimbo moja. Hakika tatizo la ukabila halitakuwepo. Lakini angalau tutakuwa tumeondoa *risk* ya kulundika mlundiko wote wa majukumu yote ya Kitaifa kwa kundi moja dogo la watu.

Mheshimiwa Spika, ninayozungumza hii ni pamoja na kuangalia mifumo yote sasa ya kodi, uchumi mkuu tunausimamia VIPI, mamlaka katika maeneo mbalimbali na si kweli dhana inayojengwa kwamba eti kuna mikoa ambayo itakuwa haina rasilimali, miaka kumi iliyopita kila mtu alikuwa anafikiri Mkoa wa Lindi na Mtwara ni mikoa maskini, lakini leo Mikoa ya Lindi na Mtwara inaonekana ni mikoa yenye utajiri mkubwa wa *natural resources* kuliko mkoaa mwingine wowote katika nchi hii.

Vile vile mikoa yote ina watu na hakuna rasilimali kubwa katika jamii kama *human resource*. Tatizo la *human resource* nchi yetu halipo kwa sababu tuna watu wengi tunaweza tukawa na tatizo la *skilled human resource*, lakini *human resource passé* tunayo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mchango wangu ni huo tu ambaa nilitaka niulete kwenye kikao hiki ili watu waanze kulifikiria kwamba tusitafute *temporary solution* tunachofanya sasa hivi hapa Bungeni nyingi kweli zina msingi zinasaidia, lakini ni *temporary solution* kwamba

unamwondoa huyu unamwingiza huyu, utamwondoa huyu utamwingiza huyu, sawa tufanye hivyo kwa sababu ni lazima ili kuongeza ufanisi katika Serikali. Lakini *in the long time* kwa sababu tunaandika Katiba Mpya ninataka Watanzania wote wafikirie kwa kina sana hoja ya *decentralisation*.

Chama cha Mapinduzi (CCM) waitafakari, CHADEMA waitafakari, CUF waitafakari, TLP, NCCR-MAGEUZI, dini zote zitafakari jambo hili ni hoja ya msingi sana kama tunataka kuweza kupata matumaini mapya ambapo sasa tutajenga hata ushindani wa ndani katika provinces mbalimbali katika Taifa zikaweza kila mmoja kinajipa kipaumbele chake badala ya kupanga sera zetu zote ambazo zinakuwa *central* na *Local Government* zetu tunazi *degrade* kabisa zinakuwa hazina maana hazina mchango, hazina mapato zinabaki kuwa omniaomba na tunaomba Serikali Kuu, Serikali Kuu kila siku inatereza, hakika hatuwezi kuendelea kuifikisha nchi hii katika kapu moja la mayai kama ambavyo liliivo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilisema mchango wangu katika jambo hili ujikite katika hilo ili Watanzania iwe ni *food for thought* tunavyokwenda kwenye Katiba Mpya. Ahsante sana. (Makof)

SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mussa Haji Kombo sijui yupo? Mheshimiwa Assumpter Mshama simwoni, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge. Dkt. Binilith Mahenge, alizungumza jana, Mheshimiwa Selemani Zedi, hayupo. Mheshimiwa Kigola naye nafikiri hayupo, Mheshimiwa John Mnyika alaah!!! Kigola, okay nilichanganya na Lugola. Tafadhali Mheshimiwa Menrad Kigola.

MHE. MENRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Napenda nianze kuchangia moja kwa moja na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nitoe shukrani zangu kwa Serikali kwa kazi nzuri walioifanya katika Jimbo langu na tukiongelea Uchumi ina maana kwamba tunalenga masuala ya miundombinu. Tukiimarisha miundombinu tuna uhakika kabisa uchumi unaweza ukakua. Tukiuzungumzia uchumi tunaangalia kule vijijini na vijijini kule tukiimarisha barabara zetu tuna maana kwamba wakulima wote wanaweza wakasafirisha mazao bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwenye jimbo langu kuweza kufanikisha barabara tano ambazo zilikuwa zinazunguka katika Jimbo langu na wananchi wangu sasa hivi walikuwa wanapata shida sana

21 APRIL, 2012

kusafirisha mazao yao sasa hivi wanasafirisha bila matatizo. Nikianza na barabara ambayo inatoka Mtanana kwenda Nyololo, sasa hivi iko vizuri.

Kuna barabara inatoka Nyololo kwenda Maduma ambayo ilikuwa miaka mingi kama miaka 20 iliyopita ilikuwa haijawahi kupitiwa na greda lolote sasa hivi inapitika vizuri. Nikianza na barabara kutoka Nyigo kwenda Kiyowela nayo inapitika na barabara ya kutoka Kasanga kwenda Mtambula. Kwa kweli naishukuru sana Serikali kwa juhudini walizozifanya na hii wananchi wangu inaonyesha kwamba Serikali inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo napenda kuipongeza Wizara ya Ujenzi nakumbuka kipindi kilichopita niliuliza swali la kuhusiana na barabara ya kutoka Nyololo kwenda Igowole mpaka Mgololo. Ile barabara ni ya muhimu sana katika uchumi wa Tanzania. Kuna viwanda vingi sana siwezi kuvitaja hapa kwa sababu vinajulikana. Kwa mfano viwanda vya chai viko pale. Kiwanda kile cha Mgololo ni kikubwa na uzalishaji ni mkubwa unafanyika pale ambao unaingiza pato kubwa kwa Taifa letu.

Kuna viwanda vingine vya chai pamoja na viwanda vya mbao ile barabara ni muhimu na bahati nzuri sana katika kikao chetu cha mkoa walishapitisha na napenda nitoe shukrani kwa Serikali kwamba Waziri alijibu alisema mwaka huu 2012/2013 katika Bajeti inayokuja tutaiweka tayari kwa kufanya upembuzi yakinifu. (*Makofii*)

Kwa hiyo napenda nisisitize tu katika Bajeti hii barabara wasijisahau kwa sababu ni barabara ya muhimu sana katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ile barabara inasumbua, inabidi itengenezwe kwa kiwango cha lami sio kokoto tena. Kwa sababu ukiangalia Wilaya ya Mufindi katika uzalishaji mkubwa unatoka katika barabara ile. Sasa tukiweka kiwango cha lami maana yake kuna magari makubwa sana yanapita pale.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kwenye Bajeti inayokuja kesho kutwa ambayo tunaanza mwezi Juni barabara ile ifikiriwe kuwekewa kiwango cha lami sio kokoto tena kwa sababu ni ya muhimu sana Kitaifa. Nadhani Naibu Waziri wa Ujenzi yupo na yeye ananisikia nadhani hiyo itaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la pili tuna stendi pale Mafinga. Ile stendi ya Mafinga inaunganisha majimbo mawili, jimbo la Kaskazini na jimbo la

21 APRIL, 2012

Mufindi Kusini. Sasa ile stendi ni kwamba magari yote yanaenda kusini mwa Afrika yanapita pale.

Mheshimiwa Spika, nikisema Kusini mwa Afrika ina maana kwamba magari yanayoenda Zambia yanapita pale na magari yanayoenda Malawi yanapita pale, magari yote ya Songea mabasi yote yanapita pale. (*Makofi*)

Sasa ile *Stand* ukiingalia haina hadhi kwamba ni stand ya Wilaya yetu ya Mufindi. Naiomba Serikali kwa sababu tukisema kwamba kuna Tsunami, kuna Tsunami zingine za upepo. Pale kuna upepo unavuma lile vumbi sijawahilliona. Sasa naiomba Serikali ile barabara kuanzia Bajeti inayokuja tuweke kiwango cha lami ile *stand* ya Mafinga na pale ile stand mabasi mengi sana yanaingia pale na wafanyabiashara wetu vijana wanashindwa kufanya biashara vizuri kwa sababu kuna ajali nydingi zinatokea katika *stand* ile.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi huwa siiti *stand* ile ni kona fulani. Kwa hiyo, Naibu Waziri wa Ujenzi nadhani ananisikia na yeye bahati nzuri sana huwa anapita pale, anaifahamu na bahati nzuri hata Spika wewe mwenyewe wakati unaenda Njombe lazima apite kwenye stand ile. Kwa hiyo nadhani Serikali inanisikia kwenye Bajeti hii wasitusahau wa Mafinga kwa sababu ni *stand* muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili naomba nichangie kwa upande wa Nishati na Madini. Naomba niongelee masuala ya umeme. Mimi siku zote huwa nasema umeme sio zawadi. Umeme ni haki ya mtu kupewa. Sasa wewe ukisema umeme ni zawadi wa kumpatia mtu hapa inakuwa sio sahihi. Kila kijiji inabidi kipewe umeme, sisi kwetu kule siku zote huwa naongea kwamba kwa mfano masuala ya nguzo za umeme sisi zipo nydingi tu.

Tuna nguzo zingine ambazo tunaweza tukazitumia kama kuni kwa sababu ni nydingi. Sasa mimi nashangaa vijiji vyetu vingi pale havina umeme lakini kuna tatizo moja ambalo ni kubwa linajitokeza sasa hivi. Kuna tatizo la *transfoma*. Bahati nzuri sana napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Nishati na Madini alitembelea kule na bahati nzuri alitembelea kwenye vijiji vingine havijawahi kupitiwa na Waziri tangu Uhuru, lakini yeye alifika kijiji kimoja na Ihomasa. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kijiji cha Kitasengwa pale nadhani ulishaahidi mwezi huu wa nne utapeleka pale *transfoma* na bahati mbaya mpaka sasa hivi haijafika, watu wanaulizia kwanini haijafika wakati tuliahidiwa. Lakini imejitokeza kwamba *transfoma* imekuwa ni

tatizo kubwa katika Wizara hii. Tuna vijiji pale, kwa mfano Kihanga tulishafanya *wiring* tayari, Muninga walifanya *wiring*, Kitasengwa walishafanya *wiring* lakini hatuna *transifoma*.

Sasa ninaiomba Wizara hii suala la *transifoma* inaonekana ni *critical problem*. Hebu wajitahidi, vijiji vyote ambavyo vimeshafanya *wiring* waweze kupewa *transifoma* waweze kufanya kazi yao. Kuna kijiji kingine cha Malangali ambacho kiko katika Kata ambayo ina Sekondari kubwa sana, nadhani wasomi wengi wa Dar es Salaam wamesoma katika Shule ya Malangali Sekondari. (*Makofi*)

Sasa cha ajabu katika Kata ya Malangali ambayo inafanya uzalishaji mkubwa wa kilimo cha alizeti lakini mpaka leo hii haina umeme. Naomba hili nisiliongelee sana kwa sababu Naibu Waziri wa Nishati na Madini tulishakaa tukaliongea akasema kwamba hili atalifuatilia kiundani zaidi na tulipokuwa pale Mafinga tulimweleza na yeye akakubaliana na sisi.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sana tatizo la pale hata Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba Kata ya Malangali itapewa umeme. Sasa isipite miaka mingi sana watu hawajapewa umeme. Sasa ninaiomba Serikali, wakati tunasubiri mambo mengine tuanze kuweka nguzo kwa sababu nguzo zipo na tunaweza tukaanza kupata umeme, tukaanza kupata nyaya na kuna vifaa vingine havipo.

Lakini tuanze kuweka nguzo na pale tunapopata vifaa vingine iwe tayari tunaweka umeme unawaka haraka. Mpaka sasa hivi tunaingia kwenye Bajeti inayokuja hata nguzo hatujaanza kuweka. Mimi nilikuwa namshauri Waziri wa Nishati na Madini, pale kuna makampuni mengi sana. Wewe ukitoa sauti tu kwamba waanze kuweka nguzo pale wataanza kuweka. Kwa sababu nguzo zipo na tunazalisha sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, napenda nitoe pongezi kwa kampuni ya *Mwenga Co. Ltd.*, *Mwenga Co. Ltd.* wameahidi kutoa, au *ku-supply* umeme katika vijiji kama 14. Kwa bahati nzuri hata kwenye Jimbo langu kuna Kata moja ya Luhunga ambayo ina vijiji vitano itapata faida kutoka umeme wa *Mwenga Company*. Hilo napongeza sana, napenda kuishukuru sana Serikali ya CCM kwa kuungana na wadau ambaao wanaweza kuingiza umeme katika vijiji vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pongezi wa kampuni ya *Sao Hill* ambaao sasa hivi katika *plan* yao wameamua *ku-supply* umeme wao katika vijiji 31. Sasa naiomba Serikali kwa makampuni haya

ambayo yana-supply umeme watoe ushirikiano mzuri ili vile vijiji ambavyo vimikuwa highlighted kupata umeme viweze kupata umeme haraka.

Sasa ikaonekana tena Serikali kukwamisha hii itakuwa si vizuri sana. Makampuni yameonyesha kwamba yanaweza yaka-supply umeme naiomba Serikali iweze kusimamia vizuri, ili tuweze kupata umeme katika vijiji vyetu. Kuna vijiji vingine ambavyo vinafanya uzalishaji mkubwa sana. Kwa mfano kuna kijiji kimoja cha Mtambula. Ukienda Mtambula, ukienda Idunda, ukienda Itandula, ukienda Makungu kuna uzalishaji mkubwa sana. Haya kuna vijiji vile vya Lugolofi, bado wanalinda nyaya mpaka leo, nyaya zimepita juu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali hivi vijiji ambavyo vinafanya uzalishaji mkubwa na umeme uko kama kilomita mbili, tatu basi viweze kupewa umeme. Hii itasaidia sana kupata wananchi wetu, tunasema kwamba tunaweza kupunguza ukali wa maisha wataweza kufanya biashara za majumbani. Vijana wetu wanaweza kujiajiri. Umeme unaleta maendeleo makubwa sana sehemu unakopatikana. Sasa naiomba Serikali kwenye Jimbo langu mimi kwa sababu watu wanafanya kazi, ninaomba vile vijiji vyote viweze kupewa umeme ambavyo vinafanya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tuna mashirika makubwa sana pale, sasa kuna mashirika mengine yako pale, unaweza kuona kwamba kwenye mashirika kule walijenga majengo mengi sana ya wafanyakazi. Lakini yale majengo hayana umeme, sasa ndiyo maana nasema umeme sio zawadi. Kila mmoja anastahili kupata umeme. Dunia ya leo ukiona mtu hana umeme nyumbani basi huwa tunashangaa kidogo kwa sababu hata wapiga kura wangu sasa hivi wangkuwa wanania wakati mimi naongea hapa.

Sasa hivi wananchi wangu hawawezi kuniona na kuna vijiji vingine hata radio hakuna. Sasa tukianza kuongelea kwamba kama radio hazipo kwanini wakose umeme wakati umeme inabidi wapewe. Ninaiomba Serikali umeme usichukuliwe kama ni zawadi, umeme ni jukumu la kila mwananchi aweze kupewa bila kukosa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, (Makofi)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba na mimi nichangie kuhusiana na taarifa nne za Kamati ambazo ziko mbele yetu na leo nitaomba nichangie kuhusu jambo moja tu la uwajibikaji dhidi ya ufisadi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze na taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi. Taarifa imeanisha na mimi ninaunga mkono taarifa hii kwamba kuna changamoto kubwa ya mfumuko wa bei, ongezeko la bei, kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi na hali tete ya uchumi wa nchi yetu kutokana na matumizi makubwa ya Serikali kuliko makusanyo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni jambo kubwa sana na kwa kweli Serikali ilichukulie kwa uzito mkubwa kwa sababu nchi nyingi ambazo sasa hivi kuna machafuko na migogoro, suala la mfumuko wa bei na kuongezeka kwa gharama za maisha na hali ngumu ya maisha ni moja ya kichocheo kikubwa sana. Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati chanzo kikubwa cha mfumuko wetu wa bei takribani asilimia 70 ni chakula.

Mheshimiwa Spika, bei ya chakula. Pamoja na kuunga mkono taarifa ya Kamati kuna jambo moja ningependa niliweke bayana ambalo linaathari kubwa sana kwa wananchi wa Ubungo na wananchi wa Dar es Saaam kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoa chakula kutoka kwenye Hifadhi ya Taifa kwa gharama ya mlipakodi, pamoja na Serikali kupunguza kodi kwa baadhi ya vyakula muhimu lakini bei ya vyakula iko juu, tofauti na maneno ya Serikali na ahadi za Serikali hapa Bungeni. Hii hali iko hivi kutokana na kukosekana kwa uwajibikaji, kutokana na ufisadi. (*Makofii*)

Sasa pamoja na rai ya kutaka Waziri wa Fedha ajiuzulu kwa kushindwa kusimamia hii Wizara. Mimi naomba taifa letu liende mbele zaidi. Ni muhimu sana ukaguzi maalum ukafanyika, kwenye huu mchakato mzima wa matumizi ya vyakula kutoka ghala la taifa, kwenye mchakato mzima wa misamaha ya kodi ambayo misamaha mpaka sasa hivi ni zaidi ya takribani trillioni moja kwa taifa letu wakati ambapo haina manufaa kwa Mtanzania wa kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naamini ukaguzi maalum ukifanyika kuhusu misamaha hii ya kodi ya zaidi ya takribani trillioni moja, ufisadi zaidi utajulikana na hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wote waliota misamaha ya kodi kinyemela. Taifa letu deni linaongezeka na deni hili linaongezeka kwa kweli kwa Ari, Kasi na Nguvu zaidi na kama hatutachukua hatua kudhibiti hali hii uchumi wa nchi yetu uko mashakani. (*Makofii*)

Pamoja na hatua ambazo zimependekezwa na Kamati ningeomba Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum kwenye akaunti ya deni la taifa ili watanzania waweze kufahamu mchakato mzima uliosababisha deni la taifa kukua kwa kiwango hicho ambapo kwa kiwango kikubwa kinachangiwa na matumizi ya anasa ya Serikali, matumizi yenye ubadhirifu ambao mwisho wa siku anayebeba mzigo ni Mtanzania maskini. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sasa nihamie kwenye taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini. Mimi ni mjumbe wa Kamati hii na ninaunga mkono mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati. Mara kwa mara tumesema hapa Bungeni kwamba Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kweli na narudia tena kwa mara nyingine tena ukipitia hii taarifa ya Kamati na ukipitia makandokando mengine, unaweza kujiuliza ni kwanini mpaka hivi sasa Waziri wa Nishati na Madini yupo ofisini na udhaifu wote uliomo humu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tusipochukua hatua za kuwajibishana itakumbukwa kwamba mwaka 2008, taifa lilikuwa kwenye hali kama hii wakati wa ripoti ya Kamati Teule ya Bunge kwenye Wizara hii hii ya Nishati na Madini. Lakini kwa kuwa tuna kawaida ya kuchukua hatua nusu nusu, leo ni mwaka 2012 tunarudi tena kujadili ufisadi kwenye Wizara hii ya Nishati na Madini. Ufisadi unaohusu mafuta ya IPTL, ufisadi unaohusu maeneo mengine ya Wizara hii. Mimi nitaomba sana na kwa kweli Mheshimiwa Rais na watu wanaomshauri walichukue hili jambo kwa uzito wake.

Mheshimiwa Spika, kujiuzulu kwa Mawaziri ni hatua moja na ni hatua muhimu sana lakini lazima Mheshimiwa Rais kwa mamlaka yake aliyonayo kwa mujibu wa Katiba pamoja na Mawaziri kujiuzulu achukue hatua za ziada. Kwa sababu leo Mawaziri wa Nishati na Madini waliokuwa *implicated* mwaka 2008 wangechukuliwa hatua za kufaa ingekuwa somo kwa Mawaziri mengine hali hii isingejirudia tena. (Makof)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono mapendekezo ya Kamati kwa sekta hii nyeti na kwa hali ya nchi yetu sasa hivi ya utafutaji wa mafuta na gesi na migogoro kwenye sekta ya umeme, kwenye migogoro kwenye biashara ya mafuta na mazonge yaliyomo humu kama ambavyo Kamati imedokeza lakini kwa sababu ya muda sitasema mengi yaliyojificha nyuma ya pazia.

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba kwa Mheshimiwa Rais atumie mamlaka yake. Mimi naamini kabisa Rais akitumia mamlaka yake ya kikatiba ana uwezo wa kusafisha na kwa sababu mpaka leo tunaendelea

kuzunguka kwenye masuala ya Nishati na Madini wakati ambapo yanaweza kumalizika.

Mheshimiwa Spika, nihamie kwenye taarifa ya Kamati ya Miundombinu. Hili la Bandari lina pande mbili za hadithi. Pamoja na Waziri wa Uchukuzi kuwajibika ningeomba vilevile kwamba uchunguzi wa ziada ukafanyika. Kwa sababu pamoja na maelezo yaliyomo kwenye Kamati, kuna taarifa za nyongeza kwamba jambo hili la ujenzi wa gati na jambo hili la *SBM* yote mawili yana utata pande zote. Sasa ili tuweze kushughulikia maeneo yote mawili katika hili la Wizara ya Miundombinu, ningeomba sana kuundwe Kamati Teule ikachunguze kwa undani sana suala hili.

Lakini hili suala la msongamano lilitotajwa Dar es Salaam naomba nisitumie muda mrefu kuzungumza kwa sababu kinachokosekana ni dhamira tu ya kisasa. Leo tunazungumza kuhusu kupandishwa hadhi kwa barabara 27 na naunga mkono mapendekezo ya Kamati. Lakini hili jambo limekwishasemwa miaka mingi iliyopita, mapendekezo yalishapelekwa Manispaa toka mwaka 2009 yakarudiwa 2010, yakarudiwa 2012 Waziri aliahidi humu Bungeni kwamba tarehe 15 Machi, 2012 barabara zingepandishwa hadhi angetoa taarifa kwa ajili ya kupunguza foleni, lakini mpaka sasa bado kunatolewa jibu, wataalam wanaendelea na uchunguzi.

Kwa hiyo, ili kupunguza foleni za Dar es Salaam ningeomba kwamba barabara hizi zipandishwe hadhi haraka zikiwemo za Jimbo la Ubungo lakini pesa zilizotokana na ongezeko la kodi ya mafuta ya taa, pesa zilizotokana na ushuru wa barabara kuongezeka nje ya Bajeti baada ya uchakachuaji kupungua zitumike kuja kujenga barabara za pembezoni.

Mheshimiwa Spika, nimalize na taarifa ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Nimepitia taarifa ya Kamati na naunga mkono mapendekezo mengine na naomba kwenye hili suala la maslahi ya Askari Polisi tuletewe vilevile taarifa ya Kamati ya Masha ambayo ilipendekeza nyongeza kwenye mishahara na posho za Askari. Lakini jambo moja sijalionia. Mwaka 2010 mwezi Februari, Bunge liliazimia kwamba maazimio ya Kamati Teule ya Bunge Kuhusu *Richmond* ambayo yalikuwa hayajatekelezwa bado yapelekwe kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa ajili ya hatua zaidi.

Leo tunalalamika kuhusu mikataba mibovu, kulikuwa na maazimio ya uwazi wa mikataba ambayo hayajatekelezwa. Leo tunalalamika kuhusu Mawaziri waliohusika na ufisadi na kwa mujibu wa Maazimio ya

Bunge ilikuwa uchunguzi uendelee na hatua zichukuliwe. Lakini Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo Mwenyekiti wake ni baadhi ya watu waliotajwa kwenye kashfa ya *Richmond* hajaeleza kwenye taarifa yake hatua zilizochukuliwa. (*Makofi*)

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika taarifa zile ambazo zimewasilisha mezani. Mchango wangu mimi nitatoa kwa Kamati ya Nishati na madini na sana sana nitaongelea suala la umeme.

Katika taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini, ukurasa wa nne(4), wametamka kabisa wazi kwamba maeneo mengi ndani ya nchi yamekosa umeme wa uhakika kwa sababu ya miundombinu yake kuharibika mara kwa mara.

Lakini pamoja na sababu hizi, sababu kubwa ninayoiona mimi ni kwamba Wizara ya Nishati na Madini na *institutions* zake zote zilizo chini ya Wizara hiyo zimeshindwa kuwajibika kikamilifu na hivyo kuleta usumbufu mkubwa wa ukosefu wa umeme wa uhakika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwanini nasema hivi, masuala mengine ni kweli ni makubwa yanahitaji kuchukua muda kufanya maamuzi. Lakini mengine ni madogo sana ambayo hayahitaji kuchukua muda sana kufanya maamuzi. Masuala ambayo hayahitaji muda mrefu na hayahitaji kutumia akili nydingi ni kama vile ukosefu wa *diesel* unapotokea wa kuendeshea jenerata au ukosefu wa vipuri unapotokea kwa jenereta zile ambazo zimeharibika.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu wamelalamika, wengi wameongea sana; mimi naiomba sana Wizara iwe iwajibike, itekeleze majukumu yake kikamilifu ili iweze kuwapatia wananchi wa maeneo mbalimbali umeme wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi nilisimama nikamwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Nilichomekea swali lile kusudi, baada ya kuwafuata watu wa Wizara ya Nishati mara kwa mara bila kupata majibu yanayofaa. Hii inasikitisha. Hapa ninapoongea, Wilaya yangu ya Liwale ina matatizo ya umeme takriban miezi sita sasa. Tatizo ni *spare* ya jenereta ndogo tu ambayo inaweza kuagizwa Ulaya kwa muda wa wiki tatu, ikaja kwa *DHL* au kwa *FedEx Couriers*, katika muda wa wiki tatu imefika hapa. Sasa hivi ni miezi sita, *spare* hakuna, jenereta halifanyi kazi, wananchi hawana umeme. Hivi ni kweli kwa sababu gani inakuwa hivi?

Mheshimiwa Spika, na *spare* ikifika, unaambiwa mafuta ya *diesel* ya kuendeshea jenereta hizo hakuna, inachukua tena mwezi. Hii inaonesha *completely irresponsibilities* kwa Wizara ya Nishati na Madini na *institutions* zake zote zilizo chini ya Wizara hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale ina matatizo ya umeme kwa muda mrefu mno. Wilaya ya Liwale ipo Mkao wa Lindi ambaa una Wilaya sita na juzi nilisema Wilaya zote zina umeme kasoro Wilaya hii. Kwa sababu gani?

Kwa nini Wilaya ya Liwale inakosa umeme wa Gridi ya Taifa wakati ipo ndani ya Mkao ambaa unazalisha umeme wa Songas? Kwa nini tusiunganishwe kwenye umeme wa Gridi ya Taifa? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini, inatumia *diesel* nydingi sana kila mwezi zaidi ya lita 35,000 kwa ajili ya kuendeshea jenereta wakati umeme wa Gridi ya Taifa upo pale, ambapo wangechukua *wakau-connect* kwenye Wilaya ile na tatizo likaisha, *expenditure* za mafuta zisingekuwepo tena. Serikali hivi kweli inahitaji kuwaza hili ni kwa sababu gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba sana Wizara ya Nishati, nimeshawasiliana na Waziri mara nydingi na nimeshawasiliana na watu wa TANESCO mara nydingi. Mtuhurumie, tunaomba sasa mtupelekee umeme. Inawezekana kabisa kupeleka umeme Wilaya ya Liwale ukitokea Nangurukuru, ukafika Njinjo, ukafika Miguruwe, ukafika Zinga, ukafika Kimambi, ukafika Kichonda, ukafika mpaka Liwale na sisi adha ikatupungua. Kama hiyo haitoshi au haiwezekani, basi tuunganisheni umeme kutoka Wilaya ya Ruangwa ufile Mmero, Lionja, Nangano, Kibutuka, Kiangara na Liwale. Tutakuwa na sisi tumetatu tatizo la umeme, lakini pia Serikali itakuwa imepunguza gharama za mafuta; ni nydingi mno zinatumika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie sasa suala la madini. Wilaya ya Liwale ina madini mengi sana, lakini mimi nafikiri kuna haja ya kurekebisha Sheria za Madini zilizopo. Sheria za Madini zilizopo sasa hivi zinawakandamiza wananchi na wamiliki wadogo wadogo ambaa wapo kwenye maeneo yale. Kwa mfano, inapotokea mmiliki mdogo yuko pale, mchimbaji mdogo yuko pale au mkazi wa kawaida yuko pale na akaja mwekezaji ambaye anakuja kuchimba yale madini, huyu mkazi au mmiliki analipwa fidia ndogo na huyu mwekezaji anafaidika, wale walioko pale wanapata hasara, maeneo yao yanachukuliwa, madini yanachimbwa yanabakia mashimo na mazingira yanaharibika. Hilo moja.

Mheshimiwa Spika, la pili, Wizara ya Nishati na Madini, watu mnaowapa vibali vya kwenda kumilikishwa migodi na machimbo, wanafanya kazi za ziada za kupasua mbao ambazo hawajaruhusiwa; ni kwa nini? Wanakwenda kwa kazi ya kuchimba madini, wanachimba, wanakata sasa na mbao ambazo wanazipitisha huko huko kwenye mapori bila vibali, malori kwa malori wanatoka nazo nje ya Wilaya. Kwa kweli hawatutendei haki. (*Makofi*)

Waziri wa Nishati na ofisi yako, tunaomba ulichunguze hili, mbao zetu zinaibiwa malori kwa malori. Wanafanya kazi mbili kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nasikiliza toka mnaanza kuchangia, zile hoja zipo nne, lakini maneno mnayosema utafikiri tupo kwenye *Budget Session* na mara zote mnatoka nje ya utaratibu. Nimesikiliza toka tumeanza hapa, watu wanatoka nje kabisa! Hotuba zile za kuwajibika zilikuwa zaidi kwenye *Watchdog Committees*, tulimaliza; watu wanaendelea tu. Sasa naomba tafadhali mjizatiti kwenye maeneo ya Kamati na kuna maazimio yake. Mawaziri wakipenda kujibu, watajibu kwenye maazimio yale ya Kamati. Haya mengine mtazungumza mwezi Juni mpaka mchoke. Kwa hiyo, msiende "kwetu hakuna nini wala nini." Mbona hizi taarifa hazikusema hivi.

Nilisema nitamwita Mheshimiwa Kaika Telele, atafuatiwa na Mheshimiwa Assumper Mshama na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya pia ajiandae.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nizungumzie kidogo hizi Taarifa za Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Nishati na Madini: Mimi napenda niishukuru sana Serikali kwa sababu baada ya Miaka 50 ya Uhuru, Serikali ya Awamu ya Nne, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ilitupatia umeme katika Wilaya ya Ngorongoro. Wilaya ambayo ilianzishwa mwaka 1979 sasa ndiyo tunapata umeme, lakini si haba, tumechelewa lakini tumepata. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kumbe kuona ni kusaidiki; mwaka 2007, Rais alifanya ziara katika Wilaya ya Ngorongoro na akaona haya matatizo makubwa, aliporejea akaahidi na ahadi hiyo sasa imetekelizwa.

Umeme huu bado haujaanza kuwasaidia wananchi kwa sababu

ya upungufu ambao bado upo; nguzo hakuna na usambazaji wa umeme wenyewe bado ni wa mashaka sana. Ningependa nimwombe Waziri wa Nishati na Madini kwamba, tatizo kubwa tulilopata ni kwamba, walitupa ile *offer, grace period* ya kulipa shilingi 75,000 kwa ajili ya kuwahamasisha wananchi *against* shilingi 400,000 ambayo ni bei ya TANESCO. Sasa kwa sababu wamechelewa kuleta nguzo, hakuna jambo kubwa liliofanyika, tulishindwa kutumia nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Nishati na Madini, azungumze na watu wa REA ili tuweze kupata huo msamaha turudi kwenye shilingi 75,000 na nina hakika wananchi 300 watafikiwa katika usambazaji huo wa umeme.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Taasisi muhimu za Serikali kama Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Polisi, Magereza, Boma ya DC, Hospitali ya Waso na Sekondari ya Loliondo, hizi zote ni taasisi muhimu lakini bado hawajaunganishiwa umeme. Naomba hata kabla umeme haujaenda kwa watu binafsi, Wananchi wa kawaida na Taasisi hizo ziweze kupata umeme. Taasisi pekee ambayo imepata umeme kwa sasa ni Benki ya NMB Loliondo.

Mheshimiwa Spika, miundombinu: Mimi napakana na uwanda mrefu sana wa nchi jirani ya Kenya. Sasa, sina barabara za uhakika na barabara ni *engine* ya uchumi. Ninaiomba sana Serikali kwa kuwa ilishaweka hii Barabara ya Mto wa Mbu – Angaresero – Loliondo – Musoma katika llani ya Uchaguzi ya CCM, jambo hilo litekelezwe, isije ikawa imewekwa kwenye llani halafu haitekelezwi. Barabara hii ina kelele sana, lakini namwomba Mheshimiwa Rais asimame na itekelezwe kama ambavyo ameahidi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia uwanda huu ambao ni mrefu sana, katika maeleo ya Kamati imezungumzwa habari ya kuanzishwa tena kwa JKT katika maeneo. Ningependa maeneo ya mipakani, Serikali iangalie sana katika kuweka vyombo vya ulinzi na usalama. Ningependa sana kama ingewezekana *Detach* ya Jeshi iwepo kule Loliondo kwa sababu ya uwanda mrefu sana ambao tunapakana na nchi jirani na kwamba kuna mwingiliano mkubwa wa watu, kuna njia nyingi za panya, kuna minada mingi mipakani na mambo kadha wa kadha. Kwa hiyo, kama *Detach* ya Jeshi haiwezekani, basi Kambi ya JKT ianzishwe katika Wilaya ya Ngorongoro, inaweza ikasaidia mambo mengi. Hii ipo pia katika *recommendation* ya Kamati kwamba, masuala ya ulinzi na usalama yanaweza yakaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwanda mrefu namna hiyo, tuna vituo vitatu tu vya Polisi; tuna kituo pale Ololosokwan na tuna vituo mahali pengine kule Jema na Ngaresero. Maeneo ya Pinyinyi inatakiwa kuweka Kituo cha Polisi kwa ajili ya kulinda rasilimali zetu na kulinda wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngorongoro kama nilivyo sema, haina barabara ya uhakika, lakini kuna kazi kubwa sana imefanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro katika kutengeneza baadhi ya barabara ambazo zipo ndani ya Tarafa ya Ngorongoro kwa ajili ya *movement* ya watalii, kwa mfano, sehemu za Ndutu, barabara ya kutoka Laitolle kwenda Ndutu, barabara kutoka Enduleni kupita Orumekeke kwenda Oldupai ni maeneo ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka miaka ya 2001 – 2002, tulipata tatizo kubwa sana la Wasomali. Pia naishukuru Serikali kwa sababu ilifanya uamuzi ikawatuma Jeshi la Wananchi wa Tanzania wakashirikiana na ndugu zangu wa jamii ya Wamasai na Wabatemi, kwa kweli wale Wasomali wametokomezwa na hali sasa ni shwari. Jambo hili hatuwezi kusema tumelimaliza kabisa kwa sababu tupo mpakani na hili suala la ulinzi na usalama ni bora likaimarishwa katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mawaziri wafuatao wajiandae watapata nafasi dakika kumi kumi wakati utakapofika; Nishati na Madini, Ujenzi, Mambo ya Nje, Uchukuzi, Mawasiliano na Ofisi ya Rais (Utawala Bora). Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na Mheshimiwa Dunstan Kitandula wajiandae.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Kamati ya Fedha na uchumi.

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo mambo machache ambayo naona kama yakitiliwa mkazo au yakiangaliwa vizuri, yanaweza kutusaidia katika kuinua uchumi wetu. Nianze kwa kusema kuna mambo machache ambayo ni vikwazo katika kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa kodi umekuwa hafifu, Sera za Kifedha zimekuwa hazieleweki, riba kubwa katika mikopo, mfumko wa bei kufikia asilimia 20 na tatizo la uwiano na matumizi ya Serikali. Haya ni mambo ambayo nadhani yakiangaliwa vizuri; kwa mfano, ukusanyaji wa

kodi, unakuta vijana wameingia mitaani wanakwenda kwa mashirika au kwa watu binafsi walio na biashara, kodi inayokusanywa haifiki Serikalini, matokeo yake inapunguza namna gani tunaweza kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wana Benki zimefumka kama ile BLUE inaonesha kama ina msaada wa haraka, lakini unakuta riba yake ni kubwa kiasi kwamba mtu kwa kuwa yuko *desperate*, anakwenda mahali pale anakopa, lakini kuja kulipa anajikuta amepata hasara mara tano. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani hata sera za hizi benki na za kifedha ziangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uwiano wa matumizi ya Serikali, tumekuwa tukiliongelea kwamba matumizi ya Serikali ni makubwa kuliko mapato yanayoingia. Matokeo yake tumejikuta tuna deni kubwa, uwezo wa kuendesha nchi unakuwa mdogo na matokeo yake tupo katika deni.

Mheshimiwa Spika, uwezo mdogo wa kuuza nje; hatuna uwezo mkubwa wa kutosha wa kuingiza fedha za kigeni. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri hayo mambo yakirekebishwa, tunaweza tukainua uchumi wetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa uchumi kunasikika sana kwamba uchumi wetu umekua, lakini ukimwambia Mwanakijiji wa Misenyi kwamba uchumi umekua, atakushangaa sana. Uchumi huu umeshindwa kuongeza ajira, umeshindwa kuinua hali ya uchumi na umeshindwa kuongeza ajira na kuongeza kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nishauri hivi; kwa wakati tulionao, kwa nini tusiamue sasa kuinua uchumi kwa kuanzisha au kusimamia KILIMO KWANZA? Katika kufikiria kwangu, ninaona kama tutasimama na kuongeza nguvu katika KILIMO KWANZA, tuna uwezo wa kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Katika maeneo yangu au sehemu kubwa katika nchi yetu ni Vijijini na hasa katika maeneo ambayo yana uwezo wa kuzalisha lakini watazalishaje kama hawana nyenzo; watazalishaje kama hatujaweka sera za kuwasaidia wakulima? Mimi nishauri hivi; kama tunaweza kuwawezesha wananchi kwa kuwapelekea mbolea kwa wakati, kuwakopesha matrekta na kuweka elimu ya kilimo hasa kupitia Maafisa Ugani, nina uhakika tunaweza tukainua hali yetu ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, tukiamua kuboresha miundombinu kule Vijijini, wananchi watalima mazao, watasafirisha mazao yao kwa bei nafuu na

hatimaye watapata faida. Tayari tutakuwa tumeinua uchumi kwa wananchi wanaokaa Vijijiini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukiweka maji mazuri, maji safi na salama, wananchi wakapata maji safi na salama, tutapunguza magonjwa, tutapunguza hata vifo kwa wananchi wetu, watakuwa na nguvu, hivyo watazalisha na uchumi utaongezeka.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nina neno lingine la kuongeza; uwezesho wa mikopo kwa watu walioko Vijijiini. Wananchi wengi Vijijiini tumewahamasisha kujiunga na VICOBA na SACCOS, lakini wanapojiunga wamejikuta hawawezi kupata msaada.

Mheshimiwa Spika, ninashauri kama tunaweza kuchukua VICOBA tukaviingiza navyo kwenye programme kama SACCOS, wananchi wakakopeshwa, wanaweza kufanya vizuri kuliko hata SACCOS. Mimi kwenye Jimbo langu tuna VICOBA karibu 130, ukizidisha mara 30 ni watu zaidi ya 300; hivyo kama hawa watu watakuwa wamepata mkopo mzuri kutoka Serikalini na tukiwasimamia vizuri, nina uhakika wataweza kufanya biashara vizuri, wataweza kuendeleza maisha yao vizuri, wataweza kupata faida na matokeo yake tutaweza kuwa na sauti kwao na kusikika kwamba tunawajali watu wa hali ya chini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niongelee uwezesho wa kukopeshwa trekta. Sasa hivi katika Jimbo langu tunavyo vikundi zaidi ya kumi ambavyo vinashughulikia kilimo cha miwa, lakini kutokana na ukosefu wa trekta hivi vikundi vimeshindwa kujiendeleza na mashamba yapo wanalipa hela kwa *World Vision*, matokeo yake wameshindwa kulima kwenye msimu na wamepata hasara kwa sababu hawana uwezesho. Ninashauri kama inawezekana, Wizara ya Kilimo ifanye mbinu ya kutukopesha matrekta na hatimaye sisi tunaweza tukawa tunalipa polepole ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu waweze kujisaidia katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la kodi limekuwa tatizo kweli kweli, mimi naomba niseme kama tunaweza kufanya marekebisho *TRA*, yafanyike. Kuna watu wengi, vijana wengi, wafanya kazi wengi, lakini mambo yanayofanyika *TRA* mtu anaajiriwa leo baada ya miezi mitatu ana magari matatu, ana majumba, ana utajiri ambaao haueleweki. Sasa hivi mtoto wako akitangazwa amekwenda *TRA* ni sherehe kuliko hata Ubunge, maana kusema kweli ukimwangalia kijana mwenye miaka mitatu *TRA* ukimlinganisha na Mbunge wa miaka mitano, wanatofautiana. Kwa hiyo, naombe tufanye utaratibu wa kuisimamia *TRA* vizuri kwa kuwa ni kitovu cha uchumi wetu ili tuweze kukusanya kodi na hatimaye tuongeze

uchumi katika nchi yetu. Tukifanya hivyo, tutaweza kukopesha watu, tutaweza kulipa watu vizuri na uchumi wetu utakua.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema kwamba, nawalilia Wanamisenyi, mmewaambia walime miwa, mashamba yamelimwa lakini robo tatu ya yameshindwa kumalizika hatuna vitendea kazi, tupeni vitendea kazi mwone kama Misenyi haitakuwa kama Uholanzi. Ninaamini kabisa kwa kilimo tulichonacho na hali ya hewa nzuri tuliyonayo na bidii waliyonayo wananchi, mkituwezesha kupata vifaa, uchumi wetu utakuwa tofauti na miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, naomba kuwasilisha, lakini naomba kusisitiza suala la uchumi, ukusanyaji wa kodi ni hafifu, Sera za Kifedha riba ni kubwa; hata sisi Wabunge mliotukopesha na CRDB tutakuja kulipa mamilioni na mamilioni, mimi ningejua wala nisingekopa, maana hiyo riba nimekuja kupiga mahesabu nilichukua hiyo pesa kwa kiwewe, nilikuwa nimetoka kwenye kampeni, lakini sasa najuta. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika Ripoti hizi za Kamati.

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi katika Ripoti ya Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupa afya njema na kutuwezesha kukutana asubuhi ya leo. Baada ya kusema hayo, naomba niwarejeshe nyuma kidogo, ukurasa wa 11 wa Ripoti ya Kamati ya Fedha ya Uchumi kwa kipindi cha 2010/11, naomba kunukuu unasema hivi: " Uchumi wetu unakula zaidi badala ya kuzalisha (*net consumer economy nation*), mwelekeo huu ni kikwazo katika jitihada za kuzalisha na kukuza uchumi."

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba pia niwarejeshe kidogo katika miaka mitatu mfululizo jinsi tunavyopata na jinsi tunavyotumia; mwaka 2009/10 mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa triliioni tatu bilioni mia nne tisini na mia tatu milioni, lakini matumizi yakakadiriwa kuwa yatakuwa triliioni sita bilioni mia moja arobaini na tatu, milioni mia tisa na zaidi, mwaka 2010/11 mapato yalikuwa yamekadirwa kuwa bilioni nne millioni mia mbili hamsini na sita lakini matumizi yalikadiriwa kuwa triliioni saba bilioni mia moja sitini na tisa, mwisho wa mwaka tulikuja kugundua kwamba makusanyo ndiyo yaliongezekwa yakafika triliioni tano bilioni mia sita tisini na nane lakini matumizi pia yameonekana

yameongezeka na kufikia trillioni kumi. Kwa mwaka huu wa fedha ilioneshwa kwamba, tutakusanya trillioni sita na matumizi yatakadiriwa kuwa trillioni nane na bilioni kama mia sita. Inavyoonekana, mpaka mwishoni matumizi yanaweza kuwa makubwa kama ilivyojionesha mwaka 2010/11.

Mhehsimiwa Spika, baada ya kuonesha *trend* hiyo, nakubaliana kabisa na Kamati hii ya Fedha na Uchumi ilivyosema kwamba, nchi yetu ni *net consumer economy*.

Mheshimiwa Spika, haya mambo yanaonekana hata tukiangalia Kamati zetu ambazo ni za *oversight*; kwa mfano, mimi nipo Kamati ya PAC, kuna mambo ambayo yanaonesha kabisa matumizi mabaya ambayo kwa makusudi kabisa Serikali inavunja sheria. Kwa mfano, ndiyo maana tunaona umaskini wa Watanzania hauwezi kwisha kwa sababu kidogo tunachokipata hakitumiki sawasawa. Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 imekiukwa makusudi, tena ni mfano mbaya sana ambao umeoneshwa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kutumia vibaya Sheria hiyo na kufanya manunuzi bila kufuata Sheria na kutumia bilioni arobaini na tisa milioni mia nne thelathini na tatu. Hali hii kwa kweli siyo nzuri.

Mhehsimiwa Spika, vile vile kwa Serikali nzima, Sheria ya Manunuzi, kifungu cha 45, kinahitaji kuwepo na mfumo au mpango maalum wa ununuzi, lakini bilioni hamsini na milioni mia sita themanini na tano zimetumika kwa kufanya manunuzi bila ya kuwa na mpango maalum wa mwaka. Hii maana yake ni kwamba, Sheria imekiukwa na humu ndiyo tunapokutana na mambo ambayo hayaeleweki; kwa sababu haiwezekani Sheria inatambulika kwamba inabidi tuwe na mpango maalum wa manunuzi halafu Serikali inakwenda kinyume na hivyo, maana yake ni kwamba humo ndani kuna ubadhirifu wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile inaonekana kabisa Sheria inaendelea kuvunjwa kwa matumizi ya bilioni mia tatu sitini na mbili kutumika na hakuna viambatanisho vyovoyote ambavyo vinaonesha kwamba hizi huduma na mali zimetumiwa kweli kwa kiwango hiki cha bilioni mia tatu sitini na mbili.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC, tumegundua kuna mianya mingi sana ya wizi katika manunuzi ya dharura kama haya ya bilioni hamsini ambayo yanafanywa bila mipango na katika matumizi ambayo hayana nyaraka, haiwezekani huduma zilipiwe halafu nyaraka zisionekane. Vile vile kuna jambo lingine ambalo

linasikitisha kwa kuonesha haya matumizi mabaya ya Serikali na yasiyo ya lazima, tena CAG yeye amesema ni matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni 2010, Serikali Kuu peke yake ..

SPIKA: Sijui *microphone* yako ina tatizo maana inapiga kelele wakati wote; *can you move to another one?*

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mhehsimiwa Spika, Serikali Kuu peke yake imenunua magari ya trillioni tano na bilioni tisini na mbili, kwa kweli nchi yetu ni maskini sana, sisi tuna Deni la Taifa trillioni kumi na nne lakini tunamiliki magari ya trillioni tano! Hii ni aibu, ukiangalia magari yenyé Namba za STK peke yake zinafikia karibu elfu tisa na mia saba, lakini ukiangalia magari hayo moja linauzwa kati ya milioni mia moja mpaka milioni mia mbili. Kwa kweli haiwezekani tuendelee na matumizi ya aina hii, inabidi tuangalie ni jinsi gani tunaweza kupunguza matumizi ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona hatuna aina ya magari kwa aina ya Viongozi; Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Mawaziri, DCs na RCs. Unakuta mtu ananunua gari yoyote, mtu anataka kununua tu VX, V8, inanunuliwa, inabidi tuliangalie hili. Sasa hivi wamehamia kwenye Lexus, tuangalie tunatumia kitu gani na wananchi wetu wana mahitaji gani.

Mheshimiwa Spika, kati ya hayo pia kuna magari kama elfu nne ambayo yanategenezwa kwa pesa za Serikali na yanauzwa kwa bei ndogo kwa watu wa kada za juu na kada za kati, wanauziana milioni nne au milioni mbili mpaka milioni tano; kwa kweli inasikitisha. Siku hizi wakala wa kutengeneza magari TEMESA haifanyi kazi. Maana yake ni kwamba, gereji zinazotengeneza haya magari ya Serikali ni za binafsi na hapo huwezi ku-control bei ambayo inatolewa katika hizo gereji, wanafanya wanavyotaka wao. Hapo kuna mwanya mkubwa sana wa wizi kwa sababu siyo Wakala wa Serikali wanaotengeneza ni watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, tuangalie vile vile matumizi yetu; Viongozi wana tabia ya kutumia magari, yeye anapanda ndege gari inamfuata huko anakokwenda, tuangalie kama kuna umuhimu, inawezekana kabisa Kiongozi anakwenda kufanya kazi kwa siku mbili katika Mkoa; kwa nini asikodishe gari kule kama yeye anakwenda na ndege? Tuangalie sana hayo.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo tuna magari ya trillioni tano, Wizara nyingi hazina majengo; kwa mfano, Wizara ya Afya peke yake inatumia milioni 480 kukodisha jingo. Vile vile tumeshuhudia Wizara ya

Kazi walifukuzwa NHC kwa kutolipa kodi, kwa hiyo, tuangalie vipaumbele vyetu ni vipi.

Mheshimiwa Spika, Polisi wanadai bilioni kumi na saba, mpaka sasa hivi tuna miadi ya bilioni mia mbili hamsini na nne kwa mwaka huu wa fedha, maana yake mpaka mwisho tutakuwa na madeni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la misamaha ya kodi; kwanza, tunaambiwa kwamba wigo wa ukusanyaji wa kodi umekuwa mdogo na kila siku unapokuja hapa ndani ya Bunge katika bajeti, vyanzo vya kodi ni vile vile.

Sasa nitaomba niongelee kipengele kimoja cha *tax exemption*. Ninajua kwa sasa hivi misamaha ya kodi imefikia takriban trilioni 1.04, ni sawa na asilimia 2.9 ya *GDP* ya nchi yetu na ni asilimia 18 ya makusanyo ya mapato yetu yote. Ninajua Sheria ipo, mimi nasema Sheria hiyo ni mbovu, iletwe haraka irekebishwe ili tuweze kupunguza kiwango hiki cha msamaha wa kodi. Waziri anaweza akaja hapa akatuambia Taasisi za Kidini ndizo ambazo zinasamehewa kodi kwa kiwango kikubwa. Taasisi za Dini zinasamehewa kodi kiwango cha bilioni moja na milioni kama mia tano, lakini hii trilioni 1.04 ukitoa bilioni moja na milioni mia tano ina maana kiwango kikubwa sana kinachobaki ni kwa watu binafsi wanaosamehewa kodi, makampuni ya madini wawekezaji na baadhi ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, suala hili inabidi liletwe mara moja, najua kuna juhudzi za *TRA* wamekwenda kujifunza Peru, Serbia na Georgia kuhusu jinsi ya ku-manage au kupunguza misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba suala hilo liangaliwe. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Kamati, Wabunge au Serikali mnawenza kuleta mabadiliko ya Sheria. Kanuni zetu zinasema kama hujui namna ya kuandika Muswada, unaleta hoja kuitaka Serikali ifanye hivyo. Kwa hiyo, tutumie nafasi ya Kanuni zetu. Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Abdallah Mtutura pia atapata nafasi.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika Taarifa hizi za Kamati zilizowasilishwa mbele yetu. Nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi, kwa taarifa nzuri ambazo zinatoa maelekezo mazuri ambayo tukiyazingatia yatatururusu katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, viashiria vya uchumi vya nchi yetu vinatuonesha kwamba, hali yetu siyo nzuri, uchumi wetu ni dhaifu na haujatengemaa. Kwamba, sasa tunashuhudia kiwango cha mfumko wa bei kikiwa kinazidi kupanda siku hadi siku, kutoka asilimia kumi na tatu mwezi Julai mwaka jana hadi asilimia ishirini mwezi wa kumi na mbili, hali bado siyo nzuri. Mauzo yetu ya nje yanakidhi mahitaji yetu kwa asilimia sitini tu, jambo hili siyo zuri.

Mheshimiwa Spika, nasema jambo hili siyo jema kwa sababu wakati uwezo wetu ukiwa mdogo kiasi hiki, bado hatujaweza kuzitumia kikamilifu rasilimali tulizonazo. Nchi hii imejaliwa rasilimali kadha wa kadha lakini hatujaweza kuzitumia ipasavyo. Wenzangu waliotangulia wamezungumzia gesi, wamezungumzia madini, mimi sitakwenda huko nitakwenda kwenye maeneo mengine ambayo tumeyasahau, ambayo yanaweza kukuza uchumi wa nchi yetu na ambayo yanaweza kutuondolea tatizo la ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya *World Economic Forum* ya 2011 inatuambia kwamba, Tanzania ni nchi ya pili Duniani kwa Vivutio vya Utalii. Brazil ndiyo nchi pekee iliyotuzidi kwa vivutio hivi, lakini katika *ku-utilize potential* hii, Tanzania ni nchi ya 110. hili ni jambo la aibu, halikubaliki hata kidogo. Taarifa za hali ya uchumi zinatuonesha kwamba, Sekta ya Uvuvi kwa mwaka jana imekua kwa asilimia moja; hii ni aibu. (*Makofi*)

Taarifa zilizopo zinasema mauzo yote ya samaki duniani hivi sasa asilimia 43 yanatokana na ufugaji wa samaki. Tanzania tumejaliwa vyanzo vya maji vingi; *Lake Victoria*, square 26,000, the second largest freshwater lake in the world; *Lake Nyasa*, square mile 8683, the ninth largest lake in the world; *Lake Tanganyika*, mita za mraba 12,700, the longest and the second deepest in the world. Hii ndiyo pride yetu, kuambiwa kwamba sisi ni wa pili duniani kwa kuwa na vyanzo vya utalii.

Mheshimiwa Spika, wa pili kwa Ziwa Victoria lakini *ku-utilize resources* zilizoko hapo ni kichekesho na inauma kwamba, leo hii nchi kama Malawi inauza samaki nje kuliko Tanzania. Inauma nchi kama Zimbabwe ina mauzo makubwa ya samaki nje ya nchi kuliko Tanzania. Inasikitisha nchi kama Sudani, inauza samaki nje ya nchi kuliko sisi.

Mheshimiwa Rais aliahidi ndani ya Bunge hili kwamba, katika kipindi hiki tutatekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuleta Mradi mkubwa, Programu kubwa ya uvuvi kama tulivyofanya kwenye kilimo.

21 APRIL, 2012

Nimeuliza swali hili, nimepewa majibu mepesi lakini vijana wa Kitanzania hawana ajira. Tungeweza kufuga samaki kwenye maziwa haya, tungeweza kufuga samaki baharini ili kukuza uchumi wa nchi yetu na ili kuondoa tatizo la ajira kwa vijana wetu lakini nini tunachofanya, majibu mepesi. Lipo kwenye mpango wa miaka mitano, tupo kwenye mchakato, utekelezaji wa llani ni wa miaka mitano, haya ndiyo majibu lakini Watanzania wana hali ngumu. Nawasihi tutumie *potential* tuliyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali imeanza kuona umuhimu wa kuwa na *drip irrigation* lakini nasikitika tunakusudia kuanza na Wilaya 23 tu kwa nini tusiwe *ambitious* tukasema *program* ya namna hii iende kwenye kila Wilaya ya nchi yetu? Kwa nini tusiwe *ambitious* tukasema yale mabilioni ya JK tuyaelekeze kwenye ujenzi wa miundombinu hii ya *drip irrigation*? Kwa nini tusijielekeze kupeleka programu hii kwenye kila Wilaya tuhakikishe vijana 200 wanaajiriwa katika *scheme* za namna hii? Kwa nini tusijielekeze kusema kwamba mradi huu tunauweka mahsus kwa ajili ya kuzalisha alizeti na mazao ya mafuta? Maana takwimu zinatuambia uzalishaji wetu wa mbegu za mafuta hautoshelezi. Hili tatizo liko kwa nchi zote za Afrika Mashariki, hakuna nchi inayojitosheleza kwa mazao ya mbegu za kuzalisha mafuta. Kwa nini sisi tusichukue jambo hili tukasema tunajielekeza huko tunataka tuzalishé mbegu hizi ili kutosheleza uzalishaji katika ukanda huu wa Afrika Mashariki? Tuache kulalamika, tutumie *potential* tulizonazo kukuza uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kidogo.

Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na Wabunge wenzangu kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote tatu zilizotoa taarifa hapa Bungeni jana.

Mheshimiwa Spika, taarifa zao ni nzuri na zinajitosheleza lakini kama ada, inabidi nitoe mchango wangu kama wenzangu walivyofanya.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wamekuwa wakisikia kwamba uchumi unakua lakini bado wameendelea kuwa na maisha duni kitu ambacho kinaendelea kuwakatisha tamaa. Pamoja na kwamba uchumi unakua bado mgawanyo wa kile kipato kinachopatikana haugawanywi sawasawa katika Mikoa mingine iliyobaki nyuma na ile ambayo tayari ilishatangulia. Sisemi kwamba Kigoma hatujanufaika, tumenufaika, naomba kupitia Bunge lako nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Awamu ya

Nne kwa kuukumbuka Mkao wa Kigoma. Ametufungulia Mkao wetu, naamini ataendelea kumalizia kazi ambazo zimebakia. Naomba niseme kwa vile tumekuwa tukisikia kwamba uchumi unakua na bado kuna mambo mengine ambayo bado hayatufurahishi, tunaomba basi wahuksika wajielekeze kwenye maeneo yale ambayo bado yana matatizo makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, reli ni kilio kikubwa sana kwa Watanzania hasa wa Ukanda wa Kati. Reli ni kichocheo kikubwa cha uchumi lakini tumeisahau. Mimi ninakuwa na wasiwasi, inawezekana kabisa kuna watu ambao wanafanya makusudi kukwamisha reli ya kati isiweze kufanya kazi. Inawezekana kabisa na ndivyo ninavyoamini. Inawezekana kati ya watu ambao wana malori ya kusafirisha mizigo ya kwenda nchi za nje, watu hawa ambao wako huko na wenyewe wanahuksika kwa sababu kama wangkuwa hawahuksiki, wangkuwa hawapati maslahi wangehakikisha kwamba reli hii inatengenezwa lakini kwa sababu inawezekana kuna kitu ambacho kimejificha huko ndani maana wengine hawaoni umuhimu wa reli hii.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kwa sababu wananchi wengi ni maskini, wanatumia usafiri wa reli, wanasaferisha mizigo kupitia reli na mizigo ikisafiri kupitia reli wananchi wanunuifaika kutokana na bei kushuka, tofauti na ilivyo kwa sasa hivi mizigo inasafirishwa na malori, bei zinakwenda juu. Kwa kweli naomba Serikali iweze kuangalia kilio cha wananchi walio wengi kwa vile ni cha muda mrefu kwa kujenga reli hii.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, haya maneno yanayosemwa kwamba uchumi umekua bado huko Wilayani sisi wenyewe Wabunge kila siku tunashuhudia Wabunge wakilia kwamba fedha haziendi Wilayani. Sasa kama uchumi unakua ni kwa nini fedha zisifike Wilayani zikaenda vijiji vile ambavyo bado vina matatizo ya miundombinu ya barabara ikajengwa, maji yakapatikana, wananchi wakaendelea kunufaika hasa wanawake ambao wanapata shida sana katika utafutaji wa maji? Kwa hiyo, kama uchumi unakua basi kile kipato kinachopatikana kielekezwe vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kilio changu kingine ni kuhusu barabara ya Kigoma – Nyakanazi. Barabara ile tangu Bunge la 2005 – 2010, mimi nilikuwa Mbunge, nakumbuka Mheshimiwa Shukuru Kawambwa akiwa Waziri aliwahi kusema kwamba zimetengwa fedha za kujenga barabara ya Kigoma mpaka Kasulu, bajeti ile barabara haikutengewa fedha na Bunge la mwaka 2011/2012 tulitenga shilingi billioni mbili kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kigoma – Nyakanazi. Mpaka sasa hivi hakuna dalili.

Mheshimiwa Spika, naomba fedha zikipatikana basi ahadi zile zilizoahidiwa zitekelezwe. Sisi tuko mpakani, barabara zile ni za muhimu sana, ningeomba barabara zile ambazo ziko mpakani ziweze kutengenezwa mapema, zijengwe haraka iwezekanavyo kwa sababu lolote likitokea watu watakimbia kupitia njia gani? Hata kwa usalama wa nchi yetu vilevile barabara za mipakani ni muhimu. Kwa hiyo, naomba fedha zikipatikana, barabara ile ambayo ni kilio kikubwa cha wananchi wa Kigoma, zielekezwe kule ili kile kipande kilichobakia kiweze kumalizika. Maana kutoka Kigoma mpaka Kidahwe ndio tumeishia. Kwa hiyo, naomba kwa sababu kwanza Mkoa wa Kigoma tumeingizwa kwenye Mikoa sita (6) ya kuzalisha chakula, barabara ni muhimu sana. Ile barabara ndiyo inayounganisha Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma za Kibondo, Kasulu mpaka Kakonko. Mbolea inasafirishwa kwenda mashambani kupitia kwenye barabara ile. Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba umesema tusijielekeze kwenye Mikoa yetu, mimi naomba niseme kwamba barabara hiyo ni ya muhimu iangaliwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, kwetu tumeprata tatizo kama ulivyosikia, Ndege ya Air Tanzania ilipata matatizo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu wananchi walinusurika, ninaomba ufanywe mpango wa makusudi ili kiwanja cha Kigoma kiweze kujengwa haraka iwezekanavyo tuweze kupata ndege za kwenda kutua Kigoma. Kwa sababu baada ya ndege ya ATC kuharibika, mimi nina imani tumbaki na matatizo makubwa ya usafiri. Kwa hiyo, kama kiwanja kitajengwa haraka, nina imani hata ndege nyingine zitatua katika Mkoa wa Kigoma na wananchi wataendelea kupata usafiri. Kwa sababu kama unavyojua reli ndiyo ulikuwa usafiri wetu mkubwa lakini sasa treni yenyewe mara moja kwa wiki ndio inasafiri, barabara hazieleweki, mtu akisafiri kutoka Kigoma kuelekea Dar es Saalam anachukua siku tatu, mvua zikinyesha, magari unakuta yamepangana. Kwa hiyo, tunaomba kupitia Bunge lako Tukufu watu wanaohusika na miundombinu ya ujenzi wa viwanja vya ndege waweze kuangalia Mkoa wa Kigoma kwa huruma ili na sisi tuweze kunufaika kwa kupitia pato hilo la Taifa.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Watanzania walio wengi wameelekeza kwenye kilimo. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba fedha zikipatikana kama ni mbolea inunuliwe mapema ielekezwe huko inakokwenda kusudi wananchi waweze kupata mbolea wakati muafaka. Maana wanasema mvua za kwanza ni za kupandia, sasa mbolea zinafika zimechelewa huo uchumi tutaukuzaje kama mbolea zinafika wakati watu wameshapanda bila mbolea?

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo, nilikuwa ninaomba kile kinachopatikana kiweze kugawanywa sawasawa. Ahsante. (*Makofii*)

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii leo. Mimi pia niko pamoja na wenzangu kuzipongeza Kamati kwa jinsi walivyotoa taarifa zao. Ninasema kwamba naungana nao kwa taarifa zao walizozitoa.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo najikita mimi ni eneo la ukuaji wa pato la taifa. Ukuaji wa uchumi bado haujasaidia kuondoa umaskini wa nchi yetu. Nazungumza hivyo kwa kuwa kwenye sekta zinazochangia zaidi ni sekta chache, lakini sekta ambayo ina watu wengi kama vile kilimo inahusisha wananchi takribani milioni 32 ambapo ni asilimia 73.7 wanaishi vijijini wanachangia asilimia nne tu ya pato la taifa. Haya ni masikitiko makubwa kwa maana kwamba watu wengi ndio ambao hawachangii pato la taifa lakini sababu zipo na hizi sababu zinafumbiwa macho.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kuelezea suala la kilimo, Serikali haijielekezi kuweza kuwasaidia wakulima wengi ambao wako vijijini kuweza kupata ardhi ili kila mtu walau angeweza kulima kiwango cha ekari mbili/tatu, nina uhakika hawa watu milioni 32 wangeweza kupandisha pato hili la taifa. Lakini kwa kuwa hawalioni hilo ndio maana pato letu linashuka kwa hiyo, wengi wao hawachangii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee suala la masoko, kama hakuna soko ni wazi kabisa kwamba haya mazao hayana maana yoyote. Sasa hatuna budi Serikali hii iweze kuwatafutia soko wakulima wote wadogowadogo. Serikali inaangalia zaidi na kupeleka jicho lake kwa wawekezaji tu. Wawekezaji ni wachache ndio ambao wanaochukua eka 100,000 na kuendelea lakini hawa wawekezaji wadogowadogo ambao ni wakulima wadogowadogo huwa Serikali haiwatilii maanani. Kwa sababu hata pungozo la bei ya vitu vingine vyenye *tax* wanapewa wale wawekezaji wakubwa lakini hawa wadogowadogo ushuru ni kama uititiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu upatikanaji wa huduma mbalimbali vijijini. Endapo kutakuwa na barabara nzuri, barabara zitajengwa, ni wazi kabisa kwamba wananchi hawa wana uhakika wa kuuza mazao yao kwa urahisi na kupeleka mahali ambapo bei inapatikana lakini barabara pia hazipo.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ninalopenda kulizungumzia ni suala la upatikanaji wa maji. Endapo kutakuwa na maji ya kutosha, Serikali itaelekeza fedha nydingi kwa ajili ya maji vijijini, wananchi wengi watamwagilia mashamba, hakuna haja ya kusema sasa hivi ni ukame, wananchi wengi wanaweza kuvuna mara tatu kwa mwaka na pato likapanda juu zaidi na uchumi wetu ukawa mzuri. Endapo maji yatakuwa hayapo na hatutaelekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji, hakuna kitu tunachokifanya kabisa. Napenda Serikali sasa ilione hilo kwamba inabidi kuelekeza nguvu kwenye vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni huduma ya fedha. Huduma ya fedha inaleta masikitiko makubwa sana kwa Serikali yetu. Imeelekeza fedha za dirisha la kilimo *TIB (Tanzania Investment Bank)* ambayo iko Dar es Salaam, tawi lingine liko Arusha, hawa wakulima wadogowadogo walioko vijijini watapata lini fedha hizo na zitawafikiaje? Wanaokopa ni watu wenye uwezo tu lakini wale ambao hawana uwezo hawapati kitu chochote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nina mfano mzuri kabisa kwa sababu SACCOS ambazo zipo kwetu zilijaribu kukopa, ilibidi tuingie gharama kubwa kwa ajili ya usafiri kutoka kijijini kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya kusainiwa tu. Tuangalie hilo kwamba ni gumu sana. Tunapenda kwamba hii Benki ya Kilimo iharakishwe haraka iwezekanavyo kufika vijijini isibaki Dar es Salaam, wakulima wako vijijini, tuekeleze nguvu huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeshauri fedha za kilimo ziende kwenye *NMB Bank* na waelekezwe kuwakopesha wakulima wadogowadogo kwa sababu *NMB* imetapakaa vijijini kote au Wilayani kote, ni rahisi kwa mkulima kufika pale kuliko *Tanzania Investment Bank* peke yake. Hii *TADB* ya kwetu ambayo tunasema ya kilimo inaanzishwa, basi wakati huo ukifika na wakulima wetu uchumi wao umeshapanda kwa sababu haitakuwa rahisi kufunguliwa mapema iwezekanavyo, lakini pamoja na hivyo ni vizuri yafunguliwe basi hayo matawi yawe vijijini na siyo mjini inavyoelekezwa kwa sababu uchumi uko huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni upatikanaji wa pembejeo, pembejeo imekuwa hadithi kwa Serikali yetu. Ninaomba hili niliekeleze kwa Waziri wa Kilimo, pembejeo imekuwa ni miradi ya watu wachache, haiwafikii wakulima hata kidogo. Mpaka leo pembejeo wengine hawajapata na masika ndio hivyo inaisha. Je, hawaoni sasa tuachane na haya masuala ya pembejeo tutafute namna nyingine wakulima wapate pembejeo kwa wingi ili wengi wao waweze kulima vizuri? (*Makofii*)

21 APRIL, 2012

Mheshimiwa Spika, kitu kingine viwanda vinahitajika, suala la ubinafsishaji limeleta athari kwa wakulima wengi nchini. Viwanda vilivyobinafsishwa vyote ni vya kilimo, viwanda vilivyobinafsishwa ni vya nyama na havileti tija kwa wananchi wetu wa Tanzania na wala havileti tija kwa Tanzania nzima kwa ajili ya uchumi wetu kwa sababu haviendelezwi hata kidogo. Mimi nadhani sasa ubinafsishaji ufe turudi kwa wananchi wenyewe na Serikali ichukue viwanda vyake ili tuwaboreshée wananchi waweze kupeleka mazao kwa ajili ya usindikaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni umeme. Kwanza kabisa umeme unapatikana vijijini, hakuna umeme unaopatikana mjini, maji yako vijijini. Sasa kama umeme unapatikana vijijini, basi umeme uanzie vijijini uelekee mjini ili wale wananchi waweze kumwagilia kwa kutumia pampu, waweze kuleta maendeleo yao na waweze kufungua viwanda vidogovidogo vya kusindika kila kitu huko vijijini, halafu ndi watu wa mjini waweze kupata mazao yaliyosindikwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni ajira. Ajira imekosekana kwa vijana wetu, vijana wetu wamekuwa manamba kwenye mashamba ya wakulima wakubwa. Sasa napendekeza na mimi kwamba mashamba hayo makubwa yapunguzwe, vijana wetu wapate heka mbilimbili kutoka kwenye hayo mashamba ili wasiwe manamba nao waweze kuzalisha pato la nchi hii kama inavyotakiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ningependa kuzungumzia...

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naona muda wangu umeisha, nashukuru. (*Makof!*)

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii leo asubuhi, Mungu akubariki.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali, nataka niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati kwa kuwasilisha vizuri hoja zao ambazo ni za msingi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kusikitika, haswa nipo kwenye nishati na madini. Tunapozungumzia nishati na madini, umeme unatoka katika Mkoa wa Tanga haswa Hale kwenye Jimbo la Korogwe Vijijini na bahati mbaya zaidi au nzuri ni kwamba mimi kwenye Jimbo langu, nina vituo viwili vya nguvu ya umeme. Kinachonisikitisha, kule Mkoa wa Kilimanjaro kuna Bwawa la Nyumba ya Mungu, kunatoka

nguvu nzuri ya umeme, lakini Bwawa lile la Nyumba ya Mungu karibu vijiji vyote vinavyozunguka eneo la Bwawa lile vina umeme.

Mheshimiwa Spika, Kihansi, Kidatu, Mtera, Mabwawa haya huwa mara nyangi sana yanakauka. Nataka niulize Serikali ni lini Mto Pangani umeshawahi kukauka maji? Ninasema hivi kwa sababu katika siku zote ikifika mahali wanasema Kidatu imekauka maji, lakini cha kushangaza Mto Pangani haujakauka maji hata siku moja, watu wanatumia magenerator, wanatumia nguvu kubwa kwa kununua mafuta, kwa nini wasiendeleze Mto Pangani kwenye vile vituo viwili vya kuleta nguvu za umeme? Wangekuwa wanarekebisha ile mitambo iliyoko pale Hale na Chemka kusingekuwa na matatizo ya namna hii. Leo hii tunashangaa sana kusikia kwamba umeme unakatika lakini kama kweli umeme unakatika ungeanzia TANESCO. Inasikitisha sana, unaweza kufika Mkoa wa Tanga mzima umekatika umeme lakini TANESCO hakukatiki umeme, wao hawajui uchungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka kuisaidia nchi hii, basi umeme unapokuwa umekatika iwe ni dhoruba ya watu wote. Mimi siku moja nimekwenda kwenye ofisi ya umeme, umeme mji mzima umekatika, wafanyabiashara wameharibikiwa, lakini unakuta kwao umeme upo, unajiuliza huu umeme kwao umepatikana wapi na huku leo tumetangaziwa kwamba umeme umekatika? Kitu hiki kinanisikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, la kushangaza vilevile ni kwamba mimi katika Jimbo langu la Uchangazi na Mkoa wa Tanga, nimesahaulika sana. Kuna vituo vikubwa vya nguvu ya umeme, lakini Jimbo langu halina umeme. Nina Kata hapa ambazo ninaomba nizitaje kwa sababu zinanitia uchungu kiasi ambacho hata ikifika hiyo siku ya bajeti mimi nitakuwa mtu wa kwanza kukataa hiyo bajeti ya Nishati na Madini na ninasema kabisa kwamba nitaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono. Wakati wa bajeti mwaka jana tulivyokuwa tumekuja hapa, mimi nilikuwa napigiwa simu mpaka saa sita za usiku yaani ni vijiji gani havina umeme? Mimi nikawa navitaja lakini mpaka leo hii hawajakanyaga kwenye Jimbo langu kwenda kuangalia hivyo vijiji vikoje. Sasa leo hii nitakwenda kuunga bajeti ya nani?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano huko kunakotoka nguvu za umeme katika Kata ya Mnyuzi, Mzindawa, Magunga, Gelaza, hakuna umeme. Kwenye Kata ya Magoma kuna Kerenge Kibaoni, Lusanga, Matalawanda, Mbuyuni hakuna umeme. Kwenye Kata ya Kizala ndiyo wamesahaulika kabisa na ndiyo kunakotoka mazao mengi ya chakula hapa Tanzania. Haya, unakwenda Kata ya Vugili, Vugili yenyewe ambapo ndiyo shule ya kwanza ya Kitanzania, mimi ndiyo nilikuwepo

pale, mpaka leo hii umeme umefika kwenye Airtel, kwenye Kata hakuna. Unakwenda Bindila, Makao Makuu ambapo hata kuonyeshwa kwenye bajeti, niliangalia nikaonyeshwa Kata ya Bindila, Mwifingo na Mugwashi, Mali na Mbwale kutakuwa na umeme, hakuna. Leo hii, hata ukimpigia simu yule aliyekuwa ananipigia simu siku za mwanzo kwamba je katika Jimbo lako kuna sehemu gani hakuna umeme? Hata kupokea simu hapokei, naunga mkono wa nini bajeti hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni faida ya nani? Leo hii mimi nakwenda kuhukumiwa kwenye Jimbo langu wenzetu wanakula starehe, ndiyo haya mjambe mmoja amekaa hapa na kuzungumza kwamba kuna watu wanatembea na magari ya kifahari, magari ya kifahari yanasaadid nini kama kwenye Majimbo hakuna umeme? Tungeiga Kenya, watu wote wana magari madogo, gharama imepungua na mambo yanaendelea na uchumi unazidi kupanda, leo hii watu wa Kenya mimi nimepita juzi Holoholo wananchi wa Kenya wanalalamika kwamba mbona sisi tunawanyima umeme? Kule Namanga umeme haukatiki mara kwa mara angalia *computer* zimekufa, basi kama kunakatika umeme mtuambie leo umeme utakatika ili na sisi *computer* zetu tuzime, hapa tuna vitu vyenye thamani tumepata hasara, je, hii ni haki ninyi Watanzania mpaka mimi nikashika mdomo, nikauliza heee, kama ninyi pia mnapata matatizo ya namna hiyo basi na sisi ni makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, sikupenda niyaseme hayo lakini ni uchungu niliokuwa nao, natamani kulia ndani ya Bunge hili. Nilie?

WABUNGE FULANI: Lia!

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Sitaki kumpa majonzi Mheshimiwa Spika naomba niendelee. Hiyo ni upande wa Kata ya Bugiri, nakwenda Kata ya Mombo hakuna umeme, unakwenda Kasiga, Mazinde, Nguha hakuna umeme, unakwenda Kata ya Nkalamo hakuna umeme, lakini eti katika maelezo hapo unaambiwa nguvu kubwa ya umeme inatoka Pangani hasa kwenye Mto Pangani. Hii imeniuma sana, nataka nirudie kusema kwamba kama kweli TANESCO wanafanya haki, basi haki hii ianzie kwenye Jimbo langu, haki hii ianzie Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Kilimanjaro hakuna hata siku moja unaona mahali pamekosekana *bulb*, hakuna hata siku moja unaona kuna mahali pamekosekana taa na ni kituo kimoja tu cha nguvu ya umeme. Inakuaje Tanga, Mkoa ambao una vituo viwili vyta nguvu za umeme, umeme unakatika kila siku hasa katika Wilaya ya Muheza? Hii ni kitu cha kusikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, tunakuja hapa kila siku, tunapiga makelele, tukifika kule wenzetu wanatuhukumu nyie kazi yenu ni makelele tu kitu gani kinafanyika? Kwa maisha haya, hatutafika mbali.

Mheshimiwa Spika, nataka niendelee kwenye upande wa madini. Mimi kwangu kuna machimbo ya madini mengi tu, lakini naomba haya madini yaangaliwe, mikataba yao inakuwaje haswa kule Kalalani. Kuna watu wanapata shida, wanavamiwa sana, lakini cha kushangaza ni kwamba ikifika wakati wa kutoa yale maeneo kwa wawekezaji, wanakuja kupewa watu ambao hawajui thamani ya madini na matokeo yake ni kunyanyasa wananchi. Naomba hii Serikali iangalie sana, si utendaji wa haki kwa binadamu wa aina yeyote. Mtu anayeangaliwa ni yule ambaye ameanza lakini wale watu ambao wanahangaika inafika mahali hawasaidiwi msaada wa aina yeyote, tuwaangalie sana.

Mheshimiwa Spika, nataka niende kwenye ulinzi na usalama. Inasikitisha sana kwamba wanapofariki binadamu wa aina yeyote, Tume za Serikali zinaundwa kwa nini Polisi wanapofariki au wanapovamiwa hamuwaundii Tume? Kwani wao sio binadamu? Naomba Serikali hii inipe majibu mazuri sana, Kamati ya Ulinzi na Usalama imeeleza vizuri sana, lakini naomba niseme na Polisi pia ni binadamu kama binadamu wengine. Wanapopata matatizo na wao wanapokuwa wanapambana kwa ajili ya kutetea maslahi haswa wanapopambana na wezi wanakuwa hawaundiwi Tume kwani wao sio binadamu? Naomba hili tuliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja za Kamati zote za Bunge. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kidogo nitoe mchango wangu kuhusu namna tulivyo na tunaelekea wapi. Nishati ya umeme ni kitu muhimu sana katika uhai wa nchi yoyote. Kwa bahati mbaya tu, Tanzania leo tunasheherekeea miaka 50 ya uhuru, tuna asilimia 12 tu ya umeme unaotumika nchi nzima. Kama tungekuwa makini, tungefanya jitihada ya kupatikana umeme wa kutosha walau *megawatts* 2000 au 2500, kwa nini nikasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, tuna migodi mikubwa, migodi ambayo inahitaji umeme wa kutosha, leo matokeo yake migodi hii inatumia umeme kutohaka na *generators* na anapata *exemption* ya mafuta, kwa upande mwingine ni hasara. Sisi tunawaruhusu kuingiza mafuta, hatujui yanahakikiwa vipi kama ni kweli yote yanakwenda kwenye migodi au mingine yanaingia katika biashara. Huwezi kuwa na viwanda au ukainua

kilimo bila kutegemea mazao unayoyatengeneza katika nchi yako na viwanda ambavyo havina umeme. Hata hospitali na elimu ni sekta zinazohitaji umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo mimi nasema, umeme ni kitu muhimu sana ni utii wa mgongo wa nchi yoyote duniani. Sisi *Alhamdullilah* Tanzania tuna utajiri mkubwa sana, ukija kwenye madini, tuna dhahabu sisi, tuna almasi, tuna tanzanite, *uranium*, makaa ya mawe na kesho gesi hiyo hapo tayari. Kwa mtazamo wangu, kama tungekuwa makini toka miaka kumi ya nyuma tusingeshughulika na madini, yangekaa chini ya ardhi mpaka wakati muafaka ama baada ya miaka arobaini au hamsini mbele. Kwa nini nikasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebarikiwa na Mungu kwamba ina ardhi ya kutosha ya kuwa na kilimo bora na cha kisasa. Tuna bahari ambayo inapoteza samaki wengi bila ya kuvuliwa mwaka hadi mwaka. Tuna mifugo, ni nchi ya tatu katika Bara la Afrika. Tuna utalii, ulikwishazungumzwa hapa kwamba tuna *parks* ambazo hakuna pahala popote duniani. Tuna bandari na reli ambazo kama tungevitumia vitu hivi sita tukawaachia dhahabu, almasi, tanzanite, *uranium*, gesi, mkaa wa mawe, tukajielekeza kwenye kilimo cha kisasa, uvuvi bora, mifugo ikafugwa kisasa, tukainua kiwango cha utalii, bandari yetu na reli mbili ya kati na ya kusini basi Tanzania isingehitaji kuchimba hata kilo moja ya dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini wapi, Angola baada ya miezi miwili inayokuja wanafungua reli yao ambayo itatoka Lobito hadi DRC na Zambia. Zambia watahiari wasafirishe mizigo yao kupitia Angola kwa kutumia Bandari ya Angola iliyoko Atlantic Ocean sisi *TAZARA* hatujafanya chochote hadi leo kitu ambacho tumepewa kama ni tunuku na ndugu zetu wa Kichina baina ya nchi hizi mbili za Tanzania na Zambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tena wale South Africa wameanzisha chombo chao kingine ambacho kinaitwa *South African Custom Union (SACU)* inaunganisha South Africa, Angola, Botswana na nchi zingine, sisi tumelala. Ukija kwenye Shirika letu la Ndege, ndiyo ndege ilishapiga mwereka Kigoma ile ya mwisho, *finish*, hakuna ndege. Kuna ndege gani? Ilikuwa ni March 28th, 2012. Madege yako Ulaya yanatengenezwa sijui yamekuwa *grounded*, wakati *KQ* sasa hivi wana mipango kabambe ya miaka minne inayokuja, wana ndege 34 wanataka *wazi-double* ziwe 68 na kuongeza *route* kwa Bara la Afrika na Asia na ndiyo haohao walioingia *joint venture* na *Precision Air* na ndiyo haohao waliongia *joint venture* na

21 APRIL, 2012

KLM. Sisi ndege yetu moja kwa bahati mbaya masikini imekwenda kwenye uterezi, imejigonga pua chini, sasa hatuna ndege tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwa upande wa Mabalozi. Mabalozi sasa hivi wa dunia nzima wanatumika kiuchumi, Mabalozi wetu wa Tanzania lazima wapewe hii elimu kwamba popote walipo watumike kiuchumi. Zaidi kwenye utalii, kwenye *investiment*, tunapata *investors* na kwa hali kama hii tunayokwenda nayo ikawa wananchi hawana imani na sisi na leo dunia ya utandawazi kila mmoja anapata taarifa za nchi yetu hata ile *Diaspora* ambayo tukiitegemea kwamba watu watakuja kuwekeza, watu wataleta fedha zao Tanzania walioko nje ya nchi hawatafanya hivyo kwa kuogopa kinachoendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema hivi, kwamba sasa Bunge liwe na maamuzi ya kutunga ama kutengeneza Kamati ya kufuatilia maamuzi ya Bunge. Siku zote tunapiga kelele tu hapa, lakini maamuzi ya Bunge hatuyaafuatillii wala hatupewi ripoti zozote na hizi Wizara zote zifuatilie vilevile maamuzi ya Wabunge. Kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi, sisi ndiyo wenye kujua matatizo ya wananchi wetu, Mawaziri ambao tunao wamebakia kuwa ni ma-Vasco Da Gama kazi yao kusafiri tu kutoka Tokyo - London, London - Washington, Washington - Nicaragua, Nicaragua sijui wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri aliyewekwa hapa kwa ajili ya kusafiri nchini hizo ni Waziri mmoja tu, ni Waziri Membe. Mwaka jana au juzi mimi nakumbuka, Rais Kikwete alikuwa Washington, Mawaziri saba waliondoka kila kona ya dunia wakimfukuzia Kikwete, kuna nini huko Amerika? Mheshimiwa Kikwete amekwenda na ziara yake, amewaaamini atakaofanya nao kazi na kaondoka nao, kama atamhitaji Membe atamchukua Mheshimiwa Membe, lakini Waziri mmoja alikuwa Johannesburg karuka mpaka Washington, mmoja Tokyo mpaka Washington, mmoja Delhi mpaka Washington ukimuuiliza umerudi na nini? Hakuna zaidi ya perfume zawadi ya mama watoto na saa ya mkononi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yes, we are not serious. We are not serious. Kama Wabunge tunatakiwa sisi tuonyeshe imani safi kwa wananchi wetu, leo tunaenda kujenga...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

TAARIFA

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Taarifa!

21 APRIL, 2012

SPIKA: Mheshimiwa Selasini taarifa!

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu ya Kanuni 68(8) lakini pia ninataka ni-refer Kanuni ya 64(a), ninaomba kumpa taarifa msemaji aliyetangulia kabla ya huyu aliyekaa na ningependa nisome Kanuni hii inasema bila ya kuathiri masharti ya lbara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Spika, msemaji aliyetangulia kabla ya huyu aliyekaa amesema hapa Bungeni kwamba katika Mkoa wa Kilimajaro, hakuna eneo hata moja ambalo haliwaki *bulb* kwa maana kwamba maeneo yote ya Mkoa wa Kilimanjaro yana umeme.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi sio sahihi na binafsi jana niliwasiliana na Naibu Waziri wa Nishati na Madini nikimkabidhi malalamiko ya Vijiji 10 katika Jimbo la Rombo ambavyo havina nishati ya umeme. Vilevile natambua katika Majimbo ya Mwanga, Same Mashariki, Same Magharibi, Majimbo ya Siha, Majimbo ya Hai na kwa ujumla maeneo yote ya Mkoa wa Kilimanjaro wananchi wa Mkoa ule wana matatizo ya umeme sawasawa na wananchi wa maeneo mengi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha.

MBUNGE FULANI: Taarifa!

SPIKA: Aaah! Tunakwenda kwa utaratibu sio kila mtu taarifa, inayoruhusiwa ni hii moja niliyosikia.

Siku moja kulikuwa na Mzee mmoja maarufu kabisa akawa anahutubia mukutano wa hadhara, akasema mimi bwana nimetembea nchi na nchi na nchi. Akaulizwa wapi? Akasema nimetembea kijiji kimoja pale Songea na kingine lakini akasema nchi na nchi. Kwa hiyo, ndiyo hivyo hivyo. (*Kicheko*)

Tunaendelea Mheshimiwa Zitto Kabwe!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia leo na nitapenda nijikite katika taarifa chache sana kwa sababu ya muda. Nitajikita taarifa ya Kamati ya Fedha, Kamati ya Nishati nkipata muda kidogo nitazungumzia Kamati ya Miundombinu na maoni machache ya Kamati ya Nje lakini zaidi Kamati ya Fedha na Kamati ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikupongeze kwa kazi ambayo Bunge imelifanya kwa siku chache zilizopita. Taarifa na mabadiliko ambayo yanafanyika ambayo yanaimarisha uwajibikaji ni mambo ambayo yanajenga heshima ya Bunge lako. Kwa hiyo, napenda nikupongeze sana. Napenda kuwaomba Wabunge waendelee kuisimamia kwa dhati Serikali ili iweze kuwajibika kwa Wabunge kama Wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha kwa ujumla imezungumzia tatizo kubwa tulilonalo katika uchumi wetu, na ninenependa ninukuu maneno ambayo yameandikwa katika ukurasa wa nne wa taarifa ya Kamati ya Fedha kwamba Kamati imebaini kuwa lipo vile vile tatizo kubwa la usimamizi na uendeshaji hafifu wa uchumi (*economic mismanagement*) na kwa kiasi kikubwa Kamati ya Fedha imejikita sana katika kuelekea kutoa mapendekezo ambayo yatatusaidia kuondokana na hali hii ya uchumi ambayo tunayo, kwa kuwa na uchumi amba unakua kwa kasi lakini hauzalishi ajira, uchumi amba unakua kwa kasi lakini hauondoi umaskini. Nashukuru kwamba Kamati imekiri kilio ambacho tumekuwa tukikizungumza mara kwa mara kwamba njia pekee ya kuweza kufanya uchumi wetu uweze kukua zaidi na ukuaji huo wa uchumi kuwa na maana kwa wananchi ni kukuza uchumi wa vijiji na Kamati imependekeza mambo ya msingi sana katika ukuzaji wa uchumi wa vijiji katika Sekta ya Kilimo, Miundombinu, Umeme, Maji na huduma za kijamii.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii ya Kamati nyingine zote ziwe ni sehemu ya hotuba za utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge ambapo Wizara zitakapokuja kwenye Bajeti ziweze kutolea taarifa za utekelezaji wa mapendekezo ambayo Kamati imetoa. Kwa kweli utaratibu huu amba tumeuanza wa Bunge la mwezi wa Nne kutoa taarifa za Kamati unasaidia sana kutoa taarifa na kusaidia maandalizi ya bajeti. Naamini kwamba Mawaziri wote wataweza kutuletea *metrics* inayoonyesha mapendekezo ambayo Kamati zimetoa na namna ambayo Serikali inatekeleza mapendekezo hayo.

Nilikuwa napenda kusisitiza sana kwamba iwapo tutakuza uchumi wa vijiji, iwapo tukirudi kwenye sera ya maendeleo vijiji kwa maana siyo *villagelization* ya kutengeneza vijiji vingine, *vigelization* ya kuwapa watu kule vijiji na kuweza kuwasaidia, kuweka miundombinu vizuri ili kuweza kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yetu unakua. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba taarifa hii ya Kamati ya Fedha ambayo wameiwasilisha hapa iweze kutekeleza kwa namna ambavyo imeinishwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la mapato ya ndani na Kamati imezungumzia kwa kina sana jambo hili. Nilikuwa nasoma taarifa ya wataalam ambayo imetolewa hivi karibuni sana ya mwezi Machi mwaka huu 2012, ambayo imeandikwa na Mwandishi David Bevan kutoka *University of Oxford, Department of Economics*, anazungumzia tatizo kubwa ambalo tunalo la namna ya kuimarisha mapato ya ndani na ameonyesha jinsi ambavyo bajeti yetu ya mwaka jana ilivyokuwa over optimistic na tukajikuta kwamba inabidi tuondoe baadhi ya matumizi ya hivi ninavyozungumza. Miradi mingi ya umeme vijiji kama siyo yote imeondolewa kwa sababu Serikali haina fedha. Kuna ambayo ni lazima sasa tuweze kujikita.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha hapa Sheria mpya ya Madini na kila wakati tunaiambia Serikali kwamba Makampuni ya Madini yahamie kwenye sheria mpya ili Sheria mpya ya madini iweze kutekelezwa. Mpaka sasa hakuna kampuni hata moja ya madini ambayo imehamia kwenye sheria mpya ya madini na hii inakoshesha Taifa mapato mengi sana. Nilikuwa naomba wakati wa bajeti ya mwaka huu tutakapokuja tuwe tumehamia katika Sheria mpya ya madini. Kama mazungumzo na makampuni ya madini yanaendelea, basi mazungumzo hayo yakamilike. Kwa sababu ni lazima ifikie wakati tuonekane ni dola, tuonekane kwamba tunajali maslahi ya wananchi. Haiwezekani tukawa kila siku tunazungumza lakini hakuna utendaji. Kwa hiyo, imefikia wakati sasa Sheria mpya ya madini iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna baadhi ya vitu ambavyo vimetokea, vitatusaidia Sheria mpya ya madini iweze kufanya kazi. Kwa mfano, pale *North Mara* mgodi ule wa *North Mara* leseni yake imekwisha. Inahitaji kufanyiwa *renewal*. Hii ni opportunity ya kufanya mgodi ule uingie kwenye sheria mpya ya madini, kwamba tutakapofanya *renew* ya mgodi wa *North Mara* tuhakikishe kwamba *renew* inahakikisha ule mgodi unahamia kwenye Sheria mpya ya madini tupate *royalty* mpya, tupate kodi ya mapato na tupate fedha kwa ajili ya maendeleo katika Wilaya ya Tarime. Lakini vile vile pale *Tanzanite One*, leseni yao imekwisha, inahitaji *renewal*. Sheria yetu ya madini inataka kwamba asilimia 50 ya watu wanaochimba vito, kwanza asilimia mia moja lazima iwe ya Watanzania. Kama Watanzania hawawezi kuendeleza, basi asilimia 50. Hii ndiyo opportunity ya kuweza kuchukua model ya Botswana katika *Gemstone* kuhakikisha kwamba asilimia 50 za *Tanzanite One* kampuni ambayo ina leseni, wakati tunatoa leseni inakuwa ni mali ya Serikali. Tunaweza tukaamua kuipa *STAMICO*, tunaweza tukaamua tukafanya sisi wenyewe au tukaunda kampuni nyingine ambayo itahusika na jambo hilo

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia, nilileta kwako barua zaidi ya mara tatu ya kutaka uchunguzi kuhusu *procurement* ya mafuta ya dharura, hasa hasa ilikuwa ni *procurement* ya *IPTL*. Nashukuru kwamba Kamati ya Nishati na Madini imezungumzia jambo hili na imependekeza katika ukurasa wa saba kwamba uchunguzi wa Kibunge ufanyike kuhusu tuhuma za rushwa na ujisadi kwenye ununuzi wa mafuta ya kuendesha mitambo ya dharura.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sasa kwa sababu Kamati imeweza kulieta ndani ya Bunge, naamini kabisa kwamba Bunge litaweza kupitisha jambo hili uweze kuwezesha uchunguzi huo kufanyika. Tunapoteza fedha nyingi sana kwenye *procurement* ya mafuta. Sasa hivi kwenye kiwango chetu cha fedha kwa ajili ya kulipa *TANESCO Shilingi* billioni 408. Siyo kwa ajili ya kununua mitambo, siyo kwa ajili ya kuwekeza, ni kwa ajili ya kwenda kununua mafuta. Tunachukua Shilingi billioni 408 kama mkopo tunakwenda kuzichoma. Kwa hiyo, ni lazima tuwe makini sana katika *procurement* hizi za mafuta. Kuna ambaao wanafaidika na *commissions* katika *procurement* hizi.

Mheshimiwa Spika, tunanunua mafuta kwa bei kubwa sana. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba uchunguzi huu uweze kufanyika mara moja, mara baada ya Bunge kuwa limepitisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kutohana na muda, naomba tuwekeze vya kutosha katika Sera yetu ya Mambo ya Nje. Tunataka Wizara ya Mambo ya Nje ifanye kila kitu, lakini hatuipi fedha. Kuna taabu sana kwenye Balozi zetu. Lazima tuwezeshe Wizara ya Mambo ya Nje iweze kutekeleza Sera hiyo ya *Economic Diplomacy* inavyopaswa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi siyo muumini sana wa *Economic Diplomacy*. Mimi ni muumini mkubwa wa Sera yetu ya awali ya Mambo ya Nje. Lakini kwa sababu tumeamua kwenda kwenye *Economic Diplomacy*, basi tuweke feadha katika hilo ili Wizara ya Mambo ya Nje iweze kuwa na *staff* wa kutosha na kwenye maeneo ambayo tunataka *investors*. Maeneo ya nchi ambazo zinaibuka kama China, India, Brazil tupeleke watu ambaao ni *specific* kwa ajili ya *promotion* ya *investments* ili kuiwezesha Wizara ya Mambo ya Nje iweze kufanya kazi zetu vizuri na kutuletea *investors*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono mapendekezo yote ya Kamati zote. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, ningetamani sana tuendelee mpaka saa 12.00 jioni, kwa sababu watu wanaotakiwa kuongea hapa wako wengi kabisa. Wamebakia kama watu 20 na kwa hiyo, tukisema tuendelee wote, hatutaweza. Hao ninaosema ishirini ni Wabunge wanaoomba kuongea. Lakini kawaida yetu, ni lazima kuwe na *reaction* kutoka upande mwingine wa Serikali halafu na Wenyeviti watoe majibu yao.

Kwa hiyo, napenda nisitishe majadiliano haya, niingie sasa kuwaita Mawaziri. Nianze na Waziri kwanza, ataanza Waziri wa Nishati, halafu watafuata Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Mambo ya Nje, Waziri wa Uchukuzi, Waziri wa Mawasiliano halafu kutakuwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Hawa wote dakika ni kumi tu.

Nasema hivyo kwa sababu bado wana nafasi kubwa kabisa mwezi ujao kuandika hotuba zao *accordingly* na pia kwa kuwa tumekubaliana na Serikali kwamba zile taarifa za Kamati zina mapendelekezo mengi sana na mengi hayakuweza ku-manifest hapa kwa sababu hata Wenyeviti hawakuweza kusoma taarifa zote, kwa hiyo, zimeingia kwenye *Hansard*.

Kwa hiyo, Serikali itabidi itoe majibu kwa maandishi kwa taarifa hizo pia, na kwa sababu hotuba zile zipo kwenye *Hansard full*, ni vizuri ikapata *reaction* upande wa pili wa Serikali. Kwa hiyo, kwa sasa hivi ni dakika kumi kumi tu. Kwa hiyo, naanza na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake.

MWONGOZO WA SPIKA

MCH. PETER S. MSIGWA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Tukifanya miongozo, ndiyo tunamaliza muda. Tunamaliza muda! Mwongozo, sidhani kama unahusiana na haya, na nimeambiwa kuhusu mwongozo wako. Naomba ukae kwanza. Kwa hiyo, Waziri wa Nishati na Madini. Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja. Naomba kwanza nitambue hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini - Mheshimiwa January Makamba ambayo ndiyo Kamati inayosimamia shughuli za Wizara yetu. Lakini pia naomba nijielekeze kwenye hoja za Mheshimiwa Daktari Abdallah Kigoda - Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ambaye amezungumzia masuala mbalimbali katika hoja yake ambayo zinaingiliana kwenye Sekta yetu moja kwa moja ambazo ni hoja mbali mbali kama za athari za usimamizi wa mafuta na bei, athari yake kwenye mfumko wa bei, masuala ya madini, suala la kwisha mikataba na

namna itakavyochangia kwenye kuongeza mapato ya Taifa, kuweka misingi ya matumizi ya gesi asilia na kuharakisha kukamilisha bomba la gesi asili, udharura wa kipekee na umuhimu wa kupunguza ghamama kubwa za kuzalisha umeme pamoja na namna ya uzalishaji wa umeme nafuu kwa ajili ya gesi.

Sasa hiyo nilikuwa nafikiri nitambue hoja hizo zilizokuwemo kwenye Taarifa hiyo ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na sasa naomba nijielekeze kwenye Kamati ya Nishati na Madini na hoja zilizotoka huko pamoja na hoja nyiningine zilizotoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala yamejielekeza kwenye maeneo mbalimbali mengi ya sekta hizi mbili. Lakini moja ni hili la kuhusu umeme na mapendelekezo ya kuchanganya vyanzo vya nishati ya umeme kama sehemu mojawapo ya namna ya kupunguza ghamama za uzalishaji na hoja hii ina misingi ya kitaalam na kiuchumi. Kule wenzetu wanaita mikakati hii wanaitambua kama *energy mix*, kwa maana kwamba kama una vyanzo mbalimbali kwa maana ya maji, makaa ya mawe, upepo na joto ardhi, unaweza ukazipangia mkakati kwa namna ambavyo kwa mfumo huu wa *energy mix* ukawa na uzalishaji wenyе ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sisi tumejielekeza huko na kwa sasa hivi tuna matarajio kwamba uwekezaji unaofanyika katika maeneo haya mbalimbali utaturuhusu kufikia malengo hayo. Kuna suala la ubovu wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme na nilikuwa nimefikiria tu, ni vizuri nikasema kwamba miundombinu hii ubovu wake na *transmission loses*, *energy loses* zinazotokana humo zimo kwenye pande zote mbili kwa maana ya *transmission* na *distribution*.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya mwaka jana wakati tunajielekeza kwenye mpango mkakati wa dharura, tulijielekeza zaidi kwenye uzalishaji kwa maana ya *generation*. Baada ya muda kidogo ikajitokeza kwamba hata ule umeme wa ziada ulioingia, ulilingia kwenye matatizo ya *distribution* kwa sababu ya kukosa ushauri wa kitaalam uliojielekeza kwenye masuala ya *transmission* na *distribution*.

Mheshimiwa Spika, kwa mimi nadhani tumelipokea, tumelizungumza kwenye Kamati mara nyangi na TANESCO wenyewe tumeshawaelekeza mara nyangi kwamba sasa tutengeneze mkakati wa kuboresha ubora wa *transformer*. Kuna suala limezungumzwa sana ambalo ni suala *transformer* mbovu, labda zinaungua mara kwa mara na kadhalika na maeneo mengine ambayo kusema kweli, ni lazima tutengeneze mikakati ya makusudi kuboresha mifumo ya miundombinu kwenye *transmission* na kwenye usambaji kwa maana ya *distribution*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililojitokeza kwenye taarifa ni ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uzalishaji ili hata sasa hivi Mheshimiwa Kigola amelizungumza kwa upande wake kule Mafinga, limeingia kwenye Sao Hill na kule Mwenga, tumekwenda juzi, tumekuta jitahada za makusudi ambayo wawekezaji binafsi wanataka kuzalisha kama Megawatt 50 hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili jambo la PPP's na nini linaonekana linafanya kazi vizuri na linapata mwamko kwa upande wa uzalishaji. Kukabiliana na upotevu wa umeme, *transmission loss* na *distribution loss* nimelizungumza hapo mbele. Ni kweli tuna upotevu mkubwa wa umeme kwa sababu ya uboreshaji wa masuala ya uboreshaji wa miundombinu ambayo hayajafanyiwa mkakati mzuri bado. Lakini una ghamama kubwa na nilikuwa nimefikiria niliseme hilo kwa sababu ghamama za usambazaji na kuboresha malipo ya uunganishaji nalo limezungumzwa kama eneo moja ambalo Waheshimiwa Wabunge na pia taarifa imejielekeza kuona namna ya kupunguza hilo, nalo ni katika masuala ambayo tumejielekeza mara kwa mara kujibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ni mkakati kwenye kupunguza ghamama za uunganishaji na usambazaji, tuliangilie zaidi. Lakini pia tuboreshe, tusisitize kwamba TANESCO waendelee na ule mpango wa kuunganisha umeme, kulipa kwa awamu kama njia mojawapo ya kuwanufaisha Watanzania kuweza kuunganisha umeme zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mapendekezo, kwenye ripoti ile kuna mapendekezo ya biashara ya mafuta pamoja na masuala mbalimbali ya Sekta ya Madini. Tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwamba atajielekeza huko. Lakini kuna masuala ya kwisha mkataba, *local procurement of goods and services* na masuala ya *cooperative social responsibility* na namna ya kupatia tafakari mpya ili yawe yana manufaa zaidi katika uchumi wetu na pia kwenye *local economy*. Naomba nimwachie Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye Sekta Ndogo ya Gesi ambayo imezungumzwa kwa ukamilifu na naomba nipongeze sana Kamati zote mbili ya Fedha na Uchumi na Nishati na Madini pamoja na Waheshimiwa Wabunge na pia Waheshimiwa Wabunge kutoka Kamati ya Mashirika ya Umma, wamelizungumzia hili. Tumeshakwenda kwenye Kamati na tunesema. Ni kweli kwamba sasa hivi Sera, Sheria zinazosimamia Sekta ya Gesi nchini ziko *out dated*. Sheria ile ni ya mwaka 1980, Sera ni ya Nishati, siyo Sera ya Gesi. Kwa sababu tunasema ziwe sera *specific* ambayo wataalam wamejifungia, wanatarajia kuikamilisha mwezi wa Kumi na Mbili. Sheria nayo ilikuwepo, lakini Sheria ile kama

ingekuja Bungeni kwa sasa hivi katika mazingira ya mpango mkakati huu, *strategic plan* mpya ya gesi ambayo inatoka mwezi ujao kama rasimu ya kwanza. Ni lazima vitu hivi vitatu viende pamoja na lazima tuseme, juzi kwenye taarifa kwenye mitandao hii ya *Gas Oil* wanasema nishati ambayo itabadiilisha *the next big energy source in the world* ni *natural gas*.

Sasa sisi Tanzania Mwenyezi Mungu ametujalia, *we are going to have hii idadi ya twenty TCF. If* tafiti hizi na *drilling* zikimalizika *in the next two years, we should be a player* katika masuala ya gesi. Kwa hiyo, masuala yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba lazima tufanye mipango ya kujiaandaa. Sisi Wizarani tunaitambua na tumeanza. Tunatambua kwamba lazima tuwe na wataalam *specific* wa gesi kwenye usimamizi wa kisheria, usimamizi wa uhasibu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala limeletwa na Kamati kuhusu utaratibu huu wa kufanya maamuzi ya GNT. Masuala haya unakuta yanaundiwa Kamati kubwa, GNT zinakaa zinazunguka mwaka mzima. Nadhani na sisi huku pia tunakubaliana na mawazo ya Kamati kwamba hizi kazi zinakosa ufanisi kama mkijaza makundi mengi yanakaa kwenye vikao miezi sita, miezi saba kwa jambo ambalo linaweza likaamuliwa ndani ya miezi miwili kwa wataalam wenyе sekta yao.

Mheshimiwa Spika, hili la wananchi waliopo kwenye maeneo ya gesi wapate mrabaha. Hili linazungumzika kisheria, tumeshalisema hapa Bunge na tutaendelea kufanya kazi na Wabunge wa maeneo hayo, akina Mheshimiwa Mangungu na wenzake. TPDC kubakia na asilimia 50, hili liko Hazina na sisi tumelipeleka. Kuhusu utoaji wa taarifa ya masuala yote husika ya gesi, hili ni suala ambalo tunalifanyia kazi ili kuboresha taarifa kwa wananchi, wapate ufahamu zaidi wa masuala yanayoendelea kwenye upande wa gesi.

Kwenye upande wa utafiti, mapendekezo ya Kamati tumeyapokea. Kuhusu mikataba mipyä kwamba isubiri Sheria mpyä, *it is true*, tukiifanya sasa hivi kuna suala la kuwa *retrospective*, litatupa shida baadaye. Kwa sababu tunatarajia kwamba Sheria mpyä itakuwa tayari pamoja na Sera ndani ya miezi miwili, linaweza likaja hata kwenye Bunge lako la Bajeti tukaomba udharura ili tulipokee, Rais alifanyie *ascension* ili lianzé kutumika na mikataba hiyo mipyä.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limeonyesha wasiwasi kwenye Kamati ya Nishati na Madini ambalo lipo, *it is a fact* ni suala la utoaji wa maeneo. Hata kule Uganda, wenzetu wametuambia, inaonekana

maeneo yetu ya leseni ni makubwa ukilinganisha na maeneo mengine. Kwa hiyo, ni jambo ambalo...

(Hapa kengele illia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia. Naomba nianze kwa kujielekeza moja kwa moja kwenye hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu - Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini na baadhi ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge, kuhusu masuala yanayohusu Wizara ya Ujenzi ambayo yanahitaji ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nikubaliane na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kuhusu kuwapa fursa zaidi Makandarasi wa ndani. Ningependa kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tumeanza kuchukua hatua katika kuwapa fursa zaidi Makandarasi wa ndani. Mfano ni ujenzi wa daraja jipya la Mbutu huko Igunga, ambalo linajengwa na Makandarasi wadogo wadogo wa ndani. Wameungana Makandarasi wadogo 13 siyo tu kwa lengo la kutekeleza huu mradi, lakini vile vile kuweza kujijengea uzoefu stahili.

Mheshimiwa Spika, vile vile miradi mingi ya barabara za Mikoa, sasa hivi tumeruhusu Kampuni za Ndani kutekeleza na baada ya kulegeza vigezo; kwa mfano, Bodi ya Makandarasi (CRB), imefikia hatua ya kuruhusu Makandarasi wadogo wadogo wa madaraja ya chini, wakijiunga wanapandishwa daraja. Hiyo imekuwa ni *motivation* na kuweza hata kuomba kazi ambazo ni kubwa zaidi ya madaraja yao. Mfano hasa, ni miradi ya PMMR, (*Performance Based Management and Maintenance of Roads Program*), ambayo inatekelezwa katika Mikoa ya Mwanza, Tanga pamoja na Rukwa ambapo Makandarasi wa ndani, ndio wanapewa hizo kazi kubwa, ambazo wasingeweza kuzipata huko mwanzoni, wanaungana kama *joint venture* wanapanda ngazi.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, tunapambana na changamoto nyingi mno, ikiwemo changamoto ya usanii wa baadhi ya hawa Makandarasi wadogo wadogo; anaunda kampuni yake yeye mwenyewe binafsi au hata kampuni *fake* tu, anajifanya anaungana nayo kuunda *joint venture* halafu anapata huu mradi. Tumegundua hiyo katika mradi wa PMMR, Mkoani Tanga na Mheshimiwa Mbunge Herbet Mtangi alilalamikia hiyo. Tumetoa maelekezo kwa *Tanroads* kwamba, kwa kweli

21 APRIL, 2012

hatua kali zichukuliwe dhidi ya Mkandarasi huyo, na mimi naamini *Tanroads* wamefanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile nakubaliana na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kutoanzisha miradi mipyä mpaka tutakapomaliza kulipa madeni ya miradi inayoendelea kwa sasa. Ni kweli tumekuwa na tatizo la malipo kuchelewa kwenye baadhi ya miradi na kusababisha kazi kwa vipindi fulani kusimama ama hata kwenda polepole.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, pamoja na kwamba kwa sasa Wizara ya Fedha imeielewa vizuri hali ambayo inatukabili ya ujenzi wa barabara na miundombinu na imeweza kulipunguza deni hilo kwa kiasi kikubwa mpaka sasa, lakini bado Wizara ya Ujenzi itazingatia ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, kuepuka miradi mipyä na kutoa kipaumbele kwa miradi inayoendelea sasa. Nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge, tutakapokuja na bajeti mipyä, ambayo kwa kweli haitakuwa na miradi mipyä msitusulubu. Naomba mwelewe tu hali halisi ambayo tunayo, lakini tutakuwa tayari kusikiliza maoni yenu.

Mheshimiwa Spika, wazo la kuwa na barabara za malipo (*Toll Roads*), nalo tunalipokea kwa mikono miwili. Lakini vile vile, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, tumeshaanza kulifanyia kazi, tumeanza kwa kuwavutia wawekezaji kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ukiwepo mradi wa barabara kutoka Bandari ya Dar es Salaam mpaka Chalinze, yenyé urefu wa kilometra 100. Tunaita *Dar es Salaam – Chalinze Expressway*, ambayo kwa kweli ikishajengwa hiyo barabara, mtu kuitumia, analipia kidogo. Tumefanya hivyo kwa kufanya kazi ya utafiti, kuwaonyesha wawekezaji kwamba mradi huo unalipa.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi tu, kwa mfano, tumebaini kwamba barabara ya kutoka Bandarini mpaka Ubungo kwa siku ina magari 47,186. Ubungo mpaka Kimara, ni magari 26,670; Kimara mpaka Maili Moja, magari 16,557 na Maili Moja mpaka Chalinze ni magari 8,806 kwa siku. Aidha, daraja la Kigamboni vilevile ambalo kwa kweli, wote mnalifahamu linajengwa kwa ubia katì ya NSSF 60% na Serikali yetu 40% kwa gharama ya Shilingi bilioni 214.64 litakuwa la kulipia, litakuwa ni *Toll Bridge*.

Mheshimiwa Spika, suala la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, tumeliongelea sana hapa katika Bunge lako Tukufu na Kamati yetu vilevile imetushauri mara kwa mara ni yapi ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kueleza tu kwamba, Jiji la Dar es Salaam peke yake lina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometra

2,727. Kati ya hizo, ni kilometra 540 ambazo ziko chini ya Wizara yangu na kwa sasa tunapitia maombi ya Halmashauri ya Jiji ya barabara nyingine 23 kuwa za Mkoa kama alivyoeleza Mheshimiwa Mnyika, na kama ambavyo tunapitia maombi mengine zaidi ya 200 ya kutoka sehemu mbalimbali nchini kwa lengo la kuziboresha.

Mheshimiwa Spika, tuna miradi inayoendelea ya ujenzi, tumeshaielezea hapa *Ubungo Bus Terminal – Kigogo – Kawawa Roundabout* kilometra 6.4, *Kawawa Roundabout – Mbezi Valley – Jangwani/Twiga Junction* kilometra 2.7 na *Jet Corner – Vituka – Davis Corner* kilometra 10.3. Tunapanua vile vile barabara ya Mwenge kwenda Tegeta na tukimaliza tunapanua barabara ya kutoka Morocco mpaka Mwenge kwa lengo tu la kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano Dar es Salaam. Sasa hivi, tunaboresha barabara ya Kilwa na uboreshaji huu utakwisha mwishoni mwa mwaka huu. Ujenzi wa daraja la Kigamboni vilevile na ujenzi wa barabara ya Bagamoyo kwenda Msata ambayo ina urefu wa kilometra 64, ni sehemu ya mikakati ya kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, aidha, tuko kwenye mazungumzo na Serikali ya Japan, kufadhili ujenzi wa *Fly Over* eneo la TAZARA. Tunahangaikia financing ya *fly over* maeneo ya Ubungo, Mwenge, Morocco, Magomeni, Chang'ombe na hata Uhasibu. Aidha, tuna msururu wa barabara tunazozifanyia usanifu zikiwemo *Ring Roads* ambazo kutohana na muda, siwezi kuzitaja zote. Lakini kuna barabara za pete kama Pugu (*Nyerere Road*) kwenda Mbezi mpaka Bunju, kilometra 33.9 na vilevile barabara ya Banana (*Nyerere Road*) kwenda Mbezi – Maramba Mawili mpaka *Wazo Hill*, kilometra 37.67.

Mheshimiwa Spika, vilevile mradi wa mabasi yaendayo kwa kasi, ambao unahuishwa ujenzi wa barabara mbalimbali, ujenzi wa vituo na hata karakana. Mradi huu, unaendelea ingawa umekuwa na vikwazo vya hapa na pale, hasa katika uondoaji wa miundombinu, milingoti ya umeme, mabomba ya maji, bomba la gesi na vilevile nyumba za ibada na nyumba za wananchi wa Dar es Salaam. Tumejikuta mara nyingi tukifkishwa Mahakamani na mradi kusimama, lakini tuna uhakika tutaukamilisha huu mradi. Serikali inaangalia pia uwezekano wa kutumia usafiri wa maji kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo ili kupunguza pressure kwenye barabara za Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa wazo ambalo limetolewa kwa nguvu na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa, nakumbuka Mheshimiwa Mwanjale na Mheshimiwa Daktari Mahenge kwamba, kwa

kweli kuna umuhimu sasa wa kuanzisha *Rural Road Agency*. Suala hili la kuanzisha *Rural Roads Agency*, linafanyiwa utafiti na *TAMISEMI*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami napende kwanza kuipongeza Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa Taarifa nzuri ambayo imetupa mwanga na changamoto nyingi. Napenda pia niwashukuru Waheshimiwa John Komba, Mheshimiwa Sanya na Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa kuchangia kwenye masuala yanayohusu Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la mpaka wa Tanzania na Malawi, ambalo lililetwa na Mheshimiwa Komba, na kwenye Taarifa ya Kamati ya Kudumu limejitokeza.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, kama alivyosema Mheshimiwa Komba, kumekuwa na matatizo yanayokera kwenye mpaka wetu na Malawi baada ya mwezi uliopita kuonekana ndege mbili za kitafiti na meli kando kando ya mpaka na hasa upande wa *Mbamba Bay*.

Ningependa kuwahakikishia Watanzania wote na hasa wanaotoka kwenye maeneo yale niliyoyasema ya *Mbamba Bay* na Ziwa Nyasa, bila kuwasahau wakwe zangu na shemeji zangu kwa sababu nimeoa pale, kwamba, wasiwe na wasiwasi kabisa kwa sababu hatua za Kidiplomasia zimeanza kuchukuliwa. Mara baada ya msiba uliowakuta wenzetu wa Malawi kumalizika Jumatatu, mazungumzo ya Kidiplomasia kati ya pande zote mbili yatakuwa yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata kwa upande wa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, ningependa kuwahakikishia wananchi wa maeneo yote yale, wakae kwa amani na utulivu bila wasiwasi wowote kwa sababu, majeshi na vyombo vyetu viko imara na viro katika hali ya kuwalinda na kuwatetea wananchi wale na wala wasiwe na wasiwasi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wa mazungumzo yote yaliyokuwa yanafanyika hapa, yanalingana sana na Diplomasia ya Kiuchumi ambayo Wizara yangu inasimamia. Ningependa kwanza nitoe *caution* ya ujumla kwamba, Afrika sasa hivi, Tanzania ikiwemo, inapita kwenye mtihani mkubwa sana wa mataifa makubwa kutaka kuingia Afrika kwa ajili ya kufanya mambo mawili makubwa yanayoweza kuleta hatari.

La kwanza, wamebaini kwamba, Afrika ni sehemu ambayo unaweza sasa kuleta kila aina ya bidhaa bila kujali *standards* zake, Afrika ikawa a *dumping place*, kwa *markets* ya *products* za Ulaya. Hili ni jambo la hatari na nimefurahi kwamba, baadhi ya michango iliyotolewa humu ni ya kujaribu kujiasa wenyewe kuwa waangalifu sana na bidhaa zinazoingia kutoka duniani kuja nchini, ambazo tusipoangalia tunaweza tukajikuta tunakuwa soko la kila kitu kinachoweza pengine kuathiri afya na usalama wa nchi yetu. Nimelipongeza hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini ipo hatari ya pili. Hatari ya pili ni ya dunia kutaka *resources* za Afrika kwa kutaka maendeleo yao. Huo ndiyo mtihani wetu wa pili. Nimefurahia sana mijadala iliyoenedlea hapa kwamba, wakati umefika wa kuchunga mali na rasilimali zetu, tusizitoe kirahisi. Hivi ninavyozungumza Bara la Afrika tayari limepoteza ekari milioni 29 kwa wageni kutoka nje ya Bara la Afrika, ekari za ardhii milioni 29, hatunazo tena, ni mali ya watu wa nje. Kwa hiyo, ni wajibu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninalipongeza Bunge kwa kuziangalia rasilimali za nchi yetu na kutuhimiza kwamba tusiwe na uholela katika kutunza rasilimali za nchi yetu. Ndugu zangu, Afrika inaweza ikaishi bila dunia ya Nje, lakini dunia ya sasa inashindwa kuishi peke yake bila rasilimali za Afrika. Tusipokuwa macho kulinda rasilimali zetu, tusipokuwa macho kuwa na sheria zinazowabana wageni katika kufika na kushiriki kutoa rasilimali zetu, tunaweza tukajikuta Afrika imechukuliwa kama walivyogawana mwaka 1884 wakati wa *Berlin Conference*. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Mambo ya Nje, na ninashukuru mmeliona hili, mbali na ukata mkubwa wa fedha, mbali na matatizo makubwa ya fedha kwenye Balozi zetu, tunachokifanya kikubwa ni kujaribu kutoa Sera ya Uchumi wa nchi yetu na tunashukuru Wizara mbalimbali na *TIC*, pamoja na Wizara ya Utalii na Maliasili pamoja na Wizara nyingine zote na mipango, kwa kutupa nyaraka zinazowaelekeza wawekezaji, wafanyabiashara, watalii, pamoja na watu wengine wote wanaokusudia kuja kufanya shughuli zao nchini wafuate masharti gani? Waje wamwone nani? Wafuate taratibu na sheria gani? Kazi hii inafanya na Mabalozi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii kuwapongeza mabalozi na Maafisa wa nje ambao wanafanya kazi kwa hali ngumu sana kutohana na ufinyu wa bajeti, lakini wanajaribu sana kwa kasi inayotakiwa, kujaribu kuwaleta wawekezaji, kuleta wafanyabiashara na watu wengine kuja kuwekeza nchini. Lakini kama mnavyojuu wote na mlivyozungumza, siri ya ku-break poverty circle tuliyonayo kwa vyovvye vile ni *investment* kwenye *energy*.

Nawashukuru wote ambao wamezungumzia suala la umuhimu wa *energy investment* kwamba, wenzetu wa Korea Kusini ambao tulikuwa na *population* moja mwaka 1965, tulikuwa na *GDP* moja mwaka 1965 na hali ya uchumi yote ilikuwa ile ile, wenzetu sasa wametuzidi baada ya kuwekeza sana kwenye *energy*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wenzetu wana *Mega Watts* 70,000. *Mega Watts* za umeme 70,000. Sisi *Mega Watts installed capacity* 1,000 na zenyewe ikinyesha mvua, isiponyesha mvua ni 930 na mvua ikikosekana kabisa tunarudi mpaka 300, wenzetu 70,000. Kwa hiyo, tunao umuhimu na wametuzidi sasa, wanaunda magari, wanaunda matrekta na kila kitu.

Kwa hiyo, siri kubwa pamoja na yote, akina Mheshimiwa Membe kuwaleta wawekezaji, wafanyabiashara na hasa wawekezaji, swali moja kubwa wanaloatuuliza, unaweza kunigawia *Mega Watt* 2,000 ili nilete viwanda vinne? Tuna *Mega Watt* 900.

Unaweza ukani patia *Mega Watt* 500 ili niweze kuleta kiwanda cha *Tractor Assembly* kwa mfano, anahitaji *Mega Watt* 500, tuna 900. Kwa hiyo, kwa vyovytile, naunga mkono wazo linalojitokeza sasa kwa kasi kwamba, ili ku-break poverty circle na kuleta maendeleo ya kweli nchini, ni lazima tu-invest kwenye *energy*.

Mheshimiwa Spika, tupate *Mega Watt* zakutosha, ili tuweze kuwa na pesa za kutosha, tutapata ajira za kutosha, ili tuweze kuondokana na matatizo haya ambayo yanaweza kabisa kuhatarisha hata usalama wa kazi zetu tunazozifanya. Napenda kutoa Hoja na kuunga mkono Hoja ya Kamati. Ahsante.

SPIKA: Umezungumzia habari ya Korea ya Kusini, sisi tulikwenda kule tukakutana na wanafunzi wa Tanzania wanaosoma Korea ya Kusini. Wao ombi lao lilikuwa hivi, Korea Kusini ule umeme anaousema Mheshimiwa Waziri, ni wa *Nuclear Energy*, hawana madini haya tunayozungumza sisi, hawana kabisa. Wanafanya *importation*.

Sasa wale wanafunzi kwa nia njema wakasema, kawaambie basi Tanzania, muwatafute hawa Wakorea Kusini, wachimbe haya madini ya *Uranium* hapa, wenyewe wawaekeni mtambo wa *Nuclear Energy*. Basi ndivyo walivyosema, hawana hii *uranium* kabisa, wana-import na ndiyo hiyo inayotengeneza *Mega Watts* zote hizo.

Kwa hiyo, wale wanafunzi wa Tanzania walioko kule, ndio wanasema, kwa nini Serikali yetu isiwauzie *uranium* na wao

21 APRIL, 2012

watutengenezee mitambo ya *nuclear*? Mimi sio Mtaalam, kwa hiyo, ndiyo hapo hapo waliposema hivi siku hiyo.

Waheshimiwa Mawaziri, hapo hizi Hoja ni za Kamati, sio zenu. Kwa hiyo mnachangia tu. Kwa hiyo, ukimchagua Naibu ndio huyo huyo, ukisimama wewe ndio huyo huyo. Lakini siyo kwamba, Naibu na nani mtazungumza. Hapana.

Kwa hiyo, sasa naita Wizara ya Uchukuzi. Sasa mtaamua nyie, Naibu au nani? Lakini ni mmoja tu.

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):
Mheshimiwa Spika, name nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambazo ziko hapa.

Mheshimiwa Spika, masuala ya uchukuzi yaliyoongeleta ni mengi. Siku ya leo tungekuwa na nafasi ya kuyadadavua na kuyachambua moja hadi nyingine, lakini tutaleta kwa maandishi kwa sababu kuna moja nzito ambayo inabidi ipate ufumbuzi hapa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ambazo zimefanywa na Kamati na pamoja na kufuatilia kwa makini, Kamati ya Miundombinu ilipokuja kuliongelea suala la gati namba 13 na 14 ya Bandari ya Dar es Salaam, wakataja kuna *MoU*, na *MoU* ikawa na shutuma kubwa dhidi yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako hili, pamoja na Watanzania na dunia kwa jumla kuwa *MoU* iliyotajwa hapa haipo. Hakuna *MoU* ambayo tumesaini na *China Merchant* hasa nikiambiwa nimesaini mimi ambayo imetajwa hapa na tuhuma zote hizo. *MoU* peke yake ambayo Wizara ya Uchukuzi imesaini na *China Merchant*, *MoU* ambayo ilianzishwa kwa kuangalia *proposals* ambazo *China Merchant* walizileta, ikafanyiwa kazi kwa undani sana na taasisi zote husika, wakati huo mimi nilikuwa Zambia na Waziri wa Uchukuzi wa Zambia. Niliporejea tukaenda *China* kwa mwaliiko wa Serikali ya Uchina kukutana na Wizara tatu kuongelea maendeleo ya mambo ya uchukuzi na pia kwenda *China* kukutana na Rais wa *Exim Bank*.

Mheshimiwa Spika, mpaka Novemba, 2011 *Exim Bank* walikuwa hawajatoa kauli yoyote kama wataweza kutukopesha pesa au laa. Niliongea na *Exim Bank* kwa simu, nikaenda *China* na nikakutana na Rais wa *Exim Bank* Bwana Li Ruogu akatoa kauli kwa mara ya kwanza baada ya kuwa tulikuwa tunaongelea kuomba hela za *Exim Bank* tangu mwaka

2008, Novemba 27 ndiyo kwa mara ya kwanza mbele ya watendaji wa TPA Bwana Li Ruogu alitoa kauli hiyo.

Mheshimiwa Spika, tulipofika kule tukaichambua zaidi hii MoU ambayo imetayarishwa na taasisi zote hapa AG Chambers, Taasisi, Wizara lakini hata ilivyokuwa nilipofika kule bado kulikuwa na vipengele ambavyo ilibidi niviingilie kati niviweke sawa. MoU tuliyo nayo ni hii. Kule niliambiwa naweza ku-*initial* tu, nika-*initial* tukiwa Uchina, tukarudi hapa. Tarehe 5 Disemba, 2011 MoU ikasainiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi. MoU hii inachofanya ni kumpa fursa yule mwekezaji aje atayarische *feasibility study*, akiweza atayarische *detailed design* bila ya sisi kuingia gharama. Tumeingia kwenye MoU siyo na *China Merchant* peke yake bali tunazo nyingi sana na kampuni tofauti. Hii MoU ya sisi na *China Merchant Holdings* naomba kuiwasilisha kwenye meza, tunazo nyingi ambazo siyo za China tu, kule China tulisaini baadhi na tumesaini na watu wengine wengi. Kwa nini tulikuwa tunafanya hivyo? Nilipoingia Wizarani hapa sikuona mwelekeo unaokwenda kwa kasi katika kutekeleza miradi yetu. Nikaanza mtindo huu wa kuwa twende tuitishe wawekezaji kwa kila project wawekezaji wa maeneo mbalimbali. Kama tunataka tugharamie sisi wenyewe hiyo miradi basi tukope pesa, kama tunataka mtu awekeze basi aje mwekezaji, tumetumia mifumo yote miwili hiyo.

Sasa kabla sijaenda mbali, naomba niende kwenye tuhuma zilizosemwa hapa ambazo zimeorodheshwa katika taarifa ya Kamati ya Miundombinu aya ya 3.4.1 hadi 3.4.5 na pia aya ya 3.3 – 3.10; ya kwanza imesema, tuhuma ya 3.4.1 inadai kuwa mwekezaji *China Merchant* atakayemiliki kuendesha gati hizo na kuzikabidhi kwa Wizara ya Uchukuzi (Serikali) baada ya miaka 45, tuhuma zote hizi siyo kweli nachelea tu kusema ni uongo na uzushi kwa sababu niko Bungeni hapa.

Ya pili inasema mwekezaji hatawajibika kwa lolote kutokana na hasara ambayo Wizara ya Uchukuzi itapata kutoka kwa mdau mwengine, hii nayo siyo kweli. Ya tatu Wizara ya Uchukuzi itatoa mamlaka ya kisheria, siyo kweli. *Memorandum of Understanding* yenye tuhuma hizi haipo na ningeomba Kamati kwa unyenyekevu kabisa wailete hiyo *memorandum of understanding* wanayoongelea ionekane hapa, kila mtu aione. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu lingine ni kuhusu *Exim Bank*, kama nilivyosema *Exim Bank* nilikwenda nikaongea na Rais Li Ruogu na nikaomba na kwa mara ya kwanza wakatoa kauli. Lakini taratibu zilizopo za kutaka tupate mkopo wa *Exim Bank* hazijakamilika na mpaka sasa hatuna mkopo wa *Exim Bank*. Sasa katika Gati 13 na 14 waliojitokeza aidha kuwekeza au kutukopessa pesa nitawataja. Kuna mabenki pamoja

na ya hapa nchini *HSBC, Stanbic, Standard Chartered, Barclays Bank na Development ya South Africa* kwa nyakati mbalimbali na *Exim Bank*. Kama tunataka sisi wenyewe kuwekeza itabidi tuchukue kwenye benki hizo na kila moja ina riba mbalimbali. Lakini kila mmoja kama tunamwambia afanye *feasibility study* kwa gharama zake mwenyewe na kila mmoja anaonyesha gharama zake za ujenzi huo katika gati hizi wawekezaji waliojitokeza ni *DP World, Hutchson Port Holding, Boleroe Company, Gulftaine na China Merchant Holdings*.

Mimi ninachosema ni kuwa washindanishwe hawa ili tuweze kupata ni nani ambaye anatufaa kabla hatujaua ni nani ni mjengaji. Kuna waendeshaji pia waliojitokeza *Trans Net Company* na *Megapro Consulting*, sasa hapa ndiyo tulipo na huo ushindanishaji, siyo hapa hatuuongelei hapa, nilisema wakati mmoja *preference* yangu ni kwa Watanzania wenyewe kuwekeza kwenye Gati 13 na 14. Wanaweza waka-mobilize pesa za kujengea, *preference* yangu ilikuwa ni Watanzania wenyewe kuwekeza pale.

Tatizo lioelezwa hapa ni kama ni tatizo la Nundu yaani Waziri wa Uchukuzi anashinikiza *China Merchant*. Ndugu zangu hilo ni kubadilisha kibao, tatizo siyo hilo, tatizo ni kuwa kuna mjenzi anaitwa *China Communication Construction Company* ambaye kuna watu wanashinikiza atunukiwe miradi hii bila kanuni na taratibu za kueleweka. Kwanza ametucheleweshea huu mradi kwa muda mrefu. Kama nilivyosema tangu mwaka 2008 alisema anafanya *feasibility study*, akasema tunajenga kwa dola milioni 523; halafu atatafuta mkopo wa *Exim Bank* hadi Novemba, 2011 nimekwenda *China* hakuna mkopo ambao *Exim Bank* imeutolea kauli.

Mheshimiwa Spika, Li Ruogu nikiwa naye ndipo kwa mara ya kwanza akatoa kauli kuhusu mkopo. Sasa hawa *China Communication Construction Company*, kwanza haijulikani wamepatikana vipi, hiyo *feasibility study* walioambiwa wafanye ni nani kawatafuta, je, walikuwa na MoU kama hizi zetu sisi, hakuna, gharama zake za ujenzi ni dola za Kimarekani milioni 523 ukifananisha na gharama zinazojitokeza kuitia *feasibility study* za aidha wawekezaji ambao watawekeza wenyewe au tutakopeshwa na benki wao wanaongelea dola za Kimarekani milioni 523 wengine wanaongelea dola za Kimarekani milioni 300.

Halafu hawa *CCCC* wanashinikizo sana, wanashinikizo na shinikizo juzi mtu mmoja alisema mimi sipatani na Naibu Waziri wangu, tulikuwa na Naibu Waziri wangu tunakwenda vizuri sana mpaka walipojitokeza hawa *CCCC*, walipojitokeza wakasema mimi wakanilipie sehemu mbalimbali nikakataa. Wakamchukua Naibu Waziri...

(Hapa alizimiwa microphone kwa kuwa muda wake wa kuzungumza ulimalizika)

WAZIRI WA UCHUKUZI: leleweke vizuri ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Taarifa Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Tunaendelea kwanza, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hizi, hasa hasa hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nitakwenda moja kwa moja kwenye hoja hasa hasa zilizotolewa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu hasa tukianzia na hoja kuhusu ubora wa sauti katika simu za mikononi.

Mheshimiwa Spika, simu za mikononi zimeingia katika nchi hii kuanzia mwaka 1995 na ukiangalia takwimu mwaka 1995 kulikuwa na wateja 2,185. Lakini kufika mwaka 2000, wateja walikuwa wameongezeka kufikia 110,000; kufikia mwaka 2007 tayari kulikuwa na wateja milioni 8.2, lakini mwaka 2008 Disemba tayari tulikuwa na wateja milioni 13, mwaka jana Disemba tayari tulikuwa na wateja milioni 26 yaani milioni 25.8. Lakini vilevile huduma zimekuwa zikiongezeka katika makampuni haya, mwanzoni tulikuwa tukitumia simu tu na sms lakini sasa hivi tutaona ongezeko la *internet* na huduma za utumaji wa fedha. Kwa vyovyyote vile tutaona mitandao hii ilizidiwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini kati ya mwaka 2008/2011 kulikuwa na mtikisiko wa kiuchumi na kulikuwa na ongezeko kubwa sana la wateja, ukiangalia Disemba, 2008 utaona tulikuwa na wateja milioni 13, lakini leo hii (Disemba, 2011) tuna wateja milioni karibu 26 karibu mara mbili ya hapo na uwekezaji *uli-slow down* katika miaka hii na tutakumbuka mashindano ya bei tuliona shilingi moja, nusu shilingi na robo shilingi, kwa hivyo wawekezaji walikuwa katika kupima namna gani soko litakuwa katika hali hiyo kwa hivyo uwekezaji ulikuwa umeshuka kidogo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nini kinafanyika, kabla sijaja hapa nilipata nafasi ya kuwaita ma-*CTO* yaani *Chief Technical Officers* wa mashirika tuone ni kwa namna gani tunaweza kuhakikisha kwamba ubora wa simu unarudi katika kiwango ambacho tumekizoea. Kinachofanyika kwa mfano

mitandao mingi wamekubali na wamesema kwamba kwanza watabadilisha teknolojia zile za kizamani na kuhakikisha kwamba wanaweka teknolojia mpya itakayaoendana na mahitaji ya huduma ya sasa ambayo yanahusisha pamoja na utumaji wa pesa na utumiaji wa mtandao yaani *internet*.

Vilevile makampuni mengi tumeyashauri na yamekubali yatumie Mkongo wa Taifa kwa mawasiliano ya ndani na ya nje ili kuhakikisha kwamba mahitaji ya nafasi katika utumaji wa *data* yaani kwa kutumia *internet* yapitie zaidi kwenye Mkongo wa Taifa na yale mawasiliano ya kawaida yaweze kutumia ule mtandao wao wa zamani. (*Makofi*)

Vilevile tumeyashauri kuongeza na kuhakikisha kwamba yanaongeza minara katika sehemu ambapo kuna *congestion*. Hili nalo watalifanya kuhakikisha kwamba huduma zinarudi katika hali ambayo tumeizoea. Itachukua muda lakini nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba haya mambo tunayafulilia kwa karibu na Taasisi ya TCRA ipo karibu zaidi na tayari imeweka mtaalamu atakayekuwa anaangalia ubora wa mawasiliano katika kila maeneo ambayo huduma inatolewa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kulipia kodi au ukusanyaji wa mapato limezungumzwa sana katika makampuni yetu ya simu. Ni kweli inawezekana kwamba haya makampuni hayalipi kama inavyotakiwa, lakini kama ambavyo nimekuwa nikizungumza au nikijibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tayari Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti yaani TCRA wameanza mchakato wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na uwezo wa kuangalia namna ambavyo watumiaji wanalipia huduma hizo, hiyo ni pamoja na kuangalia na sheria na kanuni zilizopo ili ziendane na mahitaji hayo.

Vilevile hivi karibuni tutatangaza *tender* ambayo itawezesha kumpata mtoa huduma wa namna hiyo ili kutuwezesha sisi kama Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla kuweza kuangalia ni kiasi gani hasa hasa hawa wenzetu wanapata. Kwa hiyo, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge tushirikiane na tuzidi kuangalia na niipongeze tu Kamati yako ya Kudumu ya Miundombinu ambayo kwa kweli tunafanya nao kazi kwa ukaribu sana na tunayachukua mapendekezo yao na tutayafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la kuhamza kutoka analojia kwenda digitali, Mheshimiwa Mwenyekiti ametushauri na Kamati imetushauri kwamba tuweze kuhamasisha kwa kutoa matangazo, suala hili tunalikubali na tayari tumeshaanza, kuna Kamati ambayo itatembelea mikoa yote niwaombe Waheshimiwa Wabunge Kamati itatembelea

katika maeneo yetu na itahusisha vilevile kukutana na Mabaraza ya Madiwani ambao wapo karibu zaidi na wananchi waweze kutoa elimu hii katika maeneo yao na sisi kama Madiwani katika Halmashauri zetu basi tushiriki na tuweze kutoa hamasa.

Mheshimiwa Spika, inawezekana Kamati isifike katika kila eneo kwa sababu ukiangalia mpaka sasa hivi mtandao wa analogia wa televisheni unagusa asilimia 24 tu ya nchi yetu. Mpaka sasa hivi tumeshafika asilimia 20 kuweka digitali kwa hivyo tutaanza sehemu ambazo tayari kulikuwa na mtanado wa televisheni wa analogia halafu tutaenda katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, ningeweza kutoa mengi zaidi lakini nitakumbusha yale ambayo Waheshimiwa Wabunge walipewa na wenzetu wa TCRA siku ya Jumamosi iliyopita waweze kuyapitia yale makabrasha ili waweze kutusaidia na vilevile kuweza kutoa elimu hiyo huko watakaporudi katika majimbo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie hili la anuani za makazi, hili nalo kubwa lilirozungumzwa na Kamati ni kuhakikisha kwamba Wizara inaweka bajeti, labda nizungumzie ili kwamba siyo Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia linalosimamia hili, hili ni suala mtambuka linahusu Halmashauri zote za Manispaa na Wilaya zetu. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge watakaporudi katika Halmashauri zao kama Madiwani, hili tumeliomba kuitia Kamati yetu elekezi yaani *Steering Committee* kwamba kila Halmashauri angalau itenye kiasi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu na kwa ujumla wake pesa itakayotengwa katika Halmashauri hizo ndiyo itakuwa bajeti ya mradi huu.

Kwa hiyo, huu mradi si wa Wizara ya Mawasiliano Sayansi na Teknolojia peke yake bali ni wa sisi sote na niwaombe Waheshimiwa Wabunge tushirikiane, nakushukuru sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):
Mheshimiwa Spika, mimi ni Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, (Mahusiano na Uratibu), Waziri wa Utawala Bora amesafiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nichangie ripoti za Kamati mbalimbali lakini hasa najikita kwa Kamati ya Fedha na Uchumi. Mjadala ambao umeendelea kuwepo hapa umezungumzia kwa kirefu sana na kuhoji juu ya kama kweli uchumi wetu unakua na kama ni kweli unakua kwa asilimia zinazotajwa, mbona kukua huko kwa uchumi hakuna uhusiano na kupungua kwa umaskini?

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoju tatizo la umaskini ni tatizo, kwa hiyo kuhoji jambo hili ni jambo la halali kwamba lazima kukua kwa uchumi kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kupunguza umaskini wa watu wetu. Kamati ya Fedha na Uchumi imetoa *analysis* ambayo mimi nakubaliana nayo kwamba ni kweli kwanza uchumi wetu umekuwa na unakua kwa asilimia zinazotajwa, lakini sekta ambazo zimekuwa zinakua na kuchangia kwa kiwango kikubwa katika ukuaji wa uchumi, siyo sekta zinazoajiri watu wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ambazo zimekuwa zinachangia katika kukua kwa uchumi ni sekta za huduma zaidi. Kwa mfano mawasiliano, huduma za kifedha, utalii, utawala na kadhalika zimekua zinakua kwa kiwango mbalimbali na kuchangia kiwango kikubwa zaidi cha kukua kwa uchumi kuliko sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo imechangia kwa asilimia nne kwa wastani kwa kipindi kirefu kilichopita na kwa sababu sehemu kubwa ya Watanzania takwimu inaonyesha kwamba kuna takwimu inaonyesha kwamba kuna Watanzania milioni 32 wanaishi vijiji na wanategemea zaidi sekta ya kilimo. Ukweli ni kwamba sekta hii inapokua kwa pole pole zaidi basi lazima umaskini utakuwa unapungua kwa pole pole kama sekta yenyewe inavyokua.

Kwa hiyo, nakubali kwamba uchumi umekuwa unakua lakini viwango vyatya kwa sekta inayoajiri watu wengi bado havijakidhi kuweza kupunguza tatizo la umaskini nchini. Sasa kama hivyo ndivyo ilivyo tunafanya nini, ndiyo maana katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano ambao nitauwasilisha mbele ya Bunge lako likiwa linaketi kama Kamati ya Mipango tutatoa maelezo ya vipaumbele ambavyo tunaviweka katika mpango ule ili kusaidia kupunguza kwanza kuendeleza kukuza uchumi lakini vilevile ku-address tatizo la umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kilimo kinaajiri sehemu kubwa ya watu, lazima uwekezaji kati ya kilimo uende sambamba na uwekezaji katika miundombinu kwa sababu huwezi kukuza kilimo bila kukuza miundombinu. (*Makofi*)

Kwa mfano, wewe ukiwa Rukwa unalima mahindi lakini mahindi yako yanaoza Rukwa kwa sababu huna barabara ya kufikisha mahindi yako kwa walaji ambao wapo Shinyanga ambapo kuna *deficit* lazima uzalishaji wa kilimo utashuka na umaskini utaendelea.

Kwa hiyo, ninachotaka kushauri hapa ni kwamba katika mipango yetu inayokuja na ule ambao tutaujadili na tutapenda Waheshimiwa Wabunge watoe maoni yao ili kusaidia Serikali kutengeneza mpango na kuuboresha, mpango unaokuja kuanzia mwaka ujao wa fedha na ndiyo

utakuwa mwaka wa kwanza wa kutekeleza mpango wa maendeleo wa miaka mitano, tujaribu kulitazama jambo hili jinsi kilimo kinavyoweza kukua, jinsi miundombinu inavyoweza kusaidia kilimo ili tukifanya hivyo basi tunaweza tukakuza uchumi katika sekta ambayo inaaejiri watu wengi na vilevile kuboresha masoko kwa mfano kama unalima lakini huwezi kuuza huwezi kuendelea kulima. Kwa hiyo, miundombinu ni kitu muhimu sana katika kukuza uchumi na soko kubwa kuliko yote ambayo yanaweza kusaidia kupunguza umaskini ni soko la ndani kwamba unalima hapa na unaweza kuuza hapa hapa na kinachobakia unaweza kuuza nchi za nje na hasa nazungumzia suala la chakula. Kwa hiyo, miundombinu inatusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, reli kama ilivyokwishazungumzwa na wengine na barabara na ninapozungumza miundombinu nazungumza vilevile nishati kwa sababu ili mazao yetu yaweze kuongezeka yaongezewe thamani na wawekezaji wa viwanda lazima tuwe na nishati ya uhakika. Sasa hivi asilimia ndogo sana ya watu wa vijijini wanapata nishati, ili tuweze kukuza zaidi uchumi wa watu wa vijijini ni lazima vilevile tuanze mkakati wa kupeleka nishati kwa maeneo ya vijijini ili viwanda vidogo vidogo vinavyohitaji umeme viweze kupatikana na uwekezaji ukuzwe katika maeneo ya vijijini ambapo ajira ikipatikana tutapunguza watu kukimbilia mijini kwa sababu watakuwa wanajiajiri kule kule, wanalima na mazao yao yanaongezewa thamani na miundombinu ya barabara itafikisha mazao yao sokoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa miundombinu kwa muda mrefu sana kumetuathiri na mimi nasema kwa kweli hatua zilizochukuliwa na Serikali sasa hivi za kuongeza miundombinu ya barabara kutafungua na kuifanya Tanzania iwe nchi ambayo si kubwa kama inavyosema. Wapo watu wanaofikiri kwamba Tanzania ni nchi kubwa, inahitaji Serikali nydingi sana ndiyo ufanisi uonekane, lakini mimi nataka kusema kwamba Serikali nydingi siyo jibu kwa sababu Tanzania ni sawa na Texas kwa ukubwa, Texas ina *State Government* moja na *Local Government*. Kwa hiyo, kuwa na Serikali kila mkoa wenzetu wa Kenya wamejaribu kwa Katiba yao wameweka Katiba ambayo ina Mabunge kibao, ina Mawaziri kila mkoa na mimi nasema hata wenyewe wameanza kulalamika kwamba mfumo huo wa Serikali ni *very expensive*, kwa hiyo, tusije tukaiga tukakuta kumbe pesa zote zinakwenda kulipa posho ya Mabunge katika state kwa sababu rasilimali haziwezi kuongezeka kwa kuongeza idadi ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema ni kwamba tukiimarisha miundombinu ya barabara, tukiimarisha miundombinu ya mawasiliano ya simu na kama tulivyoweka mitandao ya Mkongo wa Taifa kwenda katika

kila Wilaya Tanzania itakuwa nchi ndogo, kama dunia inavyokuwa ndogo kwa sababu ya mawasiliano. Kwa hiyo, mimi nadhani hoja hapa siyo kuongeza Mabunge, Bunge lenyewe moja linatushinda kulipa posho je, tukiweka 10, 20 au 30 tutakuwa tunalipwa wapi? Fedha zetu zote zitaishia katika kulipa posho za Mabunge haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hizi hoja. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na Wajumbe wote wa Kamati yake kwa kweli taarifa hii ni nzuri sana na inatakiwa kuungwa mkono na Wabunge wote na kuitaka Serikali kutekeleza ushauri na mapendekezo yalitolewa na Kamati, pamoja hoja za Wabunge walizotoa kupitia michango yao kwa kuzungumza na kwa kuandika.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na mapendekezo ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu kuanzishwa kwa Kamati ya Bajeti. Hii itasaidia sana Serikali kwa bajeti inayoendana na mahitaji ya wananchi kwani Wabunge ndiyo wawakillishi wa wananchi hivyo wanafahamu mahitaji muhimu ya jamii ukizingatia Wabunge wengi wana fani mbalimbali wakiwemo wachumi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuwa iwe inazipangia ahadi za Mheshimiwa Rais muda wa kutekeleza hii itasaidia kupunguza usumbufu wa kuuliza kila mara. Vilevile utekelezaji upangwe kwa kuangalia umuhimu wa mradi husika.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumalizia mchango wangu kwa kuuunga mkono taarifa ya Fedha na Uchumi mia kwa mia. Hivyo ni vema Serikali ipokee ushauri, mapendekezo na maazimio ya Kamati na kutekeleza mapema.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Spika, Watanzania tunaishi katika hali ngumu sana ya maisha. Ugumu huu wa maisha kama ulivyoelezwa katika taarifa ya Kamati umesababishwa na mfumuko mkubwa wa bei uliofikia asillimia 19.8 katika mwezi Desemba, 2011 na wala hauna dalili ya kushuka kwa siku za karibuni.

Mheshimiwa Spika, ingawa tunaelewa kuwa mfumuko huo wa bei kwa kiasi fulani umesababishwa na *factors* za nje yaani *imported inflation* kama vile kupanda kwa mara kwa mara kwa bei za mafuta na baadhi ya

vyakula vinavyoagizwa kutoka nje. Lakini sehemu kubwa unatokana na mambo ya ndani ambavyo ni vyakula, mchele, sukari, nyama na samaki.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanaweza kudhibitiwa kama Serikali itaamua na kujipanga vizuri. Mfano nchi yetu kujikita na kusimamia mikakati ya uzalishaji wa chakula cha kutosha ndani ya nchi kwa kutoa pembejeo za kilimo kwa wakati ikiwemo mbolea tofauti na hivi sasa ambapo mbolea inapelekwa kwa wakulima wakati muda umeshapita na kuwa hauna msaada wowote.

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani kutowafikia wakulima wote ni tatizo. Lakini pia Serikali ijaribu ili wananchi wapate afueni ya maisha wapunguze kodi katika bidhaa mbalimbali mfano sukari na hata mchele, na isitoshe tu kupunguza lakini ifuatilie kama punguzo hilo la kodi linaendana au linasababisha kupungua kwa bei za vyakula? Kwa sababu wapo wafanyabiashara wajanja wanaoweza kutumia fursa hii kwa faida yao yaani kujiongezea faida na bei zikaendelea kubakia juu.

Mheshimiwa Spika, inashangaza sana Tanzania tuna eneo kubwa la maji kwa bahari, mito na maziwa lakini samaki ni bei juu. Hii ina maana wavuvi tulionao hapa nchini hawana uwezo wa kuvua samaki wa kutosheleza mahitaji, iwe mahitaji ni makubwa na upatikanaji wa samaki ni mdogo kiasi ambacho bei ya kitoweo imekuwa ni kubwa mno. Serikali ijikite katika kusaidia sekta hii ikue kwani inaonekana Serikali imeisahau kabisa sekta ya uvuvi ambayo Watanzania wengi wanaitegemea katika kupata maisha yao na pia sekta hii kama ikiwekewa mikakati madhubuti inaweza ikawa sekta muhimu katika kukuza uchumi wa nchi yetu na wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwasaidie wavuvi wadogo kupata zana za kisasa za uvuvi, elimu ya uvuvi bora na kadhalika yanaweza yakasaidia sana kuongeza mavuno ya samaki na hatimaye bei ya samaki kupungua. Sekta ya uvuvi ipewe kipaumbele na wananchi wapewe elimu ya ufugaji wa samaki pia. Inashangaza pia Tanzania yenye ng'ombe wengi kuliko nchi nyingi za Afrika lakini nyama ya ng'ombe hainunuliki kwa kuwa na bei kubwa. Wanyonge wa nchi hii hawali nyama.

Mheshimiwa Spika, elimu itolewe kwa wafugaji wetu kuwa wanyama hawa watumike kuboresha maisha ya wafugaji na wananchi kwa jumla, kwa maana ya kuwa ng'ombe wanenepeshwe, wauzwe na wachinjwe ili watosheleze soko la ndani. Lakini cha msingi hapa ni kuanzisha viwanda vya nyama, kusindika nyama ili wafugaji wawe na uhakika wa soko.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kupunguza mfumuko wa bei wa vyakula kama Serikali itakuwa na dhamira ya kweli ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, yapo masikitiko kwa wananchi wengi kwamba Serikali inaeleza kuwa uchumi unakuwa lakini ukuaji huo wa uchumi hauendani na upunguzaji wa kiwango cha umaskini wa Watanzania walio wengi. Taarifa imeeleza kwamba sekta zinazosababisha uchumi kukua sio zile zinazowagusa wananchi walio wengi moja kwa moja, mfano, sekta ya kilimo (wananchi wengi wanategemea sekta hii) hadi sasa dhana ya kilimo kwanza ni nyimbo tu ingawa malengo yake ni mazuri, uwezeshwaji wa wananchi katika sekta hii ni mdogo sana. Mifuko ya uwezeshaji inawafaidisha watu wa mijini zaidi, fursa nyingi za mikopo na elimu zipo mijini tu, umeme vijiji bado kabisa, barabara za vijiji henzieleweki, hivyo basi umaskini kwa watu wa vijiji ni vigumu kuondoka. Serikali iongeze bajeti ya kilimo kwa maana ya kuhakikisha wakulima na wengine waishio vijiji wananaufaika ili wao waone na wahisi kuwa kweli uchumi wa nchi unakua na maendeleo ya nchi yao yamewafikia hata wao.

Mheshimiwa Spika, viwanda ni sekta muhimu katika maendeleo ya nchi. Kwa maana ya kwamba ajira ndani ya nchi itaongezeka hasa kwa kuwa tunaelewa tatizo la ajira ni kubwa ndani ya nchi yetu. Aidha, wakulima watapata soko kwa mazao yao hasa yale yanayotumika kama malighafi za viwandani.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba Watanzania tumebakia wanyoge ilhali ni matajiri, tunasababisha wenyewe kunyonywa na kuendelea kunyonywa na nchi za kibepari. Mfano hai mazao ya korosho tunauza bila ya kubanguliwa anayefaidi ni nchi tunazowauzia na wao wanaongeza thamani kwa kuzibangua na kuzitengeneza na kumfikishia mlaji.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kusindika samaki havipo, tunauza samaki kama walivyo, nchi nyingine ndio zinazofaidika Tanzania bado inabaki maskini.

Mheshimiwa Spika, tubadilike, tufanye kila linalowezekana tujenge viwanda vingi ndani ya nchi yetu. Sekta binafsi isaidiwe ikue na iwe na uwezo wa kufanya mambo kama haya hasa ya ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi katika nchi yetu imedorora tofauti na nchi nyingine. Tumepata taarifa kuwa katika Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) kuna dirisha la kutoa mikopo kwa wawekezaji/wafanyabiashara wa sekta binafsi lakini Watanzania

hawajitokezi kabisa kuchukua mikopo hii, hivyo mikopo inachukuliwa na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali ibebe jukumu la kuhamasisha sekta hii itumie fursa hizi kwani watakaonufaika ni Watanzania wa nchi hii sio wengineo.

Mheshimiwa Spika, sekta nyingine ambayo itaweza kuchangia uchumi wa nchi hii kwa kiasi kikubwa ni sekta ya utalii. Watanzania tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa na vivutio vingi tu vya utalii vivutio ambayo tumevikuta tu Mungu ametutengenezea na nchi yetu kupitia Serikali yake ni kutumia maarifa tu na kuweza kuvuna matunda yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali hadi sasa haijaweza kuvitangaza vivutio hivi kiasi cha kuridhisha huko duniani. Hivyo ni watalii wachache tu ndio wanafika nchini kwetu. Pia miundombinu na vifaa vinavyosaidia kutembeza watalii viboreshwe ili wanapokuja wasisumbuke.

Mheshimiwa Spika, utitiri wa kodi katika sekta hii upunguzwe ili iweze ku-compete na nchi nyingine. Hivi sasa sekta hii imewekewa kodi nyingi sana kiasi kwamba inakuwa ni vigumu kuwapata watalii wengi kutokana na mali hiyo watalii wanakimbilia nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ikiwekewa mikakati madhubuti inaweza ikatoa ajira kwa vijana na kuongeza mapato ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaipongeza *TRA* kwa kazi nzuri inayofanya hata hivyo uwezekano wa kuongeza mapato upo, iendelee kufanya utafiti wa maeneo mapya ya vianzio vya mapato, sekta ambayo sio rasmi ifanyiwe kazi ipasavyo.

Aidha, vianzio visivyo vya kodi visimamiwe na vifuatiliwe vizuri. Serikali nzima kwa maana ya Wizara zote na Mawaziri wote wawe na msimamo mmoja katika ukusanyaji wa mapato hasa yasiyo ya kodi yanayohusiana na Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Kamati. Ahsante sana.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi zangu kwa Kamati ya Nishati na Madini kwa taarifa, maoni na mapendekezo mazuri. Maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii kwa Wizara ya Nishati na Madini pamoja na *TANESCO* wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake ukurasa wa nne, Kamati imetamka wazi kwamba tatizo la upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo mbalimbali hapa nchini bado lipo, aidha, kutohana kuharibika mara kwa mara kwa miundombinu yake kama vile *transformers* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana Wizara ya Nishati na Madini iwe *serious* katika utekelezaji wa majukumu yake. Mambo mengine ni ya wazi na matatizo mengine yanayojitokeza yanashindwa kufanyiwa kazi kwa wakati na hivyo kusababisha ukosefu wa umeme wa uhakika kwa wananchi. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba kuna sababu nyingine za msingi na kuna sababu nyingine siyo za msingi za kuwafanya wananchi kukosa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili Wizara ya Nishati na Madini na ndugu zetu wa TANESCO ningewaomba sana waongeze *efficiency* katika utekelezaji wa majukumu yao. Masuala mengine ni madogo madogo lakini yanashindwa kufanyiwa kazi bila sababu za msingi na hivyo kusababisha ukosefu wa umeme kwa wananchi mfano wa hayo ni ukosefu wa mafuta ya *diesel* kwa ajili ya jenereta pamoja na vipuri au *spare* za jenerata zilizoharibika.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Liwale, suala la ukosefu wa umeme wa uhakika sasa limekuwa ni la muda mrefu sana na mara nyingi tumejikuta tunakuwa waathirika, aidha, umeme haupo kwa sababu ya *diesel* ya kuendeshea jenereta haijaletwa au umeme hakuna kwa sababu jenerata ni mbovu na *spare* haijaletwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa takribani miezi sita wananchi wa Liwale wapo katika shida ya umeme nimeshatoa taarifa kwa wahusika wa TANESCO si chini ya mara tano, ninajibowi kwamba *spare* ya jenerata imeagizwa na hapa ndipo tatizo lilipo. Hapa ndipo ndugu zangu wa TANESCO wanapoonesha kutokuwa *responsible*.

Mheshimiwa Spika, *spare* ndogo tu ambayo inaweza ikaagizwa kutoka Ulaya na ikatumwa kwa *DHL* ama *FedEx Courier* ikaletwa ndani ya wiki tatu hadi nne sasa inachukua miezi sita ni kwa nini? *Spare* hiyo inakuja na meli au inatoka wapi? Hata kwa mtu wa kawaida asiyejua lolote hawezি kuelewa.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya *diesel* ya kuendesha jenerata yanapokwisha huchukuliwa wiki mbili kuletwa mafuta hayo wakati huo umeme hakuna sababu mafuta hayajaja ni kwa nini! Ndugu zangu wa TANESCO wenzenu wananchi wa Liwale mnatuangusha, hospitali ya

Wilaya, *maternity ward* wakunga wanalazimika kutumia taa za chemli enzi hizi kweli!

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengi hapa Tanzania ambayo Wizara ya Nishati na madini ikijipanga na kuwa *responsible* tatizo la ukosefu wa umeme wa uhakika litahusisha moja ya maeneo hayo ni Liwale.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa umeme wa *Songos* ukasambazwa kutoka Nangurukuru, Njinjo, Miguruwe, Zinga, Kimambi, Kichonda hadi Liwale na inawezekana pia umeme wa *Mnazi Bay*, ukasambazwa kutoka Ruangwa, Mnero Lionja, Nangano Kibutuka, Kiangara hadi Liwale, Wizara ya Nishati wawe *responsible* na watimize majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale ikipatiwa umeme wa Gridi wa Taifa Serikali itapunguza sana gharama za *diesel* ambayo kwa sasa si chini ya lita 35,000 kila mwezi zinatakiwa kupelekwa Liwale kwa ajili ya jenerata, Wilaya ambayo iko kwenye Mkao unaozalisha umeme wa kutosha kutoka *Songas*, je, kwa mwaka mzima zinatumika shilingi ngapi kwa ajili ya kununua *diesel*? Je, kama umeme wa Gridi ya Taifa ukifikishwa Wilaya ya Liwale Serikali ita-serve kiasi gani? Wizara ya Nishati na Madini mfanye mahesabu hayo na muone hasara ambazo Taifa inazipata bila sababu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mungu kwa afya na uhai, nikushukuru wewe mwenyewe kwa nafasi uliyonipa ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nitachangia Wizara zote nne nikianza na Wizara ya Nishati na Madini, ni rai yangu na napenda kuishukuru Wizara kwa juhudzi zake za kusambaza umeme nchi nzima hususan Mkao wa Rukwa. Pia napenda kukumbushia kuwa Rukwa haijapata umeme wa kutosha na kwamba umeme huo mchache wa jenereta hautaufanya Mkao wa Rukwa kuendelea kama ilivyo mikoa iliyo na umeme wa Gridi ya Taifa. Hivyo basi naikumbusha na kuiomba Serikali iwapatie wana Rukwa umeme wa Gridi ya Taifa na kama Serikali ina mpango huo basi iharakishe ili na sisi Rukwa tujenge viwanda vya kuchimba madini, kusindika mafuta ya alizeti, kusindika unga wa kuisambazia nchi yote na kusindika samaki wa Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika na mengine mengi kwa wajasiriamali wadogo wadogo. Rukwa tunahitaji maendeleo.

21 APRIL, 2012

Kuhusu miundombinu, Rukwa tunashukuru kwa ajili ya barabara zinazojengwa MCC lakini na zile za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna hali ya kutisha kuwa mwanzo barabara zilitia matumaini lakini hivi sasa ujenzi wa barabara hizo umesimama na magari, magreda na *plants* nyagine zimesimama tu ni hatari vitendea kazi hivi vinaliwa na kutu vitakufa lakini basi tunaomba Serikali ijitahidi kumaliza barabara hizi Tunduma – Sumbawanga – Sumbawanga – Sumbawanga - Kasanga, Sumbawanga – Mpanda. Barabara ziishe kulingana na muda uliopangwa kwenye mikataba. Barabara zikiisha Rukwa tutaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, vijiji vya mwambao ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa vimevamiwa na wahamiaji haramu kutoka DRC na Burundi, uvamizi huo ni mkubwa kwa kiwango cha kusababisha ufinyu (*acute shortage*) wa huduma za jamii kama vile afya, shule, dawa zinakuwa zimekadiriwa kwa wazawa basi zote zinaishia kwa wavamizi hawa na wanasababisha vurugu, mapigano na vifo. Tunaomba Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Fedha ndiyo Wizara mama inayo-determine uhai wa maendeleo ya Serikali. Nchi ina mipango mizuri ya maendeleo, Bunge hupitisha bajeti ilioandaliwa na Wizara kutokana na mipango ya Halmashauri ambayo ndiyo mipango ya wananchi (*O and OD*), sasa basi Wizara ya Fedha inapokuwa inachelewesha *funds disbursement* kwa Wizara na Idara mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, lakini pale Wizara inapoamua kutoa/ku-release *funds* huchelewa mno, fedha hazitolewi kama inavyopangwa kwenye mipango hii na inasababisha utekelezaji wa zimamoto, hii haina ufanisi na inapelekea umaskini wa nchi yetu ya Tanzania. Naunga mkono hoja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu nishati. Mikoa husika imebahatika kuwa na gesi, mafuta na *gypsum* huko Mtwara na Lindi. Tunaiomba Serikali iwaandae watu wa Mtwara na Lindi kwa kuwawezesha katika kilimo, ujenzi, ufugaji, uzalishaji wa samaki ili kuwaweka tayari katika kujandaa kwa kuhudumia watu wengi watakaokuja katika uwezeshaji wa viwanda mbalimbali.

Kwa vile gesi ipo Mtwara na Lindi tunaomba basi vijiji ambavyo vipo barabarani ambapo bomba la gesi linapita kwenda Dar es Salaam wapatiwe umeme. Bado kuna vijiji havijapata umeme.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafuta na gesi iliyogundulika katika mikoa ya Kusini, sasa kumeibuka watu kuomba viwanja vya ardhi Kusini na ofisi ya madini wanaonekana kutoa vibali viwanja hivyo na wanatoa maeneo makubwa makubwa hivyo kusababisha ugomvi na wananchi mfano huko Ruangwa kijiji cha Nachilungo kuna mwekezaji mmoja amepewa ardhi kubwa sana na kufanya wanakijiji wakose ardhi. Kwa hiyo, ushauri wangu kuwa wawekezaji wanaotaka ardhi kuwa wawekezaji wanaotaka ardhi kwa ajili ya gesi au mafuta wapewe kiwango fulani cha ardhi na sio sehemu kubwa sana kama ilivyotokea huko.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali iingilie kati mgogoro huo wa ardhi Ruangwa kijiji cha Nachilungo kwani habari kamili ninayo.

Kuhusu uchumi, Tanzania tuna vitu vingi vya kuweza kuzalisha mali na sisi kama Watanzania hatungekuwa na matatizo ya uchumi ulio nyuma. Tuna madini mengi, makaa ya mawe, bahari na utalii ulio mkubwa lakini hatutumii fursa hizo katika utalii kama kuna yule *Dinosaur* (mjusi) aliyekuwa Ujerumani ambaye amezalisha pesa kwa ajili ya Ujerumani, sisi wenyewe Tanzania hasa Lindi alikotoka mjusi huyo hakuna tunachopata. Tunashauri na sisi Tanzania tupate mrahaba kutokana na mjusi huyo ambaye ananufaisha Ujerumani tu.

Mwisho barabara ya Mingoyo - Kibiti au Kibiti - Lindi. Barabara hii imeanza kujengwa miaka mingi lakini mpaka leo haijaisha kujengwa. Tunaiomba Serikali sasa itoe kauli hiyo barabara itaisha lini?

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Lindi tunaomba ikarabatiwe ili wananchi wa Lindi wapate ajira, tuhurumieni mikoa ya pembezoni.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na tatizo la umeme. Pamoja na kuwa matatizo makubwa ya umeme bado Shirika letu la TANESCO lipo kwenye matatizo makubwa ya kifedha. Mpaka sasa hivi Shirika hili linadaiwa shilingi bilioini 296.8 na nyingi ya fedha hizi ni *capacity charges*. Kwa nini tusiweze kutimiza Maazimio ya Bunge ya kutaka kuwepo na umeme wa uhakika kwa kununua mitambo yetu wenyewe?

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi katika Wizara ya Nishati na Madini wawekezaji wengi wameanza kuchimba gesi, hivi hawa wachimbaji wa gesi wanatumia sheria ipi? Tusipokuwa waangalifu itakuwa kama kwenye sekta ya madini ambayo Watanzania hatufaidiki kabisa na faida ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilete sheria ya gesi mara moja ili iweze kutusaidia Watanzania ikiwa ni pamoja na matumizi ya nyumbani ambayo itasaidia kutunza mazingira yetu badala ya kukata miti kwa ajili ya mkaa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa nguvu zangu zote nakataa kabisa uchimbaji wa *uranium*, bado hatujaweza ku-manage yaliyopo tunakimbilia kuchimba mionzi mibaya sana kwenye madini haya. Dar es Salaam kuna viwanda katika kata ya Kawe, viwanda vile vinapeleka maji yenye sumu kwenye mfereji wa Mlalakuwa na pale Mikocheni. Serikali imeshindwa kabisa kusimamia suala hili. Je, ni kwa jinsi gani wataweza kusimamia uchimbaji wa *uranium*.

Mheshimiwa Spika, ni lini makampuni yanayochimba madini yataanza kulipa mrabaha kama sheria mpya ya madini ya mwaka 2010 inavyosema?

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme mkoa wa Kilimanjaro kwa masikitiko makubwa wajumbe wengi wamechangia na wanasema Kilimanjaro kuna umeme mpaka majumbani. Ule umeme unaonekana kule ni sawa na nyumba zisizokuwa na umeme sababu hauna nguvu kabisa ni lazima watu wawashe mishumaa. Je, kwa mtazamo huu utasema kuna umeme Kilimanjaro wakati hauwaki?

Mheshimiwa Spika, ni lini tutapata umeme wa uhakika katika mkoa wa Kilimanjaro badala ya huu mfano wa umeme wa urembo usiowaka?

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia suala la ukuaji wa Pato la Taifa. Wakati takwimu zikiituambia kuwa Pato la Taifa limekuwa likikua (7.0% mwaka 2010 na 6.0% mwaka 2011). Hali hii ya ukuaji wa Pato la Taifa haijitalfsiri katika kuondoa umaskini kwani hali ya ugumu wa maisha imezidi kuwaelemea wananchi siku hadi siku na bila matumaini yoyote.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Pato la Taifa umeshindwa kuondoa umaskini kwani unachangiwa na sekta ambazo haziojiri watu wengi, mfano, sekta ya huduma 8%, viwanda na ujenzi 8.7% ilhalii sekta ya kilimo inayoajiri takribani 84% ya Watanzania ikichangia 4% tu katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali na sera ya Kilimo Kwanza. Wakati Serikali ikijinasibu na sera ya Kilimo Kwanza, utekelezaji wa vitendo wa sera hii haupo kwani ukuaji wa sekta ya kilimo umepungua hadi 3.6% mwaka 2011 kutoka 4.2% mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo ya ukame na nishati tuliyonayo, utendaji mbovu na kutokuwa na vipaumbele kumechangia kwa kiasi kikubwa kudorora kwa sekta ya kilimo. Pembejeo za kilimo zimekuwa zikichelewa kuwafikia wakulima na tena bei zake zimekuwa za juu kuliko ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kuona kuwa Serikali kwa miaka yote imeshindwa kutafuta wawekezaji katika sekta ya usindikaji wa mazao ya kilimo kama vile matunda ambayo yana soko kubwa, lakini tunaagiza maji ya matunda toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu wanalima alizeti hasa Mkoa wa Singida pamoja na mazao mengine ya kusindika mafuta ya kula. Naishauri Serikali itafute wawekezaji katika kusindika mafuta ya kula ili kuinua kipato cha wakulima na hatimaye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali inatuambia kuwa katika nusu ya kwanza ya mwaka 2011/2012 *TRA* waliweza kukusanya mapato ya kodi kwa 101.4% na matumizi ya Serikali katika kipindi hicho yalikuwa 87.7%. Cha kushangaza ni kwamba ikiwa *TRA* walivuka kiwango cha kukusanya kodi kiasi hicho, ni kwa nini basi fedha za miradi ya maendeleo hazikupelekwa kwa wakati hususan katika Halmashauri nyingi nchini? Matumizi haya ya 87.7% yaliyelezwa wapi?

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Hesabu za Serikali imetuambia kuwa takriban shilingi trilioni 1.3 zilitumika kwa matumizi yaliyokuwa nje ya bajeti tena bila kupata idhini ya Bunge liliopitisha bajeti husika na bila hata kuitaarifu Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambayo kimsingi ndiyo msimamizi mkuu wa bajeti ya Serikali. Hii ni dharau kwa Bunge lako Tukufu na wananchi tunaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, wigo wa kodi umeendelea kuwa finyu kwa kufuata vyanzo hivyo vya miaka yote. Inashangaza kuona kuwa makampuni makubwa ya simu hayalipi kodi Serikalini ilhali gharama za simu kwa watumiaji ni kubwa sana.

21 APRIL, 2012

Mheshimiwa Spika, sekta isiyo rasmi ambayo ingechangia kuongeza Pato la Taifa imeachwa bila utaratibu maalum wa utambuzi na uendeshajji na hivyo mchango wake halisi kutokuonekana.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi imeendelea kuwa tatizo sugu pamoja na Kamati kuishauri Serikali kupunguza misamaha ya kodi na kufikia 1% kutoka 2.3% ya Pato la Taifa. Nchi zote Afrika Mashariki zinaruhusu misamaha ya kodi ya 1% tu. Cha kushangaza ni kwamba misamaha hii inatolewa kwa mashirika au makampuni ambayo yana uwezo wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ubadhirifu wa fedha za umma ni wa kutisha kama ambavyo ripoti ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alivyoainisha. Naitaka Serikali ichukue hatua mara moja dhidi ya wote waliohusishwa na ubadhirifu huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nazipongeza Kamati zote kwa taarifa nzuri walizowasilisha hususan Kamati yangu ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Daktari Kigoda.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono mapendekezo yote ya Kamati. Ninaomba kuwasilisha.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kinanishangaza ni viwanja vya madini vinavyotolewa ovyo na Maofisa wa Makao Makuu, kwa kutumia Ramani wakiwa wamekaa maofisini bila kufika site. Elimu kwa Watanzania ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa Watanzania, madini yalikuwa ni urithi waliopewa na Mwenyezi Mungu, lakini wenyewe uchu na pesa wamegawa urithi wetu ovyo kwa watu ambao ni wanyang'anyi na waporaji wa mali zetu. Watoaji hao na waporaji hao hawana huruma na sasa hivi wameanza kuingilia sehemu za mbuga za wanyama eti kuna madini ya *uranium*. Hili jambo kwangu ninaishangaa Serikali hii!

Mheshimiwa Spika, historia itajirudia na utumwa utakaotupata utazidi ule wa Afrika ya Kusini huko mbele wanetu wanakokwenda.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatupeleka pabaya kwani Biblia inasema, maskini hata alichonacho atanyang'anywa. Pia Biblia hiyo inasema, watu wenyewe akili, akili zao zitapotea na ufahamu wa wenyewe busara utafichwa wala hawatajua kinachoujia ulimwengu. Si hivyo tu, Kitabu hiki Kitakatifu kinasema, nchi nydingi zitapinduliwa na wakushi tutafyata nyoyo zake.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii inaendelea kutupeleka pabaya; hivi hawa wanaotuhujumu wakishirikiana na wageni hata wakipewa mali ya dunia dunia yote watafaidika nini?

Mheshimiwa Spika, wahujumu hao waelewe siku za mwisho au siku ya kiyama fedha hizo walizojitwalia kwa njia ya kudhulamu wanyonge zitakuwa kitanzi kwao na wala hazitawaokoa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Nishati na Madini iwachunguze sana Wazungu wanaokwenda Mkoa wa Rukwa hasa Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Spika, shida kubwa ni maovu yetu, matendo yetu, ambayo yametufanya tumsahau Mola wetu na tumegeuka kuwa kama wanyama ndiyo maana laana hizi zinatupata.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Kifungu cha 3.3.1(v), ili tuyafanye Madini ya Vito ya *Tanzanite* kuwa Nembo (Alama) ya Taifa la Tanzania ni budi tuyatangaze kuwa madini maalum na Alama ya Taifa letu. Madini haya yanapatikana nchini Tanzania tu. Tunayo haki na uwezo wa kuyatunza na kuyachimba kwa ufahari wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kufanya hivyo, tunahitaji kuyatungia Sheria na Kanuni Maalum zinazoyazuia kumilikiwa na mtu mwingine ye yeyote isipokuwa Serikali. Serikali pekee ndiyo iwe mchimbaji na mfanyakishara wa madini haya (*STAMICO*), kwa kushirikiana na wawekezaji wakubwa wenye mitaji na teknolojia, endapo STAMICO itashindwa kupata mtaji hapa hapa nchini, ichimbe madini haya. Katika kutayarisha Kanuni za *Tanzanite* tunaweza kuiga Kanuni za Almasi zilivyokuwa zamani kwamba, almasi ilikuwa Nyara ya Taifa.

Tukifanya hivi tutaweza ku-account each and every stone (mineral) na kujipatia pato kubwa sana. Kwa sasa Madini ya *Tanzanite* mengi yanatoroshwa na Serikali tunapata manufaa kidogo licha ya kuwa madini hayo yanapatikana Tanzania tu.

Kifungu cha 1.1.1 kinazungumzia kuhusu Wakala wa Ukaguzi Madini (*TMAA*). Wakala huu ulianzishwa kisiasa baada ya Alex Stewart kuondolewa nchini kwa vile Kampuni hiyo ilikuwa inatumia fedha nyingi sana.

Lengo la msingi la TMAA ni kukagua uwekezaji katika migodi ili kuhakikisha hakuna udanganyifu. Makampuni makubwa ya madini yanao uzoefu mkubwa sana katika kudanganya uwekezaji wake ili kupata faida kubwa.

Kazi hii ya kukagua uwekezaji inafanana sana na kazi ya TRA ya kukagua uwekezaji ili kuona kama kampuni inapata faida na kulipa kodi. Kuna mwingilio mkubwa sana wa kazi kati ya TRA na TMAA kiasi cha kuonekana kuwa migodi inakaguliwa mara mbili. Kutokana na sababu hiyo, TMAA inajikuta inafanya kazi pia za kukagua mazingira, mrabaha na uchimbaji mdogo, kazi zinazofanywa na NEMC na Idara ya Madini. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa kuunda Wakala kubwa inayofanya kazi za taasisi zingine.

Mapendekezo ya awali yalikuwa kwamba, TMAA iwe Idara ya TRA ikiongozwa na Kamishna chini ya Kamishna Mkuu wa TRA ili kazi zote za TRA za kukagua uwekezaji wa migodi zifanywe na TMAA hiyo mpya na shughuli zingine za ukaguzi wa migodi ziachiwe Idara ya Madini chini ya Mkaguzi Mkuu wa Migodi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya kama ilivyoonekana kwenye taarifa yao. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pia kwamba, TANESCO kama Shirika limeshindwa kabisa kusimamia nishati ya umeme. Hatuna namna wala lugha nyingine ya kuendelea kuwa na matumaini na Shirika. Kwanza, lina wafanyakazi wengi kupita uzalishaji hivyo kama tutafuatilia mapato ya TANESCO tutoe na matumizi mbalimbali na mishahara ni wazi kwamba, huenda matumizi yakazidi mapato. Matokeo yake, wananchi wanaotumia nishati hii wanabebeshwa mzigo mkubwa kwa kupandishwa gharama kila mara ili kufidia. Nashauri Shirika la TANESCO lifanyiwe uchunguzi ili kubaini watumishi ambao siyo lazima kuwepo. Mbaya zaidi, watumishi wengi wameajiriwa kindugu, kama yupo baba basi utakuta wajomba na watoto wamo humo.

Ikumbukwe pia kuwa, umeme siyo anasa bali ni bidhaa muhimu kwa maendeleo ya wananchi Wilayani Mbarali. Wananchi wa Vijiji vya Ilongo, Uturo, Ukwavila, Igalaiko na Sonyanga vimepititiwa na nguzo za umeme kando ya Barabara Kuu ya Dar es Salaam – Tunduma – Mbeya. Wao wamekuwa watazamaji na walinzi wa nguzo za umeme bila wao kunufaika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipotembelea Kata ya Madibira kwenye mashamba makubwa ya mpunga, alishangaa kuona kinu kikubwa cha kukoboa mpunga kipo lakini hakifanyi kazi kutokana na ukosefu wa umeme akatoa ahadi kwamba utaletwa Madibira lakini hadi leo umeme haujapelekwa. Umeme ungesaidia wananchi kuuza mchele kwa faida kubwa badala ya kuuza mpunga. Kuendelea kupewa ahadi bila mafanikio ni kuwakatisha tamaa wananchi ambaa wanalima kila mwaka bila mfanikio.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua hivi ni kwa nini ghamara ya kuunganisha umeme ipo juu sana; ukiunganisha kwa nguzo tatu siyo chini ya shillingi milioni tatu na zaidi; katika hali hii wananchi wenyе kipato kidogo watamudu? Kwa nini bei za nguzo za umeme ni kubwa sana na hali nguzo hizo zinazalishwa hapa hapa nchini? Nashauri ufanyike uchunguzi kuona ukweli wa bei za nguzo za umeme.

Umeme Vijijini; REA isiwe kwa baadhi ya wilaya, wilaya zote zиже mpango mzima na utaratibu wa REA. Nasikitika pia kuona mpango huu haujafika Wilaya ya Mbarali ambayo nimekuwa nikiiombea iingie kwenye mpango. Ninasisitiza pia kuwa Mbarali iingizwe. Sekta ya Madini ni nyeti sana kwa Uchumi wa Taifa, lakini lipo tatizo kwenye mikataba inayofanywa kati ya wawekezaji na Serikali haina tija kwenye Pato la Taifa. Ninashauri mikataba yote ipitiwe kwa faida na manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Yusuph Makamba (Mb) na Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri iliyofanywa kwa kpindi cha mwaka mzima, kuishauri Serikali mambo mbalimbali ambayo yatasaidia kuboresha utendaji wa Wizara kwa lengo la kuinua uchumi kuititia Sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa, Serikali itafuata ushauri wa Kamati ili kuondoa kero mbalimbali za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya utekelezaji wa umeme wa dharura, wananchi walitegemea kabisa suala la mgawo litakuwa limemalizika, lakini bado tatizo la umeme kukatikakatika lipo kwa sababu ya miundombinu ambayo imechakaa kwa kiwango kikubwa. Hivyo basi, ninaiomba Serikali iliondoe tatizo hili mapema kuititia Bajeti ya 2012/2013,

21 APRIL, 2012

kwa kutenga fedha za kutosha kukarabati miundombinu ya umeme ili kuondoa adha inayowapata watumiaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Wajumbe wa Kamati na Wabunge wote waliochangia Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuwa, Serikali ilazimike kulinusuru Shirika la TANESCO kifedha ili liweze kuijendesha, ukizingatia wazabuni wengine sasa wanasihamisha Mikataba. Tatizo hili limetokana na TANESCO kukabiliwa na tatizo la miundombinu mibovu na lazima ikarabatiwe.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika transfoma nyingi hazina ubora kwani hulipuka mara kwa mara; hivyo ni vyema sasa iagize transfoma zenyé ubora. Hii itasaidia sana kupunguza adha ya wananchi kukosa umeme kila wakati hususan kwenye miji mikubwa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa kabla ya utekelezaji wa Serikali kusaini Mikataba ya Madini; mfano, Madini ya Urani ni muhimu elimu itolewe kwa wananchi kwa njia mbalimbali; mfano, televisheni, magazeti, redio, vipeperushi na kadhalika. Hii itaondoa kabisa migogoro kati ya wawekezaji na wananchi. Vilevile itasaidia wananchi kuwa na uelewa ili kujikinga na madhara yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, inakatisha tamaa sana rasilimali za nchi zinapochukuliwa na Wawekezaji na Serikali bila kutoa mrabaha kwa wananchi wa maeneo husika. Ninashauri Mikataba itakayowekwa sasa iweke wazi suala la mrabaha. Mfano, Mradi wa Umeme wa Upepo Singida, suala la mrabaha lazima liwe wazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono Taarifa ya Kamati kwa asilimia mia kwa mia, nikitegemea Serikali itazingatia ushauri huu, ushauri wa Kamati na ushauri wa Wabunge kwa ujumla.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja na kuipongeza Kamati kwa kazi nzuri na mapendekezo iliyotoa kwa ujumla wake.

Naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kuhusu mapendekezo ya usambazaji wa umeme vijiji (REA). Nia hii njema, kwa masikitiko makubwa ni jinsi ambavyo mgawanyo wa mapato haya hauzingatii uwiano na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, napata tabu sana hapa Bungeni wakati Waheshimiwa Wabunge wanaposimama na kuhoji juu ya baadhi ya vijiji

21 APRIL, 2012

vyao kutounganishiwa umeme wakati mimi Wilaya yote ya Kalambo, yenye jumla ya Kata 17, hakuna umeme hata Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uhalisia juu ya mahitaji ya umeme, Makao Makuu ya Wilaya iliyopo Matai, haina umeme. Kata ya Kasanga iliyopo Mwambao wa Ziwa Tanganyika kuna upanuzi wa bandari na pia ujenzi wa Soko la Kimataifa la Samaki lakini kwa bahati mbaya sana umeme wa shughuli zote hizi unakosekana, kama alivyoshuhudia Mheshimiwa Makamu wa Rais na kuahidi kulipatia ufumbuzi suala hili.

Pili, gharama za uunganishaji wa umeme ni kubwa na kuwaathiri wananchi ambao wapo tayari kuunganishiwa umeme lakini huduma hii haijafikishwa na Serikali na hivyo imekuwa kama adhabu kwa mwananchi kwa kosa ambalo siyo lake. Napendekeza gharama ya kuunisha umeme ipunguzwe na iwe *fixed* kwani hakuna sababu ya msingi kwa mwananchi kulipia gharama kubwa kuunganishiwa umeme.

Tatu, kukatika kwa umeme kunakotokana na kuharibika kwa transfoma. Tuna bahati ya kuwa na kiwanda cha kutengeneza transfoma nchini kwetu, ni vizuri tukatumia fursa hii.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Ngorongoro, napenda niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuipatia umeme Wilaya ya Ngorongoro (Loliondo), baada ya Miaka 50 ya Uhuru wa nchi yetu. Tumechelewa lakini tumepata.

TANESCO katika mipango yake ya kupeleka umeme katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Ngorongoro, ilikuwa tupate umeme mwaka 2015, Makao Makuu ya Wilaya.

Ingawa umeme wa Ngorongoro/Loliondo ni wa jenereta, naomba yafuatayo kwa Serikali ya Awamu ya Nne:-

Kwanza, nguzo za kusambazia umeme ni chache mno, zipelekwe za kutosha kwa ajili ya Mji wa Wasso na Loliondo.

Pili, maeneo mengi ya wananchi umeme haujafika.

Tatu, naleta ombi maalum kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini la kuongezewa muda wa kulipia umeme kwa bei nafuu ya shilingi 75,000 badala ya shilingi 400,000 na zaidi.

Wananchi wengi hawakuweza kutumia *offer* ya kwanza kutohukua na nguzo kuchelewa na wananchi wengi kutofikiwa na TANESCO wakati wa kusambaza umeme (*area of distribution*).

MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO: Pamoja na Taarifa ya Kamati na michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, nina mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Hatua za makusudi zichukuliwe kuhakikisha kuwa tatizo la umeme nchini na hasa kukatikakatika ovyo bila utaratibu ni vizuri likapatiwa suluhu ya kutosha.

Umeme una mchango mkubwa sana kwa maendeleo ya nchi; ikitokea unakatika ni vyema taarifa ikatolewa mapema ili wananchi husika wazime umeme kwenye nyumba zao na maeneo mengine ili kuepuka hasara ambayo inaweza kutokea.

Mfumo wa uingizaji mafuta kwa wingi (*Bulk Procurement System*) ni mzuri, ambao ulitarajiwu kupunguza uhaba wa mafuta nchini. Hata hivyo, kutohukua na changamoto zilizopatikana ni vyema Serikali ikachukua hatua za makusudi kama ilivyoshauri Kamati ya Nishati na Madini. Ninaamini ushauri uliotolewa ukifuatwa, utasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha utaratibu huu.

Serikali ichukue juhudhi za makusudi kuiongezea uwezo *REA* ili iweze kusambaza umeme vijijini kwa kasi zaidi. Jamii pia inaweza ikahusishwa katika kuchangia *REA*. Mfano, kuwepo na kiasi fulani cha pesa ambacho kwa kila mtu mwenye simu atakatwa na kupelekwa *REA* ili pesa hiyo itumike kuongeza kasi ya kupeleka umeme vijijini.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua ya kuboresha noti zake kwa sababu zinachakaa haraka sana kuliko zile za zamani.

Mheshimiwa Spika, Serikali iharakishe mchakato wa ufunguaji wa mabenki maeneo yote yaliyoanzishwa Wilaya Mpya. Kwa mfano, Wilaya Mpya ya Itilima, Mkoani Simiyu. Ahsante.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, nitaanza kuzungumzia kuhusu ukusanyaji wa mapato. *TRA* imesema kuwa, imeshindwa kufikia malengo, lakini nasema kuwa, hawatafikia malengo ya ukusanyaji wa mapato hadi kiyama.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wasio waaminifu wa *TRA* wanashirikiana na makampuni ya Wakala wa Forodha, wanaitia Serikali hasara kwa kutoa hasa makontena ya nguo, *spear parts*, vifaa vya ujenzi na kadhalika kwa bei ndogo sana. Lakini muagizaji wa mzigo huo hutozwa pesa nyingi. Kontena la nguo la dola laki moja, kulipiwa ushuru wa laki tano za Tanzania, wakati huyo mmiliki hulipa milioni 40 au zaidi za Tanzania. Lakini kwenye mapato ya *TRA* huingia shilingi milioni tano; milioni 35 hugawana Mtendaji wa *TRA* na Wakala wa Forodha.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ni kweli na ninaomba ifanyiwe kazi na nipewe jawabu la kuridhisha. Na ninaomba unijibu hii leo kwamba, taarifa yangu utaifanya kazi, ikiwa nitapata kuzungumza hii leo nitaizungumza, lakini kama sijapata kuzungumza leo nakuomba ipokee hii taarifa na unijibu kuwa utaifanya kazi. Usipate tabu sana, nakuomba ufuatilie mizigo iliyointia kuanzia Januari mpaka Aprili, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato *TRA*, moja ya Taasisi ya Umma, ulioshindwa kufikia malengo, *TRA*, *TPA* na kadhalika, ukiangalia kwa makini Bandari ndio uso wa nchi yetu na Bandari inafanya kazi sana. Je, iweje *TPA* ishindwe kufikia malengo? Kwa kuwa, *TPA* wanawapa umuhimu zaidi hawa watu wa Bandari kavu kwa kuwa, Viongozi wana mkono wao (*share* yao).

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haijengi Bandari Kavu yenyewe na ikawa inakusanya mapato? Iweje Serikali inao uwezo wa kukusanya mapato yenyewe, kuwaachia Bandari Kavu kukusanya mapato? Nakuomba Mheshimiwa Waziri, unijibu kuwa, mko tayari kujenga bandari kavu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa taarifa hii. Napenda kuunga mkono taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwani imegusa *almost* kila eneo. Katika kuchangia nitagusa maeneo machache.

Kwanza, mfumuko wa bei ambao unachangiwa pia na kupanda kwa bei za vyakula. Hili linaweza kudhibitiwa na Serikali. Usambazaji wa chakula umekuwa wa tabu sana kutoka mikoa inayozalisha chakula kwa wingi. Serikali inaweza kurekebisha miundombinu ili magari yaweze kupita kwenda kuchukua chakula, kama vile mahindi.

Pili, Serikali pia iimarishe mipango ya hifadhi za chakula na ziwekwe katika Kanda zote za Tanzania. Wakati huo huo wakulima waachwe

wauze chakula wanakotaka ili wapate kipato kitakachowawezesha kulima tena au kuongeza wigo wa biashara. Serikali isijiingize katika makubaliano ya kununua vyakula mfano, korosho. Serikali inunue kama wafanyabiashara wengine. Ili kusaidia wakulima hawa Serikali inaweza kujenga Kiwanda cha Korosho ikishirikiana na wafanyabiashara ili kutoa ajira. Pia Korosho zikiwa *exported* wakati zimebanguliwa na kuandaliwa vizuri zitaleta fedha za kigeni.

Tatu, wakulima na wananchi wanalamika kwa sababu mbolea zinachelewa jambo linalosababisha wasipate mazao ya kutosha. Mbolea zikipelekwa kabla ya msimu wa mvua, mazao yatakuwa mazuri na chakula cha kutosha kitapatikana nchini. Serikali inaweza kutumia Sheria ya PPP kuhamasisha wafanyabiashara kuanzisha kiwanda kingine cha mbolea ili kukidhi mahitaji ya mbolea.

Nne, Serikali ikidhibiti bei za vyakula mfano, sukari, mchele, unga, itawapa ahueni wananchi. Inawezekana kabisa Serikali ikazuia uingizaji wa vyakula vinavyopatikana nchini kama vile mafuta ya kula ili kuweka hamasa kwa wakulima wetu kulima zaidi alizeti, karanga na kadhalika.

Tano, uagizaji wa mafuta ya jumla *bulk procurement* utapunguza udanganyifu katika manunuzi na kuhakikisha ubora wa mafuta *quality*. Serikali iagize na kufanya zoezi hili, ili kuwepo na uhakika wa *flow* ya bei na usalama wa upatikanaji wa mafuta hayo kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, mapato na matumizi. *TRA* inakusanya kodi kwa takriban Watanzania 1,600,000. Idadi ya Watanzania wakiondolewa watoto na vijana wanaosoma inawezekana ambao wanaweza kulipa kodi ni zaidi ya Watanzania milioni kumi. Kuna haja vitambulisho vya Taifa vipatikane mapema ili idadi ya wale ambao wanaweza kulipa kodi ijulikane.

Wafanyakazi wa *TRA* waliopo sasa wengi wameingia katika tabia ya rushwa. Makadirio wanayofanya hasa kwa wafanyabiashara wa asili ya Kiasia ni kidogo. Kuna haja ya wafanyakazi hawa waangaliwe upya na pengine TAKUKURU ifanye kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali imeanza kupeleka gesi maeneo ya Kilwa. Serikali ijiaandae kupokea zao hili la gesi, waandaliwe wataalam waadilifu. Mikataba budi iwe ya uwazi na yenye tija kwa Taifa. Watanzania wakipata gesi ya kupikia, wataacha kukata miti. Viwanda vikipata gesi ya kuendeshea mitambo gharama za uendeshaji zitapungua na bei ya *products* zao zitakuwa pia nafuu kwa Mtanzania.

Misitu ilindwe na Serikali itekeleze mpango wake wa *performance forest management*. Vijiji vinavyozunguka mipaka ya hifadhi za Taifa vipewe asilimia ya mapato yanayotokana na uwekezaji katika misitu hiyo ili wailinde. Wafanyabiashara waliopewa leseni wapande miti kwanza na picha zao zibandikwe katika kijiji au kitongoji husika na ofisi za Wakuu wa Wilaya wawe na nakala ili wanakijiji husika wasirubuniwe na mtu ye yote mwingine ambaye ni tofauti na picha waliyonayo.

Serikali pia ihamasishe Watanzania kuwa na utamaduni wa kuwa na mashamba ya miti. Hii itasaidia *effects* za *climate change* na pia itawapatia wananchi kipato.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji unatakiwa uwe na msukumo zaidi hasa katika uanzishwaji wa viwanda, jambo ambalo litakuza ajira nchini. Mfano, Kiwanda cha Juice Mkoani Tanga, Kiwanda cha Nyama Mkoani Shinyanga, Kiwanda cha *Sliced Potatoes 'French fries'* Mkoani Iringa au Mbeya, mashine za kukoboa mpunga na mahindi na kufungasha package mchele au unga katika Mikoa ya Tabora na Mbeya, Kiwanda cha Kusindika Tangawizi Mkoani Kilimanjaro, Kiwanda cha Kusindika Nyanya, Mbogamboga na Kiwanda cha Kusindika Ngozi Mkoani Mwanza au Shinyanga. Viwanda hivi vikipatikana hakika ajira itapatikana na Taifa la Tanzania litapata utajiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kazi nzuri. Baada ya utangulizi huu naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu *balance of trade*. Taarifa inaonesha kwamba naksi (*deficit*) ya urari wa biashara imekuwa ikiongezeka toka asilimia nane mwaka 2000 mpaka asilimia 17 ya *GDP* mwaka 2010. Maoni ya takwimu hii ni kwamba tumeendelea kuagiza *imports* nyingi sana wakati uwezo wetu wa kuuza nchi za nje *exports* si mzuri. Tunahitaji mtazamo na mikakati, sera mpya ya kuhamasisha uzalishaji yaani *competitiveness related policies*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme *energy for the country*. Tunahitaji bajeti ya umeme vijiji (REA) iongezwe mara dufu ili kuhakikisha kwamba, vijiji vinakuwa na nafasi ya kuchangia nguvu zaidi kwenye uchumi wa Taifa .

Mheshimiwa Spika, kuimarisha vyanzo vya uzalishaji umeme vilivyo na bei nafuu yaani mkaa wa mawe, gesi na upepo.

Mheshimiwa Spika, huduma za fedha na benki. Tunahitaji mkakati mpya wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na *micro finance services* vijijini ili huduma ya fedha iimarike na iwafikie wengi *financial deepening*. Huduma nzuri ya fedha vijijini itasaidia kusukuma kasi ya uchumi vijijini.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakuomba upokee pongezi zangu za dhati kabisa kwa namna ulivyowasilisha hoja ya Kamati unayoiongoza ya Fedha na Uchumi. Umetoa mapendekezo ya maana sana kama Serikali ikiamua kuufuata na kuutekeleza ungeweza kutusaidia angalau makali ya maisha yangepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha yamekuwa magumu sana. Wananchi wa kipato cha chini na wakulima wana hali ngumu sana. Kwa sababu hiyo nakuunga mkono kwa yote uliyopendekeza umechambua na umeeleza sababu zote zinazoweza kutufanya tupate nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa kuumiza vichwa ili itafute namna ya kuboresha maisha ya Watanzania. Kitakachotukwamua na kuondokana na ukali wa maisha ni pamoja na kuondokana na kodi kwenye bidhaa za chakula, umeme na bidhaa zote muhimu kwa matumizi ya lazima kwa mwananchi (chakula, maji na umeme). Pia Serikali iangalie namna ya kutumia rasilimali zetu, madini, misitu yetu, rasilimali za bahari na maziwa ili ziweze kutusaidia. Tuweze kuziba pengo la kodi zitakazofutwa ili tupate bidhaa kwa bei nafuu. Pia Serikali ipunguze kodi ya VAT ili tuwe sawa na nchi zingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti naona niishie hapo ila nakupongeza sana wewe Mwenyekiti pamoja na wajumbe wako wote, mmeefanya kazi nzuri sana na mmeishauri Serikali vizuri lakini Serikali hii mmh!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ina jukumu zito la kusimamia shughuli zote zinazohusu masuala ya fedha na ukuaji wa uchumi. Hivyo, nashauri kwamba Bunge na Serikali lichukulie kwa uzito mkubwa Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa tajwa.

Pili, Bunge lipitishe azimio maalum la kunusuru uchumi wa nchi na kupunguza gharama za maisha kwa wananchi. Hatma za haraka zinahitajika kudhibiti matumizi ya Serikali kwa kuwa kwa hali ya sasa matumizi ya Serikali ni makubwa kuliko mapato.

Tarehe 9/03/2012 mapato ya Serikali yalikuwa Shilingi bilioni 25 wakati malipo yaliyofanywa na Serikali ni zaidi ya Shilingi bilioni 58. Hali hiyo ya kuongezeka kwa matumizi zaidi ya mapato inaendelea kipindi chote cha mwezi Machi mpaka Aprili. Wizara ya Fedha pekee ni hatua zipi imechukua kupunguza matumizi kama ilivoahidiwa na waziri Mkuu wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge la Bajeti.

Aidha, Kamati ya Fedha na Uchumi ielekeze ukaguzi maalum kufanyika kwenye fungu la deni la Taifa. Bunge na Serikali kwa pamoja, mihimili yote miwili ihakikishe kwamba kiwango cha misamaha ya kodi hakizidi asilimia tano ya kiwango cha mapato yanayokusanywa, suala ambalo linahitaji Sheria ya Kodi ifanyiwe marekebisho ya dharura mwanzoni mwa Bunge la bajeti katika Mkutano wa Nane.

Hili Serikali ilichukulie tatizo la mfumko wa bei, ongezeko la bei na kupanda kwa gharama za maisha kuwa ni tishio kwa usalama wa nchi na maisha ya wananchi. Hivyo, mpango wa mwaka na mwongozo wa bajeti utakaojadiliwa katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge, kipaumbele cha pekee kiwekwe katika kushughulikia tatizo hili. Kwa kuwa asilimia 70 ya mfumko wetu wa bei unachangiwa na kupanda kwa gharama za chakula, kipaumbele cha mipango na uchumi wetu kiwe ni kuongeza uzalishaji na usambazaji wa chakula.

Aidha, mianya ya ujisadi katika pembejeo na ruzuku za kilimo izibwe haraka. Pia mianya ya ujisadi katika usambazaji wa vyakula toka Hifadhi ya Taifa ambacho kinasambazwa lakini bei ya vyakula haijashuka ikiwemo katika Jimbo la Ubungo. Aidha, hata baada ya kupunguza kodi kwa baadhi ya vyakula, bei haijashuka kama ilivoahidiwa na Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu Bungeni. Serikali inapaswa kutoa maeleo ya kina kuhusu hali hii. Serikali itekeleze mapendekezo niliyotoa ya kutungwa kwa sheria ya udhibiti wa bei ya bidhaa.

Tatu, katika kutekeleza majukumu yake hususan ya kuisimamia Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, naomba Kamati ya Fedha na Uchumi itoe uzito unaostahilli katika kufuatilia fedha za miradi ya maji ya Jiji la Dar es Salaam. Kamati izingatia kuwa miradi ya awamu ya kwanza ya DWSSP/DWSSP haikutengewa fedha za kutosha na zilizotolewa hazikutolewa kwa wakati na kusimamia ipasavyo.

Hivyo, katika mpango wa bajeti kwa mwaka 2012/2013, uzingatie mahitaji yaliyotajwa kwenye Mpango wa Taifa wa miaka mitano na mapendekezo niliyotoa wakati wa kupitishwa kwa mpango husika. Aidha, Kamati na Wizara ya fedha ifuatilie kwa karibu kuhakikisha

kwamba fedha za ujenzi wa bwawa la Kidunda, upanuzi wa Ruvu Juu na uwekaji wa mtandao wa mabomba unatekelezwa kwa haraka kwa fedha na mkopo kutoka India pamoja na vyanzo vya ndani.

Nne, katika kushughulikia bajeti ya Wizara ya Mahusiano na Katibu (Ofisi ya Rais) na kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara husika mradi wa MKURABITA ambao ilitengewa Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi eneo la Kimara na maeneo mengine ufanyike ili mradi uweze kuwa na matokeo mapana katika maeneo mbalimbali.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kuchangia machache kuhusu Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, maendeleo hayawezi kupatikana katika nchi hii iwapo tunachagua viongozi ambao wanajisahau shughuli zao. Tutaishia kusema uchumi unashuka, moja ya vitu vinavyochangia ni umeme. Ni lini umeme utasambaa nchi nzima? Umeme umekuwa na ghamama kubwa kufanya mtumiaji wa kipato cha chini kushindwa kutumia.

Je, ni lini tutaepuka ukataji wa miti kiholela wakati hata hiyo gesi pia haijawafikia wananchi walio wengi? Mfano Wilaya ya Kondoa, umeme upo maeneo ya karibu na Kata ya Kondoa Mjini. Je, huko kwingineko ni lini umeme utafika, au gesi nao hao wananchi wanufaikie na wapunguze adha za ukataji miti ovyo?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iliangalie Shirika hili la TANESCO, limekuwa haliwajali wateja wake wa haliwathamini kama Watanzania wenzao, kwani mtumiaji wa kawaida hulipa ghamama kubwa kuliko anayetumia mashine ya upasuaji mbao au nafaka. TANESCO huwaleta bili wateja wao kubwa mno bila kujali kupanua wigo wa kufuatilia hayo ili kupunguza manung'unico ya wananchi juu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, bado nipo Wizara hii ya Nishati na Madini, hivyo naomba niisisitize Wizara hii kuitia Serikali kwamba mikataba mibovu isiyo na faida na wananchi imekuwa ni matatizo katika Sekta hii ya Madini na Nishati.

Mheshimiwa Spika, naomba hapa nianze na suala la uchukuzi. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilikuwa zamani, siyo wakati huu tena.

Mheshimiwa Spika, ujenzi hauna ufanisi, utendaji kazi, kwani kila mwaka Serikali inapoteza mabilioni ya fedha kwa kukarabati barabara. Barabara hazina uimara hata ijengwe kwa lami. Utakuta siku chache tu tayari imeshabomokabomoka, Mkoa wa Dodoma hauna stendi ya

mabasi iliyo na tija, ni ndogo, haina hadhi hata kidogo, labda mfano tu huo, Madaraja yakijengwa leo mwaka huu mwakani tena yanajengwa. Tuangalie tatizo la Idara ya Ujenzi ni nini, na iweje hata barabara za vumbi zinakuwa tatizo? Serikali iangalie kwa umakini, utendaji ndiyo tatizo au vitendea kazi labda havina uimara.

Mheshimiwa Spika, suala la fedha na uchumi, ukusanyaji mapato kupanda na kushuka, hii yote utendaji bila uaminifu husababisha nchi na uchumi wake kuyumba. Serikali ikae kwanza kutathmini watendaji wake. Ipo wazi kabisa!

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi yetu Tanzania ni mkubwa na rasilimali tunayo ya kujivunia hata nchi za Ulaya wanazitamani. Tuna madini, bandari, mbuga za wanyama, rasilimali watu na mizunguko ya kila siku *TRA* inakusanya mapato, pesa nyingi zipo Serikalini na watu wachache tu. Je, kwa nini uchumi unashuka? Je, hawa wananchi wa kawaida watapataje maisha yenyenafuu?

Mheshimiwa Spika, tuangalie vitu kama vile sherehe zisizohitaji fedha zisitumike zielekeze kununua vifaa vya uokoaji majini na nchi kavu kukuza kilimo chetu kwa kuwapatia wananchi pembejeo, mbolea, vifaa vya maabara kujenga nyumba za maaskari na watumishi kwa bei nafuu kwa kutumia mapato yetu wenyewe. Serikali iangalie hayo yote yawezekane, tusikalie kubinafsisha ardhi yetu yenyenafuu rasilimali zetu. Naishauri Serikali kuanza kwa kurekebisha angalau machache. Nashukuru.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja za Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa kamili ya Fedha ukurasa wa tisa imesilitiza kwa Serikali kuhusu programu zake za kuhakikisha chakula kinanunuliwa kwa wakulima kwa wakati na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati na kusambazwa kwenye mahitaji na usambazaji wa pembejeo, ufuatane na misimu ya kupanda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Serikali unapopanga bajeti ya bilioni 120 kusaidia usambazaji wa mbolea za ruzuku. *LZM* wasambaze kulingana na kalenda ya kilimo siyo sahihi kuleta mbegu wakati wakulima wameshapalilia mazao na wanunue mbegu hizo kwa kulazimishwa kusaini vocha ili wakala alipwe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, Serikali iwahi kununua mahindi ili iweze kusaidia uchumi wa wakulima kuliko kuchelewa na Kitengo cha

Hifadhi ya Chakula kununua kiasi kidogo na kuacha mahindi mengi mikononi mwa wakulima. Hivyo, ni sahihi kabisa sera ya mauzo ya chakula nje, isiwe inabadilika mara kwa mara, kitu ambacho kinaathiri sana uchumi wa wakulima, kwani wanauzwa nje mazao, huacha kwenda kununua mazao (mahindi) kwa wakulima moja kwa moja. Sasa tuwaachie wauze kulingana na soko la *NFRA* na wanunuzi wengine

Pia naomba Mawakala walipwe fedha zao mapema, kwani kuchelewa kuwalipa nako kunaathiri uchumi wao SBB wanakopa Benki na vile vile wanakopeshwa mbolea na waingizaji wakubwa wa mbolea kama *T.F.C.* ambao wamekopa toka Benki. Sasa malipo yao yanapochelewa kulipwa na Serikali, husababisha tatizo la uchumi kwa wahusika na Taasisi hizo kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, nchi tajiri duniani zinapimwa na uhifadhi wa fedha na wingi wa dhahabu iliyopo katika Hazina zao. Umuhimu huu wa kuwa na hifadhi ya dhahabu, umejionyesha katika nchi tajiri duniani. Kama ilivyofanyiwa utafiti mwaka 2006, *USA* walikuwa na tani 8,146 za dhahabu; *Ujerumani*, tani 3,433 za dhahabu; *Ufaransa*, tani 2,978 za dhahabu; *Switzerland*, tani 1,332 za dhahabu; *Netherland*, tani 767 za dhahabu; *Japan*, tani 765 za dhahabu na Uchina tani 600 za dhahabu.

Nchi tatu za Afrika ambazo zimehesabiwa ni tajiri ni *South Africa*, tani 124; *Libya*, tani 112 na *Egypt*, tani 76.

Ushauri, Serikali itengeneze mtandao wa kununua kwa wachimbaji wadogo na kuweka mrahaba wa wachimbaji wakubwa, nusu yake iwekwe katika fomu ya dhahabu na kuhifadhi Benki Kuu ili kuongeza thamani ya hifadhi ya Hazina yetu kiuchumi. Naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante, sasa nitaomba tena nianze kuwaita Wenyeviti, wao wanachukua dakika 15 each, tuanze na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya awali kabisa kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kufanya majumuisho ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa yetu ya Nishati na Madini imepata wachangiaji wa kuzungumza 22 na kwa kuandika wachangiaji 11 na kufanya jumla ya wachangiaji 33. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa January Makamba – Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Daktari Dalaly Kafumu, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Daktari Binilith Mahenge, Mheshimiwa Kepteni John Komba, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Freeman Mboge – Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Asumpter Mshama, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Kigoma Malima – Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Stephen Wasira – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuandika ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Saidi Bwanamdogo, Mheshimiwa Moza Abeid Saidi, Mheshimiwa Faith Mitambo na Mheshimiwa Lucy Owenya.

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuwa nitafanya ufanuzi wa hoja chache nikiwa na matumaini kwamba Serikali itachukua hoja zote na kuzifanyia kazi kadri mlivyowasilisha hapa Bungeni na zile mlizochangia kwa maandishi nitaziwasilisha ili ziweze kufanyiwa kazi. (*Makofii*)

Vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Nishati na Madini Mheshimiwa January Makamba kwa kuwasilisha vizuri taarifa ya Kamati yetu ya Nishati na Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri waliyoifanya kupitia michango yao kwa kuzungumza na kuandika. Kweli wachangiaji karibu wote wameunga mkono kwa asilimia mia moja taarifa ya Kamati yetu ya Nishati na Madini. Ninawaashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na ninaamini tukiendelea hivi hivi kuwa wamoja tutasaidia sana kuibana na kuishauri Serikali yetu ili iweze

kutekeleza mambo mengi muhimu yenyeye maslahi na Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuainisha baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi nikianza na suala la mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa taarifa za kuthibitisha kuwa uchakachuaji wa mafuta umepungua sana lakini bado lengo la Kamati ni kuhakikisha tatizo hilo limekomka kabisa. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Kamati ipo imara ina Waheshimiwa Wabunge makini kabisa, hivyo tatizo hili tutakwenda na Wizara sambamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kufuatilia na kutoa taarifa endapo bado tatizo linajitokeza kwenye maeneo yetu ili tuendelee kuibana Serikali na ninyi Waheshimiwa Wabunge twende sambamba kufuatilia kwenye maeneo yetu kama tatizo la mafuta bado linajitokeza.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Waheshimiwa Wabunge wengi wamehimiza kuhusu suala la bei kupanda. Niiombe Serikali isisimamie bei kwa maeneo ya juu tu bali ifuatilie bei hizi mpaka ngazi ya chini, mpaka ngazi ya mtumiaji wa mwisho. Waheshimiwa Wabunge wengi wameliongelea sana hili suala na kwa uchungu mkubwa kwa sababu wananchi wetu wanapata shida sana, Serikali inadhibiti bei ngazi ya juu lakini haifuatili mtumiaji wa mwisho anaathirika kwa kiwango gani kwa bei kutokudhibitiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie suala la umeme vijijini kwa maana ya *REA*. Hoja imetolewa na Wabunge wengi sana juu ya umeme vijijini ufile majimboni kwetu. Kama tulivyoeleza kwenye taarifa yetu tunajenga hoja sehemu kubwa ya fedha zinazookolewa kutokana na uchakachuaji zielekezwe kwenye ujenzi wa umeme vijijini. Mfano, ilikadiriwa kuwa uchakachuaji wa mafuta ulikuwa unapoteza mapato kwa njia ya kodi kati ya shilingi bilioni 40 hadi shilingi bilioni 50 kwa mwezi ambazo ni sawa na shilingi bilioni 600 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati ni kuwa *REA* itengewe angalau shilingi bilioni 300 badala ya shilingi bilioni 104 za sasa ili kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme vijijini. Hii itapunguza kelele za Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuhusu suala zima la umeme kuwafikia wananchi walio wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia pia suala la uadilifu. Kamati imeliona suala la umuhimu wa uadilifu kwa viongozi na watendaji katika meneo ya kazi au kwenye nafasi zao ndio maana tumeshauri kwamba ugawaji wa vitalu vya kuchimba mafuta ufanyike kwa *tender* huru zikiendana na kilemba. Hii itasaidia sana suala la watumishi na viongozi kuwa waadilifu, bila kufanya hivyo tukienda na usiri na mambo ya kuwa na ubinagsi hatutaisaidia Serikali hii kuweza kudhibiti au kuzalisha pato la nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pia wamezungumzia kuhusu TANESCO. Kamati imeshauri umeme unaojengwa na REA au TANESCO uunganishwe kwa gharama ndogo na sehemu ya gharama inayobaki iwe sehemu ya gharama za mradi au iwekwe kwenye gharama za bei na ilipwe kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kweli Watanzania wetu wana haja sana na umeme, Waheshimiwa Wabunge wameeleza hapa lakini wengi wao wanashindwa kutokana na gharama kuwa kubwa. Hivyo, tunaomba sana ushauri huu na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge upokelewe na Serikali kuwasaidia Watanzania ili waweze kupata umeme walio wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vileyile Waheshimiwa Wabunge wameongelea suala la umeme kukatikatika. Kwa kweli hii ni kero, tatizo hili Serikali inasema ni miundombinu, basi Serikali iangalie namna ya kuiwezesha TANESCO ili iweze kukarabati miundombinu ili iweze kuepukana na suala hili la umeme kukatikatika kwa sababu Watanzania wanaathirika sana, samani zao nyingi zinaharibika, kama tungekuwa tunapata tahadhari kwamba umeme utakatika saa fulani mpaka saa fulani basi Watanzania wanakuwa na tahadhari na mali zao. Lakini umeme mara nyingi unakatika bila taarifa na vyombo vingi vinaungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wameongelea kuhusu majenereta kupasuka pasuka mara kwa mara bila utaratibu, hili nalo ni tatizo. Sasa tunaiomba Serikali iangalie majenereta haya yana matatizo gani, yamechakaa sana au wanunua viwanda feki ili tatizo hili lisijirudierudie, tunaomba sana TANESCO ituletee majenereta ambayo hayatakuwa na tabia ya kulipuka lipuka kila wakati ili kuondoa tatizo la umeme kukatikakatika kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, pia suala la gesi limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi tu, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa mikoa ya Kusini kwa kutambua mchango wa Kamati na mwitikio wa Serikali. Tunawahakikishia kuwa Mikoa ya Kusini ya Tanzania

kwa ujumla mtafaidi matunda ya rasilimali hii kwa sababu Kamati hii ipo imara kweli kweli kuhakikisha inaibana Serikali kuona uwekezekano wa wananchi wa maeneo hayo wanapata mrahaba na pia wale wananchi ambao vijiji vyao ambavyo vina wakazi wengi na miradi mingi basi ipitiwe na umeme huu kuliko mabomba haya yapite tu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kuhusu suala la madini. Kamati imesisitiza kuwa haja ya wananchi au viongozi wa ngazi zote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ni kupata maelezo ya kina kuhusu madini kabla ya mradi kuanza. Kwa mfano, madini ya Urani hata ukimuuliza Mbunge haelewi maana ya Urani kwa hiyo ni vizuri Wabunge wakawa wanapewa elimu na vilevile Watanzania kupewa elimu hii itasaidia wananchi kuwa na uelewa na kuepusha migogoro mbalimbali inayojitokeza bila umuhimu wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kitabu cha Kamati yetu ukikaa kitako na kukisoma kwa utulivu na kwa kina utaona karibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge zimetolewa mapendekezo ili kuokoa muda.

Mwisho, nimalizie kwa kuipongeza Serikali kwani Sheria mpya ya mwaka 2010 sasa imeanza kufanya kazi. Nliombe tu Serikali isimamie kwa kina kama ni hisa sasa Serikali ianze kuchukua hisa kwenye migodi kuliko ilivyokuwa mwanzo mwekezaji ananufaika kuliko Watanzania wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninategemea kwamba hawa wachangiaji wote nitawasilisha majina ili yaweze kuingia kwenye taarifa yangu. (*Makofi*)

Mwisho, naomba nimalizie kwa kutoa hoja na ninaomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki! (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, naona ameungwa mkono. Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii kuelezea baadhi ya yaliyojitokeza katika mjadala wa taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Napenda kutoa taarifa kwamba waliochangia kwa kuzungumza walikuwa ni Waheshimiwa Wabunge 14 na kwa maandishi tulipokea maandishi kutoka kwa Wabunge 13. Tunaahidi kwamba ile michango ya maandishi tutaipeleka Serikalini ifanyiwe kazi na hili ndiyo linatufundisha kwamba pamoja na utaratibu huu tunaoendelea nao ni vizuri tukaingilia suala la *capacity building* kwamba hata Kamati zetu tunaweza kuwa na *supporting staff* wa kuweza kutoa majibu sahihi katika hoja zinazotolewa na Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi inashughulikia masuala yanayogusa zaidi uchumi mkubwa na tunashukuru kwamba uchangiaji wote uliofanyika umekuwa ukigusia maeneo yale yale hasa ya misingi mikuu ya uchumi mkubwa kwa maana ya masuala ya mfumuko wa bei, masuala ya biashara nje, masuala ya mapato na matumizi ambayo nina hakika kabisa kwa ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge, Selikali imepata taarifa hizo na itaendelea kuzifanya kazi na kama alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uratibu ameahidi kabisa kwamba haya yataangaliwa hata katika mpango wetu unaokuja mwakani. (*Makofii*)

Mimi ningependa tu kusema kwa sababu ya ujumla wa sekta yenyewe, jambo linalojitokeza hapa Waheshimiwa Wabunge wengi kwa njia moja au nyingine wamesisitiza sana suala la umakini katika menejimenti na uendeshaji wa uchumi wetu Tanzania. Kuendesha uchumi ni jambo kubwa na linahitaji umakini mkubwa sana na ndiyo maana tunazidi kushauri kwamba Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha na Taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya mipango na fedha ni vema zikajipanga vizuri kuimarisha uratibu, mashirikiano na maingiliano ili kuifanya Tume ya Mipango iwe ndio kitovu halisi na ambacho kinaweza kuongoza vyombo na taasisi nyingine kushughulikia masuala ya mipango na fedha na ndio maana katika taarifa yetu tumesitiza kwamba ile Sheria ya Tume ya Mipango inabidi ihuishwe.

Mheshimiwa Spika, pia si suala tu la kupeleka madaraka makubwa sehemu fulani, lakini katika nchi nyingi ambazo zina utaratibu wa Tume ya Mipango, Tume ya Mipango inakuwa kama *super Ministry* ambayo inatoa *guidance* kwa Wizara zote. Pale tutakuwa na kitovu cha *think tank* ambacho tunakizungumzia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili lazima tukubali kwamba sasa hivi uchumi ndio siasa. Uchumi ndiyo siasa kwani zipo nchi nyingi sasa hivi ambazo zinaimarisha uchumi wake na zinapoimarisha uchumi ule matatizo mengine yote yanayofuatia kwa kweli yanaweza kudhibitiwa na Serikali.

Uchumi ni eneo la kiufundi na hatuwezi kuendelea kufanya siasa katika uchumi, we can not politicize the economy. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo tutaondoka nje ya mstari. Lazima tuone sasa tunaanza utaratibu wa kuanzisha makongamano kwa kutoa ajenda za kuzungumzia uchumi wetu wa Tanzania. Kuanzia Vyuo Vikuu, kwenye taasisi zetu, hapa Bungeni, lazima tuwe na forums za economic agenda kwa sababu ya matatizo ya uchumi yanayojitokeza sasa hivi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hilo ni jambo muhimu sana. Sisi Kamati ya Fedha na Uchumi tumeona kwamba tunayo tabia ya kuelezea vyanzo vya matatizo ya uchumi wetu, lakini hatujapata fursa wakati tunapopata matokeo ya vyanzo vile kwamba tumejitayarisha vipi kupambana na vyanzo vile. Nitatoa mfano; tunapozungumzia masuala ya mfumuko wa bei kwamba yanatokana na upungufu wa chakula, tunaelewa wazi kabisa kwamba wakati wowote tunaweza tukapata tatizo la upungufu wa chakula, lakini la msingi ni ile preparedness ya uchumi wetu kujiweka kwamba mara yatakapotokea matatizo kama hayo ni kitu gani tunatakiwa tukifanye ile kuweza kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kwenye uchumi wetu. (Makof)

Kwa hiyo, tunaweza kuwa waelewa wa vyanzo tukawa tunashindwa kuelewa matokeo yake na kwamba tutajiandaa vipi.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala zima la *mind set* yetu. *Mind set* yetu kuanzia Serikalini na Watanzania kwa ujumla ni lazima tubadilike katika masuala ya uchumi. Tuwe na ujasiri wa kuhuisha taratibu zetu za kushughulikia uchumi hasa katika maeneo yale ambayo tunajua kwamba ni vikwazo katika kujenga uchumi wetu. Kwa mfano; Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamezungumzia suala zima la gharama za uwekezaji katika nchi yetu kwamba zinagusa kodi, umeme, urasimu na kadhalika. Haya ni maeneo ambayo lazima tuwe jasiri kuhuisha hata sheria zetu na hata ikiwezekana kuhuisha mfumo wetu wa kodi ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yanakwenda vizuri. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge wamesisitizia suala la kuzingatia eneo la mapato na matumizi na ni vipi tunaongelea mapato zaidi badala ya matumizi. Mfumo wa kodi unaweza kufanyiwa marekebisho kama wanavyofanya wenzenetu sasa wa Mauritius na nchi nyngine kwa sababu kodi na tozo zimekuwa ni nyngi mno na mara nyngi zinakuwa pia ni kikwazo katika kuendeleza uchumi wetu. Lakini vilevile, mikakati ya kukuza uchumi lazima iende na mikakati ya kupunguza umaskini. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka kwamba juzi juzi kulikuwa na semina Dar es Salaam, yupo Profesa mmoja kutoka Vietnam alioa modeli ya Vietnam akasema wale walifanikiwaje katika kukuza uchumi na wakati huo huo kupunguza umaskini. Kwa hiyo, ni vizuri hata Serikali tukajifunza kutoka kule tuone kwamba wenzetu wanaendeleaje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lilitlogusiwa ni huduma za kifedha. Hapa bado tunatakiwa tuendelee na suala zima la kuimarisha huduma za kifedha hasa kwa wale wenye vipato vya chini; wakulima kuititia SACCOS zao, vyama vyao vya Ushirika na ndiyo maana Kamati ya Fedha ikaainisha kabisa kwamba lazima tuendelee na utaratibu wa kutayarisha *Microfinance Act*, *SACCOS Act* na *Community Bank Act* ambazo zitakuwa zinasaidia vyombo hivi kufanya kazi hasa tukijua kwamba ni asilimia 12.3 tu ya Watanzania na vijiji ni asilimia tatu ya wakulima wadogo ambao wanapata faida hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema mwanzoni hapa mipango na bajeti zetu tunazopanga kinadharia ni nzuri, tatizo lake ni katika utekelezaji. Hili nalo ni eneo la changamoto ambalo Waheshimiwa Wabunge wanalielekeza Serikalini katika utaratibu ule ule wa kuona kwamba mipango yetu hii mizuri itoe tija na ufanisi kule tunakokwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zipo taratibu nydingine, kwa mfano; nchi kama Ethiopia kwenye suala la mfumuko wa bei wao wameamua kuondoa kodi zote kwenye zile bidhaa ambazo ni muhimu (*basic necessities*), sasa ule ni ujasiri. Wanaweza kuona kwamba unaondoa wapi kodi, ukaccompensate wapi ili vilevile kulinda mapato ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni lazima tukubaliane kwamba, *domain* ya kuendesha masuala ya uchumi na bajeti si ya Serikali peke yake. Serikali peke yake haitaweza na ndiyo maana tunazungumzia kwamba tunapozungumzia masuala yetu ya uchumi na hata bajeti zetu za Serikali ni lazima kuleta dhana shirikishi. Tuwe na mikakati shirikishi ambayo itaishirikisha Serikali, taasisi zote, vyombo vyote na wananchi kwa ujumla wao. Tukijipanga sawasawa na tukiendeleza suala la uwajibikaji kama alivyozungumza Mheshimiwa Daktari Kafumu jana, tukizungumza suala la uwajibikaji tunaweza tukajikuta kwamba ukuaji wetu wa uchumi unakua kwa kuweka mipango mizuri inayotekelzeza na hivyo kupunguza umaskini wa Watanzania walio wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo majina yote ya waliochangia kwa maandishi na kwa kuzungumza tutayaweka kwenye taarifa yetu na yale ya maandishi mengine tutayawasilisha Serikalini ili

kuendelea kuboresha utendaji kazi wa Bunge letu na Serikali kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii tena niweze kuhitimisha hoja yetu ya Kamati ya Miundombinu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tumepata michango mingi sana na karibu zaidi ya watu 35 wamechangia kwa maandishi na kwa kuzungumza humu Bungeni. Kutokana na ufinyu wa muda nitaomba nisiwataje kwa majina yao, lakini baadae tutayaandika kwenye ripoti yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Ukiwasikiliza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia humu ndani unaona wanasisitiza kwamba ili nchi yetu iweze kuendelea ni lazima tuwekeze kwenye *infrastructure*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ili kilimo cha nchi hii kiweze kuendelea tunahitaji miundombinu. Ili biashara ya nchi hii iweze kuendelea tunahitaji miundombinu na ili utalii wa nchi hii uweze kuendelea tunahitaji miundombinu. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba miundombinu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na sisi bado tunasisitiza, tunaiomba Serikali tujitahidi kadri tunavyoweza tutafute fedha kwa namna yoyote ile ili tuweze kuendeleza miundombinu ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Tanzania Mungu ameibariki na haikuwa kwa bahati mbaya sana. Ukiangalia jiografia ya nchi yetu imetuweka mahali ambapo tukitumia fursa tulizonazo nchi yetu itakuwa kwa haraka sana kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Singapore, Waziri Mkuu wa Kwanza Lee Kuan Yew wakati nchi inaanza aliangalia nchi yake akagundua hakuna resources nydingi, lakini resource kubwa waliyokuwa nayo ilikuwa ni bahari. Resource ya pili aliyoomua kuhangaika nayo ikawa ni elimu. Lakini sisi Tanzania tumepewa kila kitu, sasa ni kazi yetu kujenga miundombinu yetu ili kuweza kutumia hizo fursa tulizonazo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, barabara. Barabara ni kiungo muhimu sana kwa maendeleo ya Tanzania, lakini ni lazima tujenge barabara ambazo kwanza zitatuunganisha sisi na nchi jirani, mikoa na wilaya zetu ili kama walivyosema wachangiaji wengine, alisema hapa Mheshimiwa Wasira

kwamba ukilima mahindi Rukwa uwe na uhakika unaweza ukaenda kuyauza unakotaka. Unaweza ukaenda Kigoma, Shinyanga, Mbeya na unaweza ukaja hata Dar es Salaam. Haya yote yatawezekana kama barabara zetu ni nzuri, lakini pia kama reli yetu ni nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, umuhimu wa barabara na reli, ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Naipongeza sana Serikali imefanya kazi kubwa kwenye barabara, lakini kwa bahati mbaya sana kwenye reli kwa kweli hatujafanya kazi ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, reli ndiyo njia pekee itakayofanya ghamama za bidhaa zetu ziwe za chini. Ameondoka hapa Mwenyekiti mwenzangu Mheshimiwa Daktari Kigoda ambaye aliongelea *inflation* na ghamama za kununua vitu (*purchasing power*). Tukiwa na reli madhubuti tuna hakika bidhaa za viwandani zikifika Kigoma zitakuwa za bei ya chini kwa sababu ghamama za usafirishaji zitakuwa ni pungufu. Bei ya kuchukua mazao yetu kuja bandarini kwa lengo la kuyapeleka nje, zitakuwa za chini kwa sababu miundombinu yetu ni mizuri. Kwa hiyo, naiomba Serikali kabisa tuwekeze vya kutosha kwenye reli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumesema kwenye Kamati yetu tuna madeni makubwa kwenye barabara. Ni muhimu Serikali tujitahidi madeni haya yaishe ili tusilipe fedha nyingi mwisho wa siku. Suala la barabara limeongelewa na Wabunge wengi sana hasa kuhusiana na msongamano wa Dar es Salaam. Tunalo tatizo la Dar es Salaam, tunalo tatizo sasa la Arusha na Mwanza. Ni muhimu kama Serikali tuijandae kuhakikisha tunatatua matatizo haya. Muda unaopotea barabarani ni mwingi sana na matokeo Watanzania hawa hawawezi kuwa effective katika kukuza uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ipo rai imetolewa na baadhi ya Wabunge kuwa Dar es Salaam kuna barabara 27 zimeomba zipandishwe hadhi, nimuombe Waziri wa Ujenzi tafadhalii sana tukipandisha barabara zile 27 maana yake barabara nyingi za mitaani zitakuwa zimewekwa lami na hivyo tunakuwa na hakika watu wote hatutakusanyika kwenye barabara kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, reli. Tumesema kwenye Kamati mwaka 1914 reli (treni) ya kati ilikuwa ni *regular*, kila siku ilikuwepo, leo haipo! Hatuwezi kukubali hata kidogo. Niiombe Serikali iwekeze vya kutosha kwenye reli ya kati. Wakati tunasubiri kujenga *standard gauge* niombe Serikali itafute fedha kwenye mashirika yetu ya NSSF, PPF na kadhalika reli iliyopo sasa ikarabatiwe ili iweze kuanza kufanyakazi na tuweze kuokoa uchumi wetu, wakati tukiisubiria hiyo mipango mikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ATCL, yanaoendelea kwenye ATCL hata kuyaeleza unaona vibaya. Sisi tunaamini hatutakiwi tuseme kama tuna Shirika la Ndege. Shirika la Ndege ambalo leo lina ndege moja, lakini lina wafanyakazi zaidi ya 200, haiingii akilini hata kidogo! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bado nina amini shirika lile ni muhimu sana. Ni wakati wa Serikali sasa iwekeze, lisafishe mizania kwenye hesabu ili tuondoe madeni yote ya nyuma na baada ya hapo tuweze kwenda mbele zaidi. Niombe watu wa Wizara ya Uchukuzi tukae tujiulize tunahitaji ATCL? Tukae tujiulize ili ATCL iweze kufanyakazi tunahitaji kufanya nini? Mimi nina amini tukijiuliza maswali vizuri ATCL itaenda mbali. Lakini pia tujaribu kuweka wafanyakazi na viongozi wa mashirika hayo ambao wana uadilifu mkubwa. Leo ni mwaka wa pili ATCL haina bodi yake. Ni matarajio yangu, kuchagua bodi haihitaji bajeti bali ni suala la maamuzi tu, tena ya kisiasa. Ni matarajio yangu kazi itafanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, viwanja vya ndege. Viwanja vya ndege vya Tanzania vyote hali yake ni mbaya sana. Niwaombe sasa wenzetu tunajua ipo miradi inaendelea, lakini haiwezekani kila siku tukawa tunakutana hapa kama Bunge lako Mheshimiwa Spika, tunasema kwamba tuko mbioni, tuko kwenye mchakato, tunajipanga, tuko kwenye mazungumzo, Watanzania wamechoka kusikia lugha hizi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema kwenye Kamati yetu, tunaomba sana watu wafanye kazi ili shughuli hii ya *infrastructure* iweze kwenda vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam ndiyo kitovu cha uchumi katika nchi yetu. Kwa kweli Mungu ametusaidia tuna Bandari kubwa ya Dar es Salaam na hizi za maziwa. Bado ni ari ya Kamati yangu kama tulivyosema tunaomba Serikali uwekezaji katika bandari hii ufanyike haraka iwezekanavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba Bandari ya Dar es Salaam tuache siasa, tufanye kazi. Tuache kuweka hoja zetu binafsi, tuweke maslahi ya nchi mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam tumeanza kuongea kwenye Bunge lako toka mwaka 2008. Tangu mwaka 2008 tunaongea kujenga gati ya 13 na 14. Ni ajabu sana mwaka 2012 bado tunaongelea mikakati na mipango.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana na nimpongeze Waziri wa Fedha *in particular*. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ninayo barua hapa ambayo ameiandikia *Exim Bank* ya China ya kuchukua mkopo na wametoa guarantee ya Serikali kwa ajili ya kujenga gati ya 13 na 14. (*Makofii*)

Niombe sana watu wa Wizara na mtu yeote mwenye nia anayeona yeye inafaa tuache mkakati huu ulioanzishwa na Wizara ya Fedha na Wizara iliyokuwa ya Miundombinu na watu wa *TPA* wamalize kazi ya ujenzi wa gati ya 13 na 14. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alisema kujitegemea ndiyo heshima. Taifa lolote linalojitegemea lina heshima kubwa sana duniani. Ukiona una uwezo wa kukopa maana yake una uwezo wa kulipa. Kama una uwezo wa kulipa na una uwezo wa kukopa maana yake sasa wewe unajitegemea.

Tunaenda kutafuta mtu mwingine wa kuja kushirikiana naye wa nini wakati tuna uwezo wa kukopa, tuna uwezo wa kulipa na tulishakopeshwa? Kwa kweli kwa wale ambao mmesoma mambo ya fedha mpaka benki inakukopesha maana yake wewe unakopesheka na hii ndiyo heshima ya Taifa lolote duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema gati ya 13 na 14 ni ari ya Kamati, tuliyyoyasema yote hapa ndani ni ya kweli na tuna hakika nia yetu tunataka tunapokuja kwenye bajeti tuambiwe ujenzi wa gati hili umeanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hayo? Fedha tumeypata, contractor tumeypata, ninayo barua hapa mpaka *terms zipo* tayari. Sasa tunachelewa ili iweje? Tunamsubiri nani?

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimalizie kwa kusema Wizara ilituletea hapa orodha ya walijitokeza kuwekeza au kujenga kwenye miradi mingi ya bandari. Hapa kuna jila la kampuni, aina ya mwekezaji, chanzo cha fedha, muda wa ujenzi na matakwa mengine na maoni ya *TPA*.

Mimi nitamuongelea mtu mmoja aliyejitokeza namba 12 anaitwa *China Holding International – China*. Atajenga kwa BoT ambayo *WTO* na *ITO* hawaiungi mkono kwa sababu inakuja kuzinyanyasa nchi zinazoendelea. Watajenga kwa fedha zao, wakimaliza kujenga wanataka wapewe mkataba wa kuendesha bandari hiyo kwa miaka 45.

21 APRIL, 2012

Mheshimiwa Spika, narudia tena Kamati yetu tumesema na tunarudia hatutakubali kwa sababu tunaamini Serikali imeishatafuta mkopo, tunaomba mkopo huo ufanye kazi bandari hiyo ijengwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwenye mada yangu. Nami pia nikushukuru Mheshimiwa Spika. Naomba nikuhakikishie jambo moja kwamba, Kamati yetu imejaa weledi, ni wazalendo, inafanyakazi kwa uzalendo mkubwa na haina nia mbaya na mtu yejote, lakini asiyefanyakazi na mwenye nia mbaya hatutamvumilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Makamu wa Mwenyekiti.

MHE. MUSSA A. ZUNGU – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na pumzi ya kuwepo hapa mbele ya Bunge lako Tukufu. Lakini vile vile nikushukuru na wewe kwa kutupa nafasi Kamati hii kuweza kuwasilisha na kuhitimisha Taarifa ya Mwaka kwenye Bunge lako hili Tukufu. Jumla ya wachangiaji kwenye Kamati yetu katika suala la Ulinzi, Usalama na Mambo ya Nje walikuwa ni Wajumbe 14, nawashukuru wote kwa michango yao mizuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Mheshimiwa Komba kuhusu hofu ya mpaka kati ya nchi yetu na Malawi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Komba na napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na napenda kukuhakikishia wewe Mheshimiwa Spika, kwa vyombo vya ulinzi vimeshaanza kuchukua hatua madhubuti ya kuhakikisha kuwa suala la mpaka kati ya Malawi na Tanzania linajadilika na linalindwa kufuatana na diplomasia zilizoanza. Ni kweli kulikuwa na ndege mbili ziliruka kwa siku tano tofauti na vyombo vya ulinzi vilichukua nafasi vya kuwasiliana na Muambata wa Malawi wa Kijeshi na kumweleza kitendo hicho alichokifanya ni kitendo ambacho hakikubaliki. Lakini hata katika *charter* ya Umoja wa Nchi za Kiafrika maeneo ambayo pale tuna-share maji mpaka ni *automatically* unakuwa katikati ya maji.

Mheshimiwa Spika, sasa naingia kwenye mchango wa Mheshimiwa Kombo ambaa aliomba jana hapa kuhusu haki, iweje Jeshi la Polisi liweze kutenda haki kwa raia, lakini lishindwe kutenda haki kwa askari ambaa walikuwepo kwenye Jeshi lake. Namshukuru sana Inspeksa Jenerali wa Polisi. Nimempigia simu saa 12.30 asubuhi, saa 1.30 amenipa majibu ya Polisi na majibu ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Khamis Kombo, Mbunge wa Magogoni, Wete, Pemba. Askari namba D5657 Koplo Abass, D5713 PC Ramadhani F4982 Shaibu Khamis Makame na E3664 PC Haroub Nassor Hamad walifukuzwa kazi kwa utovu wa nidhamu na sio kusimamishwa kazi kama ilivyodaiwa na Mheshimiwa Mbunge. Askari hawa walifukuzwa baada ya kukamilisha taratibu na miongozo yote ya Mashtaka ya Kijeshi kama ilivyoainishwa kwenye PGO 106. Kuhusu barua zao za kufukuzWa kazi, *Certificates of discharge* watusika wanapaswa kuwasilisha barua za kuomba kupatiwa barua hizo na nashauri wawasiliane na Kamishna wa Polisi Zanzibar kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu askari XC8555 Koplo Amour Selemani Amour aliyefariki tarehe 2 Januari, 2008, mafao yake yalichelewa kutokana na taratibu za kifamilia kuhusu mirathi kuchelewa kuwasilishwa. Hata hivyo, kwa sasa taratibu hizo zimeshawasilishwa na suala hilo linashughulikiwa na msimamizi wa mirathi ndugu Sufiani Suleiman Amour amewasilisha nyaraka husika Ofisi ya Kamishna wa Polisi, Zanzibar kwa madai haya. Hata hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge Khamis Kombo pale ambapo bado hajaridhika na anazo taarifa za ziada ambazo zinaweza kusaidia kumaliza tatizo hili basi aonane na Kamati yetu ili tuweze kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Phillipa Mturano anazungumzia kuhusu uhalifu wa Polisi. Ziko *isolated cases* za Polisi wahalifu na hii si kwetu tu karibu duniani kote, lakini pale ambapo Polisi ye yote anakutwa anavunja maadili ya Kipolisi anachukuliwa hatua za kinidhamu na kufukuzwa kwenye Jeshi. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge, Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya zote na za Mitaa pale wanapoona kuna mchezo mbovu au kukiuka maadili ya Kipolisi kwa vyombo vyoyoyote vya kiusalama watoe taarifa ili tuweze kuwashughulikia. Suala hili si suala la Idara ya Polisi peke yake, ni suala letu Wabunge wote pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ameendelea kuzungumzia kuhusu wageni haramu. Wageni haramu wameingia wengi, lakini Polisi peke yake kukuhakikisha kuweza kudhibiti wageni haramu hawawezi. Lazima sisi wenyewe tushirikiane na vyombo vya ulinzi kuhakikisha wageni haramu wanachukuliwa hatua zinazostahili. Wageni haramu wengine tunawakaribisha sisi wenyewe. Wageni haramu wengine tunawapa mpaka watoto wanawaoa, humu humu Tanzania na rekodi hizi zipo. Kwa hiyo, suala hili si suala la Polisi, hili suala ni letu wote Watanzania tuhakikishe nchi yetu haivamiwi na wageni haramu.

Mheshimiwa Spika, anaendelea Mheshimiwa Philipa Mturano kuwa kuna haki za waliopigana vita Kagera. Kama kuna taarifa sahihi za baadhi ya wapiganaji ambao hawajapata haki zao, namwomba Mheshimiwa Philipa Mturano alete taarifa hii kwenye Kamati ili tuweze kwanza kushughulikia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Haji Khatib, Mbunge wa Micheweni, anasema toka mwaka 1937 sasa ni takriban miaka 35 hakuna jengo la makazi kwa askari katika kituo hiki. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuliona hili na hili Kamati limeliona, tutaweza kushirikiana na Wizara yetu ili tujue tutafikia wapi. Lakini kama hoja hii hii inaungwa mkono na inakaziwa na Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni kwa nyumba za askari Magomeni hazifai. Ni kweli askari wetu wanaishi katika mazingira mabaya sana. Lakini Polisi na wao vile vile tutawashawishi wafanye mkataba kama walivyofanya Jeshi la Ulinzi wa kuingia mkataba na sasa kutaka kujenga nyumba 10,000 za askari wa Jeshi la Ulinzi. Kilichotakiwa ni kuweka mikakati tu, *grace period* ya kulipa mkopo ndio wakati sasa nyumba zinajengwa na baada ya miaka mitatu wala Jeshi hili halitahitaji fedha za ziada, zile fedha tulizolipia pango sasa hivi ndizo zitatumika ku-service ule mkopo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Magogoni, yeye anasema Umoja wa Afrika umekosa meno. Kama mtakumbuka na sisi kwenye taarifa yetu tumesema vilevile Umoja wa Afrika umekosa meno, umekosa ushirikiano, umekosa uzalendo wa Kiafrika wa kujadili masuala haya ya Kiafrika. Lakini Mheshimiwa tumeshamweleza Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na kutakuwa na kikao hivi karibuni kutazama aina ya ushirikiano au mikakati gani sasa tuifanye wakati nchi ya Afrika inavamiwa na nchi zingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika, Mbunge wa Ubungo, yeye kwanza ameunga mkono kwa suala la *defence diplomasia*. Huu ni mpango ambao umeanzishwa na Jeshi ambao Wanakamati tumeuridhia. Mpango huu una mahusiano makubwa sana na Afrika Kusini, tuna uhusiano na Majeshi ya *NATO* na Majeshi yetu yameshaanza mazoezi ya kivita na nchi hizi za jirani na nchi za Ulaya katika kuboresha diplomasia ya ulinzi. Mtaona vile vile hata katika kulinda mipaka yetu baharini tunashirikiana na Majeshi ya *NATO*, tunashirikiana na Majeshi ya Afrika Kusini katika kudhibiti na kama juzi tulikamata Mabaharia hawa waharamia kama 12 kutoka nchi ya Somalia ambao walliingia kwenye maji yetu na kutaka kufanya uovu ndani ya maji yetu. Kwa hiyo huu ni mfano mzuri wa Serikali inavyoshirikiana na nchi zingine katika diplomasia ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika naye amezungumzia kuhusu ku-share *intelligence*. Yapo maeneo ambayo tuna-share *intelligence*, lakini za kiuchumi katika maeneo yetu. Mheshimiwa Mnyika pia amezungumzia posho za askari. Kulikuwa na ahadi ya posho za Askari Polisi ziwe shilingi 150,000/= kwa mwezi. Hili linafanyiwa kazi, jana nimezungumza na Waziri ameshapeleka taarifa Serikalini na Serikali inajiardaa na bajeti hii na sisi tutajaribu na tutakazia ahadi ya kuwalipa posho askari shilingi 150,000/= kwa mwezi iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile litakapokuja suala la Sera za Ulinzi katika nchi hii pamoja na *National Defence Act* ya nchi hii maslahi ya watumishi wa vyombo hivi vya ulinzi itabidi watatolewa katika ule mfumo wa kulipwa maslahi, mafao yao kwenye njia za kiraia, wapate kwenye njia maalum katika mfumo huu wa sheria hii mpya ambayo tunaiptia sasa. Mheshimiwa Mnyika ameendelea kusema suala la Afrika Mashariki kwenye mchakato wa *EPA*. Hili suala ni very sensitive Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Ulaya kama alivyozungumza Mheshimiwa Membe wana utaratibu bado wa kutaka kuja kutawala tena Afrika kwa kunyonya, lakini kwa njia za mikataba. Mikataba hii Kamati yetu imeikataa na hivi karibuni nilikuwa Brussels na tulipiga vita sana, tumekataa kabisa suala la *market excess regulation* ambayo *Commission* hii ya *European Union* wanataka kushinikiza Wabunge wa *European Union* wakubali kuweka *deadline* ya namna gani watakavyoendelea kutubana, namna gani watakavyotaka kuchukua mali kutoka nchini mwetu bila kulipa ushuru, hicho kitu hatutakubali kabisa.

Mheshimiwa Spika, nilikuomba na kuna barua inakuja Ofisini kwako na Kamati imeteua baadhi ya Wabunge kwenda ku-lobby kwenye Bunge la Ulaya na tuna mahusiano mazuri sasa hivi na *International Development Committee* ya Bunge la Ulaya ambao wanatuunga mkono kuona kuwa nchi za Kiafrika zikikubali mkataba huu zitaumia.

Mheshimiwa Spika, uko mchezo vile vile wa Bunge la Ulaya kutaka ku-lobby nchi moja moja katika *East Africa* kuingia kwenye mkataba huo. Nataka kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge katika *Treaty* ya *East African Community* kuna eneo ambalo linaitwa *Joint Trade Agreement* na wote tunakubaliana tu, tunapo-negotiate na watu kutoka nje kwenye masuala tuna-negotiate as a block. Tutakapoanza ku-negotiate nchi moja moja hatutaweza kupata haki. Kuna nchi ya jirani ndiyo itakayoumia zaidi kwa sababu wao katika rating za kiuchumi ni *non-LDC* (*non List Developing Countries*). Watakapoamua ku-negotiate peke yao

21 APRIL, 2012

wataondokana na mfumo wa nchi zetu zilizobakia ambazo hatutakiwi kulipa ushuru kwenye export zetu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile mkataba huu wameshasaini nchi za Caribbean na mpaka leo huu ni mwaka wa tatu hakuna manufaa yoyote nchi hizi ambazo wanapata, matokeo yake ni nchi za Ulaya peke yake ndizo zina-benefit na hasa zina benefit kwenye masuala ya kiuchumi. Sasa hivi asilimia 60 ya samaki wanaokwenda Ulaya wanatoka kwenye bahari zetu na samaki hao wanavuliwa bila kulipiwa ushuru wowote. Tunakosa mapato makubwa sana na ndio maana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MUSSA A. ZUNGU – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi lakini muda umekwisha.

SPIKA: Kengele ya pili. Ulipofikia pazuri.

MHE. MUSSA A. ZUNGU – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kabla sijawahoji kabisa kabisa nina mambo machache ya kufanya. Kwanza kabisa wakati tunaanza mjadala huu kufuatana na orodha yangu mchangiaji wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Arfi, wa pili alikuwa Mheshimiwa Mbowe. Sasa wote wawili walichelewa, bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge Mnyika akawa ameomba Mwongozo wa Spika. Tukawa tumeujadili huo Mwongozo, katika kufanya hivyo kweli Mheshimiwa Mbowe akawa amefika.

Sasa mimi nadhani kwa *ku-slip of the tongue*, kwa kweli nilisema kama ilivyo kwenye *Hansard* nasoma sasa: "Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, shukuru jambazi wako, nikafanya mkato, jamaa wako amesema kuhusu Mwongozo mpaka umewahi.

Sasa naomba katika *Hansard* neno jambazi litoke, nafikiri nilikuwa nataka kusema jamaa wako. Kwa hiyo, naomba kama nimemuudhi mtu hapa, itoke, lengo langu lilikuwa ni kusema jamaa wako, tena bahati nzuri yote mawili yapo. Limeandikwa jambazi wako, jamaa wako, kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika naomba unisamehe na bahati nzuri maneno yote niliweka. Hii imenikumbusha siku moja Kiongozi Mkuu wa nchi alikwenda mahali akawa amemteua DC. Sasa wenyeji wale hawajui Kiswahili kama sisi na akaanza kumshukuru huyo Kiongozi. Nakushukuru sana Kiongozi

21 APRIL, 2012

umetuletea jambazi lako hapa, kumbe alikuwa anataka kusema jasiri, yeye akasema jambazi. Kwa hiyo, naomba mnisamehe, hilo nimesema jamaa wako *rather than* jambazi wako.

Halafu kabla hatujahoji kwa kutumia kanuni ya 57 na 58 Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kwa kutumia kanuni ya 57 na 58 nipendekeze mapendekezo ya marekebisho madogo kwenye mapendekezo mawili ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, msingi wa mapendekezo haya...

SPIKA: Kamati gani?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Taarifa ya Kamati ya Miundombinu, ukurasa wa 12 na 13, pendekoz Na. 3.6 na 3.9. Msingi wa mapendekezo hayo...

SPIKA: Naomba Mwenyekiti u-note eeh!!!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ni utata kidogo ambao umejitokeza kwenye maelezo. Huko nyuma wakati wa Bunge la Bajeti Kamati ya Miundombinu wakati inachambua kuhusu huu mradi ilisema mambo mawili ya msingi wakati huo. La kwanza, iliitahadharisha nchi na Bunge kuhusiana na gharama kubwa za mikopo kutoka China na gharama za mradi huu.

La pili, ilielezwa umuhimu wa *PP* katika uwekezaji kama *mitigation*. Lakini kwenye taarifa ya sasa inaonesha maoni ya Kamati ni vice versa kwamba mkopo wa China ndio ambao sasa tunapendekezewa, kwamba Bunge liazimie, tuuchukue moja kwa moja na kwamba utaratibu huo mwingine uachwe.

Sasa kutokana na maelezo yaliyojitokeza ya pande zote, ni vizuri ili Bunge lifanye kazi yake vizuri ya kuisimamia Serikali. Maneno kwenye kifungu cha 3(6): "Serikali ichukue huo mkopo yaondolewe maana sentensi sasa inasomeka "Kutokana na mazingira ya uwekezaji kwenye gati hiyo Kamati inashauri Serikali ichukue huo mkopo mapema iwezekanavyo. Badala yake kuingizwe maneno "Serikali ifanye upembuzi huru (*independent feasibility study*) kuhusu gharama za miradi na ichukue mkopo iwapo maslahi ya Taifa yatakuwa yamezingatiwa". (Makofi)

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo madogo yatasaidia Bunge kuweza kufanya kazi yake vizuri zaidi ya kuisimamia Serikali. Pendekoz

lingine, ni upande wa pendekozo 3.9. Pendekozo hili linaanza na maneno...

SPIKA: Ngoja kwanza tulifanyie maamuzi hili. Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, kama tunafanya maamuzi nimalizie jambo dogo tu kuhusu hili la kwanza.

SPIKA: Nilitaka kwa sababu tunakwenda kifungu, kwani vinahusiana?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Linahusiana na hili, ili Mwenyekiti wakati anajibu aweze kuzingatia. Mapendekozo haya hayaondoi hoja nyingine zote za Kamati kuhusu haja ya kuwajibika kwa Waziri wa Uchukuzi na mambo mengine ila anasaidia Bunge katika kufanya kazi ili uweze kuoanisha maeneo yote ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, mimi kwanza na Kamati yangu tunayakataa mapendekozo hayo kwa sababu zifuatazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunaleta bajeti mwaka jana ikumbukwe kuwa gati 13 na 14 imeanza kuongelewa toka mwaka 2008. Kwa hiyo, ilikuwa ni jukumu la Kamati kuonesha concern, kama kuna tatizo basi tafuteni *PPP* ili tuweze kufanya haraka, hayo ndiyo yalikuwa mawazo ya Kamati. Lakini sasa baada ya kufanya kazi mwaka huu tukagundua wenzetu Serikalini wameshafika mbali, wakaja kutuambia sasa kwamba tayari tumeshafanya *feasibility study*, Wizara ya Fedha tayari imeshatoa *guarantee* na imeshapata mkopo. Tutakuwa Wabunge wa ajabu tukae hapa tuseme tufanye *feasibility study* ambayo maana yake ni nini? Unaposema tunafanya *feasibility study* leo maana yake ni miezi 18 mingine. Bado wenzenu huko Mombasa na Kala wanawasubiri nyie mnahangaika na *feasibility study*.

Mheshimiwa Spika, bado naliomba Bunge lako Tukufu, Serikali imeshafanya *feasibility study*, lakini zaidi ya hapo Serikali yote kuanzia Wizara ya Uchukuzi, *TPA*, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu na ziko barua zote hapa, jambo hili wameanza nalo siku nyingi toka mwaka 2008. Kwa hiyo, kazi yao ilikuwa kuja kutuambia jamani mlituambia haya kwenye bajeti mwaka jana, lakini sisi wenzetu tumeshafanya haya yafuatayo ambayo tukayakubali. Ndio maana kwenye mapendekozo

21 APRIL, 2012

yetu leo sasa tunasema, huo mkopo uchukueni haraka ili tujenge hiyo gati ya 13 na 14. (Makofi)

SPIKA: Taarifa tu Mheshimiwa Waziri

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRIU WA MAJINI): Mheshimiwa Spika, kwa taarifa kwanza, kwa Sheria ya Mamlaka ya Bandari ya Mwaka 2004, kifungu 69 nitaisoma. *"The Minister responsible for finance may with the concurrence of the Minister, meaning the Minister for Transport guarantee the repayment of the principles of and the repayment interest of any loan from any person organization or institution in or outside of Tanzania"*

Mheshimiwa Spika, mimi ndio Waziri wa Uchukuzi. Hapa inasema lazima nihusishwe kabla *guarantee* haijatokea. Sijahusishwa kuhusu *guarantee* hiyo. Hiki ni kipengele kimoja tu kina uvunjwaji wa sheria nyingi sana katika suala zima.

SPIKA: Ah!!!! Ngoja kwanza tunajadili hoja ya Mheshimiwa Mnyika, sio tunajadili kirefu cha hilo, tunajadili kwamba...

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Sio kuunga, unatakiwa ueleze maneno; nini umuhimu wa hicho. Yaani unatakiwa ueleze umuhimu wa mabadiliko anayoleta Mheshimiwa Mnyika, ama upungufu wa maneno anayosema Mwenyekiti, *that's all*. Sio tuingie kwenye debate.

WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika na umuhimu ni kama ifuatavyo:-

Huyu *China Construction Company*; kwa sababu hoja sio mkopo wa *Exim Bank*. Tumesema mkopo wa *Exim Bank* tunaweza tukachukua kama ndiyo mzuri lakini kwanza washindanishwe wajenzi. Huyu CCC ni mjenzi, kesho ingekuwa siko hapa ninawatuma wataalam wamealikwa China. Kuna kongamano la contractors, wamealikwa wakaone ma-contractor mbalimbali ambao wanaweza kushindanishwa China kujengwa gati hii. Zitoke hela za *Exim Bank*, lakini ashindanishwe. Unawashindanisha lini?

Kwanza ni lazima uwe na *feasibility study* ya kwetu wenyewe nimesema hatuna. Pili uwe na *detailed design* ya kwetu wenyewe ndiyo uweze kufanya *estimate* za huu mradi utagharimu kiasi gani. Huu mkopo tutaulipa sisi, *estimate* ikitisema mkopo huu ni Dola milioni 300 kama wengine walivyofanya *feasibility study* pamoja na kuwa tunalipa riba ya *two percent* ni kwa *difference* ya Dola milioni 300 na Dola milioni 543 itakuwa ni *interest*. *Principle* Dola 300, *interest* kabla hujanza chochote tayari ni Dola 243 na ukitia na ile *interest* ya *two percent* mkopo huu hautakuwa *two percent*. Utakuwa ni 77 *percent interest*. Hapo ndipo tutaingia kwenye mkenge.

Mheshimiwa Spika, msukumo wa CCC ulianza magazetini, kinachojitokeza hapa ni muendelezo wa magazeti. Magazeti yamepotosha, Bunge lako linapotoshwa, nilikuwa nasema Kamati ya Miundombinu nilifikiria imeingizwa mkenge, lakini hapa katika ripoti yao kuna kipengele wamesema mkopo huo ukipatikana wa Dola milioni 543 utumike wote usiachwe hata senti moja.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri katika hali ya kawaida tunapotumia kifungu cha 58 hoja ya Mheshimiwa Mnyika anataka kubadilisha maneno yaliyoko kwenye kifungu cha 3.6, kwamba, badala ya ilivyo hivi anasema kwamba kungefanyika *feasibility study; that's all*. Sio hizi habari zote, sisi utatupa tatizo. Sasa Mwenyekiti wa Kamati anasema kwamba hizo *feasibility* zipo. Hiyo ndiyo hoja iliyopo, sio hoja tena ya kuanza kufumua mpango huu, hapana. Mheshimiwa Hamad.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza niishukuru Kamati na nimshukuru sana Mheshimiwa Mnyika. Bara letu la Afrika wengi tunafikiri kwamba mikopo kutoka China ni mizuri na ni rahisi, *is not true*. Kuna vikwazo na mitego mingi. Kwa hiyo, pendekeso analopendekeza Mheshimiwa Mnyika ni sahihi kabisa na kama hatutakuwa *careful* tunafikiri kwamba China ni wale Wachina wa Mao. Wachina wamebadilika, wanafanya biashara tena ya ajabu sana. Mozambique hivi sasa wanashindwa kulipa deni la Wachina kwa sababu ya *trick* zilizotumika katika mikataba na madeni kama haya. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa *very careful*, tukafanya *feasibility study* tukajua tuna-negotiate kwa kitu gani. Tunaweza tukaingiza nchi katika madeni makubwa makubwa. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na pendekeso la Mheshimiwa Mnyika. Mimi nina *experience* nyingi katika haya mambo. Ahsante sana. (*Makof!*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niungane na Mheshimiwa Mnyika kwa sababu kwanza na-declare *interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Ukijaribu

kufuatilia *status* ya jambo hili kuhusiana na Gati 13 pamoja na 14, tayari inabainika wazi kwamba kuna utata. Waziri anaposema kwamba, hawana *feasibility study* yamekuwa ni majibu yake ya siku nyingi. Isipokuwa jambo moja tu ambalo kidogo Mheshimiwa Waziri amekuwa analikosa, Waziri anakuwa anabadilika badilika kwa kauli zake. Leo anawakataa *China Merchants*, lakini nakumbuka tukiwa bandarini, aliwazungumzia na kuwatetea sana watu wa *China Merchants*. Kitu ambacho kilipelekea tuone kwamba huenda Mheshimiwa Nundu ana-*interest* na kampuni ya *China Merchants*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ukija kwa upande wa *TPA* wao wamekuwa wanatueleza kama Kamati. Hii kampuni ya *CCC* wao wana *feasibility study* na *TPA* wamekuwa wanatumia matokeo ya *feasibility study* iliyofanywa na kampuni ya *CCC*. Ndiyo maana nilileta, sijui nilimwandikia Katibu nikimwomba juu ya suala la kutaka kuleta hoja ndani ya Bunge lako kwa sababu ya hizi *contradictions* za pande mbili, iundwe Kamati Teule ya Bunge ya kwenda kuchunguza ili kusudi tujue je, hivi hizi gharama za *CCC* ni za kweli au sio za kweli? Tunaweza wakati mwingine tukajikuta hizi Dola milioni 500 na kidogo ikawa ni gharama kubwa sana iwapo tutaweza ku-*hire* wataalam wetu tukafanya *feasibility study* ambayo itatupa matokeo, kama Taifa tukawa na *feasibility study* ya kwetu ambayo itatupa dira kuliko ku-rely kwenye *feasibility studies* ambazo zimefanywa na makampuni ya nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu likubaliane na ushauri ambao umetolewa na Mheshimiwa Mnyika kwa maslahi ya Taifa letu na hapo tutakuwa tumeenzi kauli ya Mao Tsetung , "No research, no right to speak" kwa sababu *current* tunazungumzia Wizara ya Uchukuzi hata Kamati yetu ya Bunge ya Miundombinu hatuna *feasibility study* ambayo kama Taifa tunaweza tuka-present mahali kwamba na sisi tumejiridhisha katika hili. Inawezekana kukawa kuna *interest* za watu. Kwa hiyo Mheshimiwa Nundu aachane na kampuni yake ya *China Merchants* na *TPA* ku-rely kwenye *feasibility study* iliyofanywa na kampuni ya *China Construction Communication Limited*, tuweke pembeni yote tuanze upya.

Mheshimiwa Spika, niliombe Bunge, nitoe hoja ya kuungana na Mheshimiwa Mnyika. Huu ushauri utatusaidia sana kama nchi. Ahsante.

SPIKA: Usichanganye mambo. Hoja iliyoko mbele yetu ni kuweka mabadiliko ya maneno. Hayo mengine, ya kwenu. Mheshimiwa Shibuda.

MHE. JOHN M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, ni kuhusu utaratibu kwa mujibu wa Kanuni 68(1). Bunge hili linataka kutumika vibaya. Mheshimiwa

Waziri ni Mjumbe wa Kamati, eti mnakuja kubishana hapa, kuvuana nguo, nani mwongo nani mkweli. Kamati inafanya kazi kwa maslahi ya Bunge zima. Ikiwa wajumbe mtaanza kututatanisha tuanze na fikra za kutangatanga tuelewe nini? Mnajenga mgutuko gani? Waziri ni Mjumbe wa Kamati je, hushirikiani na Kamati yako? Litazame kwa umakini, maana yake ni kwamba, viongozi wa Serikali hawana ushirikiano na Kamati, hivyo Kamati zinapotoshwa. Si kosa la Kamati, litakuwa ni kosa la Waziri. Huu ni ulevi wa nini? Huu ni ulevi wa uzalendo gani? Nasema ulevi wa madaraka utalipeleka Taifa hili pabaya. Tafadhalii toa busara na hekima zako.

SPIKA: Mheshimiwa Zitto. Mzingatie issue msiende nje, hii ni hoja maalum.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, naomba nisaidie. Mamlaka ya Bandari ni Shirika ambalo linaripoti kwenye Kamati yetu na mjadala jinsi unavyokwenda tunaweza tukajikuta tunafanya maamuzi ambayo yanaweza yakalitia Taifa hasara sana. Naomba nisikilizwe kidogo. CCC ilifanya *feasibility study* na Mamlaka ya Bandari na ikasema kwamba Gati 13 na 14 itajengwa kwa takriban Dola milioni 325 na wao sasa wanataka kuwa *contractors* na mkopo unatafutwa kwa ajili ya fedha hizo. Hatujafanya sisi kama Taifa an *independent feasibility study* ya kuweza ku-verify kwamba zile gharama ambazo CCC wamezifanya ni gharama ambazo ni sahihi na ndizo ambazo zinaweza kutupelekea kuweza kufanya mradi ule. Mwaka jana wakati wa bajeti hapa nakumbuka tulizungumza kwenye Hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni na baadhi ya Wabunge kwamba, ni vizuri kabla ya kukimbilia kwenye mkopo tuweze kujiridhisha na gharama ambazo zitakwenda kujenga gati lile.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwamba Waziri, Mheshimiwa Nundu akawa ana makosa, inawezekana kabisa. Lakini mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Twendeni tukafanye an *independent feasibility study* kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Mnyika anavyopendekeza. Lakini ifanyike haraka na nakubaliana kabisa na Kamati ya Miundombinu kwamba ucheleweshaji huu unaweza kutuingizia hasara kubwa sana na tukichelewa, kwa mfano, *feasibility study* ikichukua mpaka mwezi wa saba huko, tutakuwa tumpoteza kabisa. Kwa hiyo tunaweza tukakubaliana kama Bunge tuiagize Serikali na tuiombe na Kamati wakae wakubaliane, wapeane mwezi au miezi miwili watafute kampuni *independent* kabisa na hawa Wachina wafanye *feasibility study*, iweze ku-verify zile gharama ambazo zipo ili baadaye sasa tuweze kwenda katika process ya ujenzi. Naomba tuwe sober katika uamuzi huu, tusipokuwa sober tutajikuta tunaingia kwenye hasara kubwa sana. Kwa hiyo, kuna mantiki katika hoja ambayo Mheshimiwa Mnyika

amezungumza na naliomba Bunge lako Tukufu liweze kukubaliana na hoja hiyo. Hicho ndicho kilichonileta humu ndani.

SPIKA: Sasa ya mnyonge mnyongeni sisi hatuko huko. Mheshimiwa Engineer Makani. Hoja ni ile ya Mnyika kwamba katika mapendekezo ya Kamati wabadilishe maneno fulani. *That's only hoja hapa.*

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nakwenda moja kwa moja. Kwanza kabisa nataka niseme suala hili ni la kitalaam zaidi. Hata tunaposema *feasibility study*...

SPIKA: Samahani kidogo, Waheshimiwa Wabunge nimekuwa *taken* na mambo hapa, naomba nitumie nafasi hii kutumia kifungu cha 28(5) kuongeza nusu saa kusudi tuweze kumaliza.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata tunaposema kwamba *feasibility study* ndiyo ilizaa hiyo *tender price* au hiyo gharama si sahihi sana na kama ilifanyika hivyo kuna tatizo. Lakini taarifa tulizonazo ambazo zililetwa kwenye Kamati ni kwamba walifanya *feasibility study* ikakamilika, wakafanya *preliminary design* na wakakamilisha na *detailed design* halafu baadaye hiyo ndiyo inazaa gharama za mradi. Jambo hili kwa ujumla wake linahusiana na taratibu za manunuzi ambazo ziko za aina mbili, nitaje mbili ambazo ndiyo za haraka haraka zilizotumika. Moja ni ile ya ushindanishi ambayo anazungumzia Waziri. Lakini nyingine inakuwa ni ya *single source* ambayo inaweza kuwa wakati mwingine inatokana na *experience* ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, sasa katika uzoefu wa Taifa iko miradi ambayo tuli-procure kutoka Serikali ya China moja kwa moja, kama ujenzi wa Mkonga wa Taifa ambao unaendelea, ujenzi wa Uwanja wa Taifa ambayo haya mawili yanatokana pia na ukweli kwamba fedha zinazotakiwa kutumika hapo zinakuwa ni fedha za mkopo kutoka Serikali ya China kupitia *Exim Bank*. Sasa ni kweli pia kwamba uki-rely kwa gharama au kwa makisio ambayo yanatokana na yuleyle anayetaka kukupa huduma halafu wewe ukawa hujafanya chochote ni *risk* kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa kufanyika mara nyingi ni kwamba, tunatarajia Bandari wenyewe wanayo *internal capacity* ya kuweza ku-verify kuanzia *feasibility study, design* pamoja na *determination of costs*. Sasa kuna *stage* moja ambayo bado sikupata taarifa kamili kwamba je, Serikali kupitia Bandari walijiridhisha kwa kutumia *internal capacity* kuona kwamba ile *estimates* iliyo tajwa na wale ambao wanatupa hiyo *offer* kama kweli iko sahihi. Kama kweli hiyo *gap* ipo basi

21 APRIL, 2012

marekebisho yale anayosema Mheshimiwa Mnyika ni sahihi. Kwamba ni element ndogo hiyo.

SPIKA: Namwongezea muda kwa sababu ya utaalam wake.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, kwamba tunautaka ule mkopo vizuri sana, tunataka kujenga hizo gati mbili haraka sana lakini kwa gharama ambayo itakuwa kwa manufaa ya Taifa. Kwa hiyo, haitatugharimu sana kama hicho hakikufanyika. Maana hiyo sina *information* hapa sasa hivi kwa haraka. Kama hicho kweli hakikufanyika cha kufanya *verification* kwa kutumia *internal capacity* basi hiyo ni element muhimu sana tunatakiwa kuifanya. Hatuwezi kupokea tu gharama kama ilivyotolewa na yule anayetakiwa kutupa *offer*. Inaweza ikatupa hasara. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, ikiwa kweli hatukufanya *verification* kwa kutumia *internal capacity* basi hilo lifanyike haraka halafu tuweze kuchukua huo mkopo haraka sana. Kwa hiyo, marekebisho yanasema kwamba tujiridhishe. Kwa hiyo, watusika watafanya utaratibu wa kujiridhisha halafu tuchukue mkopo, *without which* ni kweli ni *risk*.

SPIKA: Naomba nimpatie Mwenyekiti tumalize.

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, Engineer Makani ameeleza vizuri na kwa kweli haya yote sisi tumeambiwa yamefanyika, lakini kwa sababu ya Bunge nakubali tubadilishe pale kwamba kabla hatuja-*finalise* huo mkopo na hiyo kazi kuanza, *TPA* wajiridhishe na wao waone kama kweli hizo gharama ambazo *real* zitakazojenga, ingawaje tunajua wamejiridhisha. Lakini nasema tubadilishe ili wajiridhishe. Hilo moja. Lakini Kamati yako tumehangaika na hili jambo toka mwaka jana, nataka tuelewane vizuri. Hivi leo Wizara inakuja hapa inasema haijafanya *feasibility study*. Mwaka jana walikuwa kwenye bajeti hawakuweka fedha za *feasibility study*.

SPIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo siyo hoja yenewe. Unaanza ku-debate sasa.

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nakubali tuseme wajiridhishe kabla hatujamalizia huo mkopo.

SPIKA: Mheshimiwa Mtoa Hoja.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Wabunge waliounga mkono hoja hii na nashukuru sana kwa ushauri wa kitaalam wa *Engineer Ramo Makani* ila niombe tu *verification* isifanywe na *TPA* kwa sababu ni *interested part*. Kwa hiyo, ifanyike *independent verification*, hiyo itaweza kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba, naomba nirudie na Wajumbe wa Kamati wanielewe. Mapendekezo haya hayaondoi matatizo ambayo Waziri, Mheshimiwa Nundu ameyafanya katika mchakato huu. Kwa hiyo, hizo taratibu zake zitaendelea, lakini ni vizuri nayo Bunge likawa salama. Nashukuru sana na naomba Wabunge waunge mkono hoja niliyoitao.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ukiweka yale maneno aliyosema Mheshimiwa Mnyika hayana hasara kabisa. Kama ni wasiwasi tulionao kwamba time factor kila kitu lazima twende kwa speed kadri inavyowezekana, ndiyo efficiency. Lakini mimi nafikiri tukubaliane na maneno aliyojasema Mheshimiwa Mnyika hayabadilishi taarifa ya Kamati isipokuwa yanatoa kinga kidogo kama kuna kitu kisichokwu chenyewe. Kwa hiyo nitawahoji.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Mapendekezo Yaliyopendekezwa na Mheshimiwa John Mnyika
Yalikubaliwa na kuingizwa kwenye Taarifa ya Kamati*)

SPIKA: Wabunge wote wameunga mkono, kwa hiyo kifungu kile cha 3(6) kitabadilika kama alivyowasilisha Mheshimiwa Mnyika. Baada ya hapo kifungu cha 3(9).

TAARIFA

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

SPIKA: Tuko kwenye kufanya maamuzi. Mheshimiwa Mnyika, rudia 3(9).

MHE JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa tumekubaliana kwenye kifungu cha 3(6) msingi wa kifungu cha 3(9) ni ule ule kwa sababu kwa mujibu wa ripoti ukurasa wa 13 inasema: "Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato wa kupata mkopo umekamilika Kamati inashauri ujenzi wa gati hii uanze mara moja." Kwa hiyo, tukishafanya marekebisho kwenye kifungu kile ambayo tumeshayafanya

tayari naomba vile vile tufanye marekebiso kwenye kifungu cha 3(9) tuondoe maneno: "Kwa kuwa mchakato wa kupata mkopo umekamilika" hayo maneno yaondolewe, badala yake yawepo maneno: "Tathmini ifanyike kuhusu mchakato wa kupata mkopo na iwapo masharti ya msingi yamezingatiwa." Halafu maneno yaliyopo kwenye taarifa ya Kamati yaendelee, Kamati inashauri na kadhalika ili yaweze kuendana na marekebiso ya 3(6).

Mheshimiwa Spika, marekebiso yale ya 3.6 yaweze kuendana vile vile na marekebiso ya 3.9. Kwa hiyo ni suala la *principle* tu, maneno yanaweza kubadilika, lakini tukishakubali hiyo *principle* ya 3.6 inaathiri vile vile 3.9.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Enhe, Mheshimiwa Mwenyekiti!

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Uzingatie tumebadilisha 3.6.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Tumebadilisha kwa kusema twende tutafute *independent* mtu ambaye ata-*verify* ile *feasibility study*, ndiyo tulichokubaliana. Lakini kuniambia sasa tusiendelee na mkopo, tuukatae, nashangaa sana! Maana ndicho alichosema!

SPIKA: Hapana! Ngoja aseme basi tumsikilize. Eleza Mwenyekiti ulivvosikia wewe.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: *Unless* sikumsikia, labda arudie.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika, hebu rudia tena!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasema tukatae mkopo ila ninachoomba tu tuweke *caveat* kwa sababu tukisema, kwa kuwa mchakato wa kupata mkopo umekamilika na bado tunaona kwamba kuna mambo yanahitajika kufanyiwa *verification*, kuna *doubt* hapo katikati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili tuiondoe hiyo, tuweke maneno hapa mwanzoni yatakayoweza kurekebisha hilo jambo. Lakini kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha na hili lingehusu zaidi Waziri wa Fedha au lingehusu upande wa Serikali kwa ujumla wake, akiweza kutuambia kwa mujibu wa utendaji wa Kiserikali, suala la mkandarasi na upembuzi yakinifu ni tofauti na *process* ya mkopo na *guarantee* ya dhamana ya

Serikali kwenye mkopo. Kama hivi vitu viwili ni tofauti kabisa, basi haya marekebisho yanaweza yasiwe ya muhimu sana. Lakini kama hivi vitu vinaoana, yaani upembuzi yakinifu na mkandarasi aliyefanya ghamara na kila kitu na process ya nchi yetu kuweka dhamana kwenye huo mkopo, kama vinaoana, kunahitajika baada ya marekebisho ya 3.6 na 3.9 nayo irekebishwe ili kuweza ku-harmonize hayo marekebisho, lakini sisemi kwamba tukatae mkopo.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli tumefanya marekebisho kwenye 3.6 ambayo maana yake ni kwamba, tumerudisha nyuma kidogo ile stage tuliyokuwa tumefikia awali, kwa kuwa yale marekebisho tuliyopendekeza hapa yatataka muda kidogo, *of course*. Kwa hiyo, 3.9 inabadilika, lakini inabadilika kidogo tu kwamba badala ya kusema “kwa kuwa mchakato umekamilika”, tuseme “mchakato wa kupata mkopo ukikamilika au utakapokamilika”, yanayobaki yote yaendelee. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Cheyo! Maana yake na muda wenyewe una matatizo! Ninachokisema hata kubadilisha hii tunabadilisha tu, lakini kutokana na 3.6 tuliyobadilisha, 3.9 inabadilika kwa kweli kwamba kama kulikuwa na *guarantee* ya Serikali, basi itegemee matokeo ya 3.6. *That is what we are saying.* (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Kuhusu nini, nimeshamaliza hiyo! Kwanza nimwache Mheshimiwa Cheyo halafu Mheshimiwa Chenge.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Msiturudishe huko nyuma.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa sababu Kamati yangu mojawapo ya mambo iliyoleta ni jinsi hizi dhamana or guarantees zinavyotolewa na Serikali. Kwa kuwa tumeona pia *linkages* hizi, yule anayetumia mkopo (*contractor*) ndiye anakwenda ku-organize mkopo, Serikali inagharamia na hakuna ushindani kati ya yule mtu anayefanya hiyo kazi. Sisi tunalipa mkopo *and a very clear example* ile ya *Songas* mpaka leo tunalipa *284 billion*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka hapo, katika hicho mnachofanya, muweke *caveat* pia kwamba utaratibu wa kupata mkopo uwe tofauti na utaratibu wa kutoa *tender* ya kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo, hivi vitu vindikuwa *independent*. Serikali itafute mkopo, halafu huyu

tenderer wanashindanishwa katika njia ambayo kanuni zetu na sheria zetu zinavyotaka. Mkiya-link hayo kwa pamoja ndiyo hivyo tutakuwa na gharama nydingi kubwa ambazo hatuzielewi. Huo tu ndio ulikuwa wasiwasi wangu na kama kunaweza kuwa na jambo linaloweza kufanywa hapo, itatusaidia sana. mkopo uje lakini *contractor* washindane.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Chenge kidogo, nina dakika tatu tu.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sikusimama kwa ajili ya mjadala huu. Nimesimama tu kuomba mwongozo wako. Mheshimiwa Mnyika katumia kanuni ya...

SPIKA: Kanuni namba 57 na 58!

MHE. ANDREW J. CHENGE: 57. Sasa, kanuni hiyo ukiisoma, inatueleza ni nini cha kufanya. Labda nisome tu kwa faida: "Hoja ikishatolewa ili iamuliwe, inaweza kubadilishwa kwa (a) kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine, (b) kuondoa maneno fulani bila kuongeza mengine au kuingiza au kuongeza maneno mapya". Inaendelea: "Kabla ya kutoa hoja hiyo, mtoa haja atamkabidhi Katibu maandishi yenyeye sahihi yake yanayoonesha mabadiliko anayoyataka yafanyike".

Mheshimiwa Spika, sasa Bunge linaletewa mabadiliko ya maneno kwa mdomo, bila maandishi! Ndiyo maana nimeona tunawasumbua Waheshimiwa Wabunge kwa sababu hakuna kitu cha maandishi! Lakini, tumeshali amulia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa masikitiko makubwa sana nasema Kanuni hizi tusipoweza kuzizingatia, itakuwa inatusumbua sana baadhi yetu. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Maneno ameyaleta na ninayo na ndiyo maana niliyaruhusu. Labda anachokisema Mheshimiwa Chenge kwamba kingechapwa, kikasambazwa kwa wote. Nadhani hiyo ndiyo *point*. Lakini kama kupata, nimepata. Nadhani kutokana na mtiririko wa majadiliano na ule ubishani uliotokea, yeye akaona aende haraka. Kwa hiyo, hata mimi mwenyewe nilifikiria akachape, lakini nikaona muda niliokuwa nao mpaka achape, mpaka arudi, ulikuwa hautoshi.

Mheshimiwa Spika, lakini, kimsingi, kutokana na kwamba, naamini Serikali kwa upande wake itakwenda kuliangalia kwa sababu bado halijakaa vizuri vichwani mwetu. Yaani ukikaa hivi, pamoja na maneno yote tunafanya mazuri, lakini unaona hili suala halijakaa vizuri. Kwa hiyo, nafikiri kwa sababu Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali yupo, hili suala

halijakaa vizuri hata kama tunapitisha vineno hapa, halijakaa vizuri, linatusumbua sana wengine vichwani hapa. Kwa maana hiyo basi, naomba niwahoji kuhusu maoni ya Kamati zote kwamba Bunge sasa lipokee na kuzikubali taarifa za Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Bunge ya Miundombinu pamoja na marekebisho yaliyofanyika na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Sasa tunaomba taarifa za Kamati hizo zikubalike!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki na kupokea mapendekezo yaliyomo ndani
ya Taarifa za Kamati zilizojadiliwa Bungeni)*

SPIKA: Taarifa za Kamati hizo zimekubalika na ni ombi langu kwa Serikali, muda hatukuwa nao, hizi taarifa za Kamati wameandika kwa kirefu sana, lakini muda waliopewa ulikuwa mfupi sana. Muda wa kusoma haukuwepo, muda wa kujadili pia haukuwepo. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukue taarifa hizi, kila sekta wazifanyie kazi halafu tupewe majibu yaliyoandikwa kusudi wote tuweze kujua Serikali imejibu nini. (*Makofi*)

Wakati huo huo mkumbuke kwamba tunaingia kwenye kipindi cha bajeti. Naamini kabisa Mawaziri pia watachukua concerns za Wabunge katika maeneo mbalimbali katika utaratibu wa kuandika hotuba zao. Kwa hiyo, hili ndiyo ombi langu.

Baada ya kusema hivyo, nina tangazo moja tu, muda sina. Wabunge wanawake wa CCM wanatakiwa wakutane sasa hivi kwenye Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya shughuli zao.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nitaahirisha kikao mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.29 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,
Tarehe 23 Aprili, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*